ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais Kuteuliwa na Rais
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/ Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe

15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni, Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake

37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
57.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
58.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
59.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Saba – Tarehe 25 Juni, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ali Salum Haji (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 48

Wafanyabiashara Kutozwa Ada za Usafi

Mhe. Ismail Jussa Ladhu – Aliuliza:-

Baraza la Manispaa Zanzibar limekuwa likiwatoza wafanyabiashara na wakaazi wa Mji wa Zanzibar ada ya ukusanyaji taka kila mwezi. Hata hivyo, mitaa na maeneo mengi ya mji, hasa ndani ya Mji Mkongwe imekuwa haisafishwi na taka huachwa zikizagaa na kurundikana, hali inayochafua mazingira, kuharibu haiba ya mji na hata kuitia aibu nchi yetu mbele ya macho ya wageni wanaoitembelea.

(a) Je, iwapo serikali kupitia Baraza la Manispaa, imeshindwa kuifanya kazi hii haioni kwamba ni kuwadhulumu wafanyabiashara na wananchi kwa kuwatoza ada kwa huduma ambayo haitolewi.

(b) Kutokana na Baraza la Manispaa kushindwa kuifanya kazi hii, serikali iko tayari kuwaruhusu wananchi wenyewe kuunda vikundi vya kuiweka safi mitaa na maeneo yao na wao kutoza ada hizi, ili ziwahudumie wale watakaoifanya kazi hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 48 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Baraza la Manispaa linatoza ada ya huduma za usafi (service charge) kwa wafanyabiashara na wakaazi wa mjini kwa mujibu wa Kanuni ya Manispaa (*Sewerage Drainage and Solid Wastes*) iliyochapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali Vol.CX15 N.6156 ya tarehe 23 Juni, 2006.

Madhumuni ya ada hiyo ni kuhakikisha huduma za usafi katika maeneo ya mijini zinakuwa endelevu, kwa kuwashirikisha wananchi na wadau mbali mbali hasa wafanyabiashara, ambao huwa wanazalisha taka kwa wingi kutokana na shughuli zao wanazozifanya.

(b) Kwa kuwa usafi wa mji unaweza kufanikiwa kwa mashirikiano ya pamoja baina ya Manispaa na wananchi. Hivyo, Manispaa iko tayari, na imeshashajihisha Vikundi vya Mazingira zaidi ya 17 kwa lengo la kushirikiana na kutoa huduma za usafi katika Shehia za Wadi zote za Mjini.

Baraza la Manispaa limeanzisha utaratibu wa kufunga mikataba na vikundi mbali mbali, ili kuwa mawakala katika kukusanya ada, kuimarisha takwimu na kutoa huduma za usafi. Vile vile Baraza la Manispaa halimzuii mtu au taasisi yoyote ambayo ipo tayari kushirikiana nayo, katika kuendeleza huduma za uzoaji taka katika maeneo ya miji, ilimradi tu ziwe zimefuata taratibu zilizopo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru pamoja na Mhe. Waziri kwa majibu yake, naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Baraza la Manispaa linajumuisha eneo kubwa sana la Mji wa Zanzibar, lakini inavyoonekana ni kwamba limejikita zaidi katika tozo za aina mbali mbali zikiwemo za usafi katika eneo la Mji Mkongwe kuliko maeneo mengine. Matokeo yake kumekuwa na upandishwaji wa bei hizi kila mara. Kwa mfano, baadhi ya maduka hivi sasa imeshafikia kutozwa shilingi 19,000/=, pia kuna nyumba ambazo zinatozwa shilingi 3,000/=.

Je, Mhe. Waziri haoni kwamba kufanya taratibu hizi kwenye eneo moja tu la Mji, ni kuendesha ubaguzi dhidi ya kazi fulani suala ambalo lilipaswa kufanyika kwa wakaazi wote wa Mji wa Zanzibar.

(b) Kwa kuwa wamekubali kwamba serikali haina pingamizi ya kushirikiana na wananchi katika maeneo yao kufanya masuala ya usafi, na ameeleza utaratibu wa kuwa na mikataba na Baraza la Manispaa, ili kusaidiana katika kazi hii.

Hivi anaweza kuliambia Baraza hili la Wananchi kupitia Baraza hili ni kiasi gani ya tozo hizo au asilimia ngapi inategemewa iende kwa vikundi hivi, na asilimia ngapi iende kwa Baraza la Manispaa, ambalo limeonekana limeshindwa kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwanza omba kumhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba Baraza la Manispaa kama taasisi nyengine yoyote ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haifanyi kazi kwa upendeleo wala ubaguzi. Tatizo ni kwenye utendaji tu, nafikiri wewe mwenyewe ulikuwa mtendaji, na unafahamu matatizo ya kiutendaji, yaani hapa kuna *efficiency one hundred percent*, huku una *efficiency seventy five percent*, na huku kuna *efficiency* asilimia 40 na hayo ndiyo matatizo ya kiutendaji.

Lakini ninachokiomba Mhe. Mjumbe wewe mwenyewe umeona, kwa sababu ni Mwakilishi na ninakupongeza kwa kufuatilia haya matatizo uliyoyaona. Kwa hivyo, tukitoka hapa mimi niko tayari nitakufuata na kule kwenye kasoro basi utuelekeze, ili tuweze kurekebisha na tutakaza kamba au soksi zetu na mambo yote yaende vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mapato, takwimu hizo sina na wala simfichi Mhe. Mjumbe. Kwa kweli wenzetu wanajitahidi kujiimarisha katika ukusanyaji wa mapato, na mwanzo tulikuwa na tatizo kidogo la risiti, na hivi sasa tayari tumesha-*centralize* risiti zote zile, lakini bado nakubali *loop hole* zipo.

Kutokana na hali hiyo, hivi sasa tumeandaa mpango mzima wa kuipitia, pamoja na kupitia upya mwenendo wake, utaratibu wake pamoja na wafanyakazi wake, kwa lengo la kuona kwamba wanasafisha mji na pia vyanzo vya mapato vinapatikana kama inavyostahiki.
Mhe. Naibu Spika, Mji Mkongwe kuna vyanzo vingi vya mapato. Kwa kweli mimi mara nyingi Mhe. Naibu Spika namuomba Mhe. Mjumbe tukae pamoja, kwa sababu yeye ndiye mwenye mji na anakuona kulivyo. Kwa hivyo, namuomba tena kwa sababu yeye ndiye mwenye Mji Mkongwe na ndio kioo chetu, kwa hiyo tusaidiane katika kupanga na sisi tuko *very flexible* wizarani na tuko tayari tutakufuata.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri ameeleza kuwa ni kweli kwamba ipo Kanuni ambayo imechapishwa na Gazeti Rasmi la Serikali kuwa Baraza la Minispaa linao uwezo wa kukusanya kodi hizo.

Vile vile kutokana na hali halisi wananchi au wenye maduka wanatoa fedha kwa mujibu wa vile viwango walivyoekewa, lakini huduma ya usafishaji hakuna. Je, huoni kukiuka haki za mtoa kodi na kudhulumu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba hatuna lengo la kubagua watu, na zile huduma wapate wote. Kwa kweli mara nyingi huwa ninasema kwa mfano hakusafishwi basi sote tungeona hali, lakini wenzetu wanajitahidi, isipokuwa tunakubali kwamba wanayo matatizo ya vifaa.

Mhe. Naibu Spika, tunashukuru ule Mradi wa *Zanzibar Urban Services Project (ZUSP)* utakuja kutusaidia gari, vifaa vya kuburura ambavyo vinapita mjini kote, yaani utatusaidia zana nyingi, na utakuwa ni mradi mzima na utaona Mhe. Mjumbe mpaka Kwahani taa zitawaka kule. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Mji Mkongwe ni sehemu moja ya kukusanya mapato na ina majumba mengi ya kuweza kuleta mapato. Je, makusanyo ya Mji Mkongwe yanakwenda vizuri kuhusu majumba yale.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema, lengo letu wazungu kupata mapato kwa kiwango kikubwa kwa kukusanya kodi. Kwa hivyo, kukusanya kodi si rahisi yaani kuna ufundi wake, na ile ni sayansi ile na wala sio mtu yeyote unaweza kusema na kumpa na kukusanya kodi.

Sasa tunajitahidi kuwafunza watu wetu, ili wasirubunike na wala wasiwe na tamaa, wakusanye kodi na hao wenye maduka nao pia wamepangiwa. Mhe. Naibu Spika, kuna mizozo kidogo kwamba kodi tunayotoza sisi, kodi inayotozwa na *ZRB*.

Lakini kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha tunafanya mapitio sasa, ili tuone hizi kodi wanazolipa wenye maduka haziwakomoi na wala sio nyingi, na lengo tusiwakamue wananchi wetu. Kwa hivyo, haya mambo tunayarekebisha tuone kodi inayostahiki kwa Manispaa inakusanywa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibiwa swali langu Nam. 194 naomba uniruhusu kwa heshima na taadhima kubwa kutoa mkono wa pole, kwa kupoteza kiongozi mahiri Shirika la Bandari marehemu Moh'd Salum kwa kifo cha ghafla Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema peponi Amin.

Nam. 194

Mashirika ya Umma Kutokurekebishiwa Mishahara Yao

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya marekebisho ya mishahara katika mwaka wa fedha 2011/2012, kwa watumishi wa umma. Lakini hadi sasa bado hayajaanza kuwanufaisha wafanyakazi wa Mashirika ya Umma.

(a) Ni sababu gani zilizopelekea hadi sasa wafanyakazi wa Shirika la Bandari kutofanyiwa marekebisho yao ya mishahara.

(b) Kwa kuwa tatizo hili limeathiri Mashirika mbali mbali ya Umma, ni lini marekebisho yao yatafanyika, ili kuondoa kilio cha muda mrefu cha wafanyakazi wa mashirika hayo.

(c) Kwa kuwa Mashirika ya Umma yana mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi. Je, serikali kuchelewa kuwafanyia marekebisho ya mishahara yao haioni kuwa inawavunja moyo na kuzorotesha uwajibikaji katika maeneo yao ya kazi.

(d) Tangu serikali kufanya marekebisho ya mishahara ya ngazi, ni mashirika mangapi ambayo bado hayajafanyiwa marekebisho hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-
Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 194 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-
Kwanza kabisa nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mjumbe kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya marekebisho ya mishahara katika mwaka wa fedha 2011/2012 kwa Watumishi wa Umma. Hata hivyo, sikubaliani na kauli ya Mhe. Mjumbe kwamba, hadi sasa marekebisho haya hayajaanza kuwanufaisha wafanyakazi wa Mashirika ya Umma.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Wafanyakazi wa Shirika la Bandari tayari wamefanyiwa marekebisho ya mishahara, ingawa serikali ilitenga kima cha chini cha mshahara cha shilingi 125,000/= kutoka shilingi 100,000/= katika mwezi wa Oktoba, 2011. Kwa wakati huo wafanyakazi wa shirika hilo wao wakipata kima cha chini cha mshahara cha shilingi 156,000/= kwa kundi A na shilingi 144,000/= kwa kundi B, marekebisho haya yalifanyika Januari, 2011.

    Katika mwezi wa Januari, 2012 Shirika la Bandari liliongeza tena mishahara, na wala hakuna mfanyakazi wa Shirika la Bandari anayepata chini ya shilingi 229,000/= kwa mwezi, ingawa mishahara hii ilichelewa kulipwa, lakini tayari malimbikizo yote ya miezi mitatu Januari hadi Machi, 2012 wameshalipwa.

(b) Utekelezaji wa zoezi la marekebisho ya mishahara kwa mashirika ni tofauti na utekelezaji katika mawizara, kwa sababu shirika linatakiwa lizalishe, ili kuweza kujilipa. Kwa hivyo, hata marekebisho ya mishahara, ni lazima yazingatie uwezo wa shirika kifedha na sio kufanya marekebisho tu.

    Mhe. Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba, marekebisho ya mishahara kwa mashirika yatafanyika mara itakapohakikishwa kuwa uwezo wa mashirika hayo kutekeleza zoezi la Marekebisho ya Mashirika ni mzuri.

(c) Pamoja na kwamba marekebisho ya mishahara kwa mashirika hufanywa na mashirika yenyewe kwa kushirikiana na Bodi zao za Wakurugenzi. Hata hivyo, wizara yangu imeyaandikia mashirika yote kuwasilisha kwetu marekebisho ya mishahara, pamoja na Miundo yao ya Utumishi, ili kufuatilia kwa karibu zaidi utekelezaji wake.
(d) Tangu serikali ifanye marekebisho ya mishahara hakuna Mashirika ya Umma ambayo hayajafanya marekebisho ya mishahara.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana Mhe. Waziri atakubaliana nami kabla hajakuwa kwenye kiti cha Uwaziri alikuwa ni Mjumbe wa Shirika la Bandari kwa vipindi viwili mfululizo, siri yote ya Shirika la Bandari anaijua.

Katika shirika linalofanya kazi katika mazingira magumu ni lile, yaani vipindi vitatu kwa siku, na kazi wanazozifanya ni hatarishi ukilinganisha na mashirika mengine, baada ya Shirika la Bandari la pili ni Shirika la Umeme, mshahara wao ni sawa na Shirika la Meli, ambapo Shirika la Meli halijiendeshi. Hivi haoni ni kuwaonea wafanyakazi wa Shirika la Bandari.

Katika majibu ya Mhe. Waziri, ili shirika liweze kujiendesha zaidi ni lazima lizalishe vizuri pamoja na kulipa mishahara. Mhe. Naibu Spika, naweza kusema Shirika la Bandari pengine ni namba mbili kwa kuingiza kipato. Je, ni suala gani lililopelekea kupewa mshahara mdogo wale wafanyakazi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba kabla sijawa katika nafasi hii ya uwaziri nilikuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Bandari. Kwa maana hiyo, naelewa vyema utendaji na mazingira ya kazi ya Shirika la Bandari kwa jumla. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sikubaliani na Mhe. Mwakilishi kwamba wafanyakazi wa Shirika la Bandari hawalipwi kulingana na mazingira magumu ya kazi zao.

Nakubaliana naye katika jibu la mwanzo kwamba mimi nilikuwa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Bandari, ndio maana wakati nilipokuwa nikijibu swali lake nilisema hivi, kwamba Shirika lolote la serikali linatakiwa lilipe maslahi ya wafanyakazi au lijiendeshe kutokana na faida ya biashara ya shirika inavyokwenda. Kwa maana hiyo, malipo wanayolipwa wafanyakazi wa Shirika la Bandari yanaendana na faida na uendeshaji wa Shirika lenyewe linavyokwenda la Bandari.

Mhe. Naibu Spika, kwa msingi huo katika kuweka umuhimu wa kuwalipa watumishi wa Shirika la Bandari, si tu kuwalipa mishahara, lakini kuzingatia kuwepo kwa vitendea kazi kwa ajili ya kuendesha shughuli za *operation* ya Shirika la Bandari.

Vile vile nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba, Shirika la Bandari wanawalipa vizuri wafanyakazi na kwa ushahidi nilionao kwamba wafanyakazi wanalipwa mishahara kwa mujibu wa biashara inayofanyika. Mhe. Naibu Spika, lakini wakati huo mwisho wa mwaka, yaani kila mwaka wafanyakazi wa Shirika la Bandari wanao utaratibu wa kulipwa *bonus* kutokana na faida ambayo linapata Shirika la Bandari, mbali ya ile mishahara wanayolipwa kila mwezi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pia nikimpongeza Mhe. Waziri kwa dhati kwa namna majibu yake alivyoyatoa namna Shirika la Bandari anavyolielewa.

Mhe. Naibu Spika, swali langu liko hivi karibuni baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Bandari walifanya mgomo, na kusababisha meli zinazotoka nje kutopakuliwa mizigo yake hapa na badala yake kwenda Dar-es-Salaam, na walifanya hivyo baada ya mishahara yao kuwa tayari imesharekebishwa, kitendo ambacho kilisababisha hata mpenzi Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwenda kule kwa ajili ya kufuatilia matatizo hayo.

(a) Katika mgomo ule wa wiki moja shirika lilipata hasara kiasi gani.

(b) Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alipokwenda kule alisikia kilio cha wafanyakazi na wakati huo ilikuwa tayari wameshalipwa mshahara kama Mhe. Waziri alivyoeleza. Je, malalamiko yale yamechukuliwa hatua gani. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora mpaka sasa haina taarifa ya mgomo uliokuwa umefanywa na wafanyakazi wa Shirika la Bandari. *(Makofi)*

(a) Shirika lilipata hasara gani katika kipindi hiki. Kwa kuwa wizara yangu sio inayosimamia Shirika la Bandari, itakuwa ni vigumu sana kuweza kusema shirika hilo limepata hasara gani. Hata hivyo, kama Waziri wa Serikali, basi nitashirikiana na wizara husika, ili niweze kujua kama shirika katika kipindi hiki limepata hasara au faida na hatimaye tuweze kumjibu Mhe. Mwakilishi kwa maandishi.

(b) Malalamiko ambayo yalilalamikiwa kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na wafanyakazi wa Shirika la Bandari, malalamiko hayo nasema kwenye Wizara ya Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora bado hayajaja, inawezekana malalamiko hayo yapo ndani ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.
Hata hivyo, kwa kuwa suala hili nimelisikia hapa, wizara yangu itawasiliana na wizara husika, ili kujua kama kuna malalamiko yoyote ambayo yamefikishwa kwao tuweze kuyashughulikia kwa pamoja.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa serikali imefanya marekebisho ya mishahara kwa Watumishi wa Umma katika mwaka wa fedha 2011/2012. Kwa kuwa wafanyakazi hawa walifaidika na mishahara hii kwa muda wote mpaka leo. Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya wafanyakazi kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali mwezi wa Mei, 2012 wanaendelea kufaidika na mishahara hiyo, lakini mwezi huu wa Juni, 2012 wamekatwa mishahara yao kwa kiasi kikubwa.

(a) Je, kuna taarifa gani kuhusu mkato huu.

(b) Je, Mhe. Waziri ikiwa mikato hii itaendelea kukatwa, si wakurudisha nyuma wafanyakazi hawa wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kuwavunja moyo katika kazi yao ngumu ya kusomesha.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, najua kwamba wako wafanyakazi na sio wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali peke yao, lakini wa taasisi mbali mbali, ambao mishahara yao imechukuliwa hatua ya kukatwa.

Mishahara hiyo imekatwa kwa sababu marekebisho ya mishahara tuliyoifanya tumefuata taaluma za wafanyakazi husika. Kwa mfano, wafanyakazi ambao wameweka kwenye madodoso yao *qualifications* ambazo hawana, yaani wameweka viwango vikubwa vya elimu kuliko hali halisi ilivyo, basi wafanyakazi hao wamechukuliwa hatua ya kukatwa mishahara yao. Lakini kama wapo wafanyakazi ambao wamekatwa kinyume na taratibu hizo, basi wizara yangu itachukua hatua za kurekebisha.

Kutokana na hali hiyo, napenda kusisitiza kwa mfanyakazi yeyote ambaye katika dodoso lake aliweka *qualification* ambayo hana, basi serikali itachukua juhudi ya kukata mshahara huo, na fedha hizo zitarudi serikalini. Vile vile katika mwaka huu wa fedha, wizara yangu inakusudia kuangalia kuanzia pale ambapo alianza kudanganya mfanyakazi huyu na fedha hizo ziweze kurudi serikalini. *(Makofi)*

Nam. 32

Uchimbaji Kifusi Makaani (Vitongoji)

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-
Kwa kuwa kumekuwa na uchimbaji mkubwa wa mawe na kifusi kunakofanywa na wizara hii katika maeneo ya Makaani – Vitongoji katika Jimbo la Wawi. Kwa kuwa uchimbaji huo umekuwa mkubwa kiasi cha kusababisha kuzuka kwa maji ya chumvi katika mashimo ya kifusi hicho, jambo linalopelekea uharibifu mkubwa wa mazingira.

Je, kuendelea kuchimba kifusi na kuacha mazingira kama yalivyo sasa si kuwatia njaa wananchi wa vijiji vya Kibokoni, Kisiwani Udusini na Vumba, ambao hutegemea zaidi kilimo cha maweni (Makaani) kwa ajili ya kupata riziki zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 32 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, uchimbaji wa kifusi wa maeneo ya Makaani katika maeneo ya Vitongoji Jimbo la Wawi tunaendelea kwa kufuata utaratibu na maelekezo yote yanayotolewa na Idara ya Mazingira, na hadi muda huu hakuna eneo ambalo lililochimbwa hadi kufikia kiwango cha kuchimbuka maji ya chumvi katika maeneo hayo.

Aidha kwa msingi huo kuchimba kifusi katika maeneo hayo na maeneo mengine ya Micheweni, Kangagani, Mwambe na kadhalika hakuwezi kuwatia njaa wananchi wa vijiji hivyo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa katika eneo la Makaani kwenye kijiji cha Vitongoji Jimbo la Wawi kuna mashimo makubwa sana, ambayo yameshajaa maji ya chumvi yanayotoka baharini, ambayo si tu kama yanaathiri mazingira, lakini hata maisha ya watu na viumbe vyengine.

(a) Kwa kuwa Mhe. Waziri amekanusha, je, yuko tayari jioni ya leo mimi na yeye twende Makaani kwa ajili ya kuona hilo eneo pamoja na hayo mashimo; nauli Mhe. Naibu Waziri atatoa. *(Makofi)*

Nimepata taarifa kwamba kuna fedha ambazo hutumika kwa ajili ya kuhifadhi mazingira pale kampuni za ujenzi wa barabara zinapomaliza shughuli za ujenzi wa barabara, hivyo kampuni hizi huwa kuna *percentage* fulani huwa inatoa kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira.

(b) Je, suala hili ni kweli, na kama ni kweli fedha hizi anapewa nani.

(c) Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Chakechake inayo kamati yake ya mazingira na kuhifadhi mazingira. Je, kama fedha hizi hazipewi Halmashauri ya Wilaya ya Chakechake si kuidhalilisha Halmashauri ya Wilaya.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu: Mhe. Naibu Spika,

(a) Nipo tayari kufunga nae safari kwenda Pemba.

(b) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna utaratibu katika serikali kwa maeneo haya ambayo yanachimbwa, tunakuwa tuna utarariibu wa kushirikiana na taasisi za Mazingira ukiwemo mradi wa SMOLE, kwa kuwarejeshea maeneo yale kwa kujaza udongo na hatimaye kuwaruhusu wananchi kuotesha miti.

Mradi huu wa SMOLE ndio wanaokuwa na utaratibu wa kutusaidia fedha. Fedha zinazokuwepo msingi wake mkubwa ni kuhakikisha kwamba yale maeneo ambayo yamechimbwa vifusi kuyarejesha katika hali yake ya uoto wa asili. Kwa hiyo hakuna fedha zinazotoka moja kwa moja isipokuwa ni kwa kushirikiana na taasisi husika katika kurejesha fedha ili kuweza kuwapatia wananchi maeneo yale ambayo yamechimbwa kurejesha udongo na kuwapatia maeneo ili kuweza kuotesha miti kama ilivyokuwa asili.

(c) Kwa msingi huo kwamba hizi fedha haziwezi kwenda moja kwa moja katika Halmashauri, isipokuwa zinatumika fedha hizi kwa kushirikiana na wadau katika kutafuta *material* ili kurejesha maeneo yale katika hali yake ya asili.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Katika majibu yake Mhe. Waziri amesema kwamba maeneo ambayo yanachimbwa vile vifusi huwa wanashirikiana na wananchi kupanda miti. Mimi nilikuwa najua gharama zile ambazo zinafanywa. Kwa sababu makampuni kwa mfano Makampuni ya Barabara haya huwa yanachimba vifusi kule na kusababisha mashimo makubwa. Mhe. Saleh Nassor Juma, pia aliuliza lakini jawabu halikupatikana vizuri.

(a) Je, kuna gharama ambazo Kampuni zile zinatoa kwa ajili ya kwenda kuhifadhi mazingira katika maeneo ambayo walichimba vifusi.

(b) Kama kuna gharama zinatozwa mimi nilikuwa nataka kujua tu, katika miaka miwili hii ambayo kuna mikataba ambayo ilifanywa na Makampuni ya barabara ni kiasi gani ambazo zilitolewa na Makampuni hayo kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kwa maandishi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Waziri ulivyokuwa ukijibu swali hapa ulitaja sehemu ya Kiwani kwamba wamepigiwa marufuku kuchimba mashimo kwa ajili ya matofali. Ni kigezo gani mnachokitumia nyinyi kuchimba mashimo haya katika sehemu aliyosema Mhe. Saleh katika jimbo lake ya kuharibu mazingira, wakati serikali inaendelea kuchimba, wananchi wanazuiwa. Ni kipimo gani kilichotumika. Si madaraka mabaya mnayotumia Mhe. Naibu Waziri hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kwamba maeneo yote ambayo Wizara ya Miundombinu kwa kupitia Idara yetu ya UUB tumekuwa tukichimba kifusi ni maeneo ambayo tunayamiliki kihalali.

Lakini uchimbaji wetu wa kifusi hatuchimbi tu kwa utashi wetu, isipokuwa kwa kufuata maelekezo na taratibu ambazo tunapangiwa na wenzetu, hasa hasa na Idara ya Mazingira. Miongoni mwa maelekezo yao watu wa mazingira ni kuhakikisha kwamba maeneo yale ambayo tumechimba kifusi tunatafuta njia ya kuyarejesha katika hali yake ya kawaida.

Dhamira hii ya serikali ni kuona kwamba pamoja na kwamba tutakuwa tumechimba kifusi baada ya kuja kurejesha maeneo yale katika hali ya kawaida ile athari ya mazingira haitokuwepo. Lakini kilichokuwepo kwa upande wa wananchi wetu wanaochimba matofali likiwemo eneo hilo la Kiwani. Ni ukweli ambao upo wazi, maeneo yale baada ya kuchimba matofali wameacha *vacant* na inakuwa ni maeneo makubwa ambayo yameathirika sana kwa msingi wa kimazingira.

Nam. 56

Wanafunzi Kufutiwa Matokeo

Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Aliuliza:-

Hivi karibuni Baraza la Mitihani la Taifa (*NECTA*) lilichukua hatua ya kuwafutia matokeo wanafunzi 1,004 wa Zanzibar waliofanya mitihani ya Kidatu cha Nne *(O-level)* kwa madai ya kuvuja mitihani na makosa mengine. Mbali ya adhabu hiyo, *NECTA* pia ilitoa adhabu ya kutowaruhusu wanafunzi hao kufanya mitihani mingine au kurudia kwa miaka mitatu (3) ijayo.

(a) Je, Wizara imeridhika na sababu hizo zilizotolewa na *NECTA* kuwafutia mitihani wanafunzi hao.

(b) Wizara haioni adhabu ya kuwafungia kutorudia mitihani kwa miaka mitatu (3) kuwa ni adhabu kubwa mno na ambayo inawaondolea wanafunzi hao uwezekano wa kujirudi na kujipanga upya kwa maisha yao yajayo ambayo yanategemea mno elimu.

(c) Wizara inachukua hatua gani ili kuwaondolea adhabu hiyo ya ziada wanafunzi hao ili kuwawezesha kurudia mitihani na kupata fursa nyengine ya kujiendeleza kimasomo.

Mhe.Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake Nam. 56 lenye sehemu (a), (b) na (c). Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba katika Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne wa Mwaka 2011, Baraza la Mitihani la Tanzania lilifuta matokeo ya watahiniwa 3,033 kutoka skuli mbali mbali za Tanzania kutokana na kubainika kufanya udanganyifu katika mithani yao. Kati ya wanafunzi wote waliofutiwa matokeo yao wanafunzi 1,010 ni wa skuli 30 za hapa Zanzibar. Mbali ya adhabu hiyo, Baraza la Mitihani lilitoa adhabu ya kutoruhusu watahiniwa wote waliofanya mitihani na kufutiwa matokeo kutofanya mitihani mengine iliyoandaliwa na Baraza hilo kwa kipindi cha miaka mitatu.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Baraza la Mitihani limefuta matokeo ya mtihani huo kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za mitihani na Wizara imeridhika kwa kufutwa huko kwa kuzingatia Sheria na Kanuni ambazo zimewekwa.

b) Ni kweli kuwa adhabu ya kuwafungia watahiniwa waliofutiwa matokeo yao kutofanya mitihani mengine ya Baraza kwa kipindi cha miaka mitatu ni kubwa ukizingatia umri wa watahiniwa hao na baadhi yao wanaweza kupoteza ari ya kujiendeleza.

c) Baraza la Mitihani imezingatia kilio cha watahiniwa waliofutiwa matokeo yao na wazazi wao pamoja na ushauri uliotolewa na Wizara zote mbili na hatimae Baraza limepunguza adhabu hiyo na kuwaruhusu watahiniwa waliofutiwa matokeo yao kufanya tena mitihani baada ya Mwaka mmoja. Hivyo watahiniwa hao wataruhusika kurudia mitihani ya Kidato cha Nne, 2013. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika na namshukuru Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake fasaha.

Mhe. Naibu Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema wizara imeridhika na sababu zilizotolewa na Baraza la Mitihani katika kufuta mitihani hiyo. Ambayo kimsingi sababu hiyo ilikuwa ni kuridhika kwamba kumepita udanganyifu. Lakini hivi karibuni tu kumejitokeza ushahidi usio na mashaka kwamba Baraza la Mitihani

la Taifa limefanya makosa makubwa ambayo mpaka leo hayajulikani kwamba ni kwa makusudi au kwa bahati mbaya. Katika matokeo ya mtihani ya Dini ya Kiislamu kwa wanafunzi wa Kiislamu kiasi cha kutilia machaka uadilifu na uamini wa Baraza hili kwa baadhi ya wanafunzi.

(a) Je, haoni kwa wizara kukubali moja kwa moja kwamba sababu zilikuwa ni sahihi, ushahidi huu umepatikana hivi karibuni unatia dosari imani hii ambayo Wizara ijenga kwa Baraza hilo.

(b) Katika kushughulikia suala hili lilipojadiliwa hapa Barazani Wizara ilitakiwa na ikakubali kwamba itachukua hatua dhidi ya watu mbali mbali wengine ambao walihusika na udanganyifu ule mbali ya wanafunzi, wakiwemo wafanyakazi wa Wizara, walimu na wasimamizi wa mitihani. Je, hadi leo kumefanyika hatua gani katika utekelezaji wa ahadi ile ya waziri katika Baraza hili. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nimezungumza kwenye jibu mama kuwa

(a) Wizara iliridhika. Wizara haikuridhika tu moja kwa moja kama ambavyo tunafikiria. Wenzetu wa NECTA walikuja kwanza wakatueleza kabla ya matokeo yale kama kuna jambo ambalo limejitokeza. Na sisi kama wizara hatukujiridhisha kwa ajili tumeambiwa tu na NECTA tulitaka vielelezo vyote watuletee. Walituletea karibu maboksi sita. Tukaandaa Tume maalum ya wataalamu kutoka Wizara yetu ya Elimu akiwemo Kamishna wa Elimu bi Maryam akiwemo Profesa Rai na wenziwao. Wakavikalia vielelezo vile siku tatu na kutuhakikishia kwamba ni kweli udanganyifu ulifanyika. Kwa hivyo suala la udanganyifu lilikuwa halina tatizo. Sisi kama wizara tulijiridhisha kwamba watoto wetu ni kweli wamefanya udanganyifu huo.

(b) Hatua ambazo tumezichukua, juzi katika swali Nam. 7 la terehe 18 nilijibu ni hatua gani ambazo tumezichukua. Kwa faida ya Mhe. Ismail Jussa na Baraza lako tukufu, nitazungumza tena.
    - Kuwaandikia wahusika wote wakiwemo wasimamizi wetu ambao walisimamia mitihani ile kujieleza na tayari Wizara yangu imepokea barua kutoka kwa wasimamizi na baada ya muda si mrefu tutakaa kikao na kuona hatua gani ambazo tutazichukua kwa kila aliyehusika. Kila mmoja atabeba msalaba wake kwa mujibu alivyohusika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii. Kwanza napenda nimuulize Mhe. Naibu Waziri suala la nyongeza lenye kifungu (a) na (b)

(a) Ni asilimia ngapi ya wanafunzi wote waliofanya mitihani ambao walifutiwa mitihani yao ukilinganisha na wanafunzi wote waliofanya mtinahi katika kipindi hicho cha mwaka huo.

(b) Ikiwa asilimia hiyo ni kubwa inayoweza kuzingatiwa. Je, haoni kwamba kuna matatizo ndani ya uendeshaji wa elimu yetu ambayo imejitokeza kwa kufeli wanafunzi au kukopia wanafunzi. Badala ya kushughulikia wale ambao wamevujisha tu hatuitizami *system* ya elimu yetu tukaona tulipofikia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, wanafunzi wote ambao walifanya mitihani ni 13,545 wote kwa jumla. Kwa Zanzibar ambao walifutiwa mitihani ni 1,010. Kwa hivyo namuomba Mwalim Rashid Seif Suleiman aziweke kiasilimia kwa sababu inaweza kunichukua muda kwani sikuwa mtaalamu wa hesabu atapata asilimia.

Lakini labda inawezekana haya ambayo yametokea ya watoto kufeli labda ni *system* ambayo tunakwenda nayo ya elimu inawezekana sana. Kama hivyo ambavyo ulivyoliuliza wewe ulivyoliona na sisi Wizara tumeliona na tumeanza utaratibu. Tumeanza utaratibu kwa kukaa na kujipima na kutathmini. Tumeanza utaratibu wa kupitia maskuli yetu mmoja baada ya mwengine na kuona ambacho kinafanyika katika maskuli.

Mheshimiwa ni kweli kama ulivyosema na baada ya muda tutajua tatizo ni nini na tutalirekebisha vipi kuhakikisha kama wanafunzi wetu wanapata elimu iliyobora.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana yenye kigugumizi ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri hivi karibuni kumetokea Kamati ya Wazee wa watoto ambao wamefutiwa matokeo yao, na kutoa *notice* kwa serikali pamoja na Baraza la Mitihani la Taifa kuyapeleka Mahakamani.

Je, wizara yako imechukua hatua gani ya kuwaita wazee hawa ili kutatua mgogoro huu nje ya Mahakama.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kadhia hii ilipotokea kulikuwa na makundi mbali mbali ya wazee ambao waliji-*organise* na kuja Wizarani kwetu. Kwa hawa ambao waliokuja tulikaa nao, tukazungumza nao na tukawasaidia binafsi mpaka nauli kwa baadhi ya Wajumbe kwenda *NECTA* kujiridhisha. Na wao ripoti wakatuletea na waliyoyakuta, kasoro ambazo walizoziona na yale ambayo walikubaliana na sisi.

Sasa hawa ambao wamejitokeza kwenda Mahakamani sisi hatuna taarifa nao. Kwa sababu kama Wizara hawajaja wakatueleza kama tunataka kwenda Mahakamani.

Nam. 72

Msongamano wa Wagonjwa Kituo cha Mwera

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kituo cha Afya cha Mwera, kinakabiliwa na ufinyu wa jengo wakati kinatoa huduma katika Shehia za Ubago, Koani, Kidimni, Mwera Mtofaani na Kianga. Jambo ambalo linasababisha msongamano mkubwa wa wagonjwa.

(a) Je, Wizara ya Afya ina mpango gani wa kukitanua kituo hicho ikiwemo Kujenga jengo jipya.

(b) Kwa kuwa wananchi wamekuwa wakipata huduma katika mazingira ya msongamano wakiwemo mama wajawazito na watoto. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mahema ya muda na kuweka mabenchi ya kupumzika wagonjwa ili kuondoa msongamano huo.

(c) Kwa kuwa kituo hicho kinapokea idadi kubwa ya wagonjwa kwa siku, Wizara ina mpango gani wa kupeleka wafanyakazi wa ziada ili kuondoa tatizo la kusubiri huduma kwa muda mrefu.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Baraza lako tukufu swali lake Nam. 72 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwa idadi ya watu wanaopata huduma katika kituo hicho imeongezeka mara dufu. Kutokana na wingi wa wakaazi wa Mwera na Vijiji jirani ambavyo vinapata huduma katika kituo cha Afya cha Mwera. Wizara ya Afya imelazimika kukipandisha daraja.

Hivi sasa wizara yangu kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) ina mpango wa kukifanyia utanuzi na ukarabati mkubwa kituo hicho ambapo kitatoa huduma za ziada pamoja na kuongeza wafanyakazi wa kutosha na wenye sifa.

Kwa kutambua hilo bodi ya Afya ya Kituo cha Mwera imeshajenga jengo Pembeni mwa kituo kwa ajili ya utawala, *pharmacy* na ofisi ya bodi. Kukamilika kwa Kituo cha Afya Mwera Pongwe na pia utakapokamilika ujenzi wa kituo cha Afya cha Kinuni, idadi kubwa ya wananchi itapungua kwa kupata huduma katika vituo hivyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa kukiri kwamba ipo haja ya kukitanua kile kituo. Tumekuwa tukizowea kwa kusikia majibu kwa Mhe. Naibu Waziri kuwa huduma zisifike kilomita tano. Kile kituo hivi sasa kamati baada ya kutembelea ipo haja ya kujengwa, nataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri.

(a) Ujenzi huo utaanza lini na utagharimu kiasi gani na utamalizika lini.

(b) Kituo kile kina kilio cha madaktari, daktari aliyekuwepo ni mmoja au wawili mpaka muda huu. Ni lini atachukua jitihada hizo kuwasaidia wananchi wale.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, vituo hivyo ambavyo nilivyovitaja vitapunguza huo umbali anaousema Mhe. Mwakilishi. Kwa sababu Mwera hiyo hiyo kutakuwa na kituo chengine ambacho juzi juzi tu kimewekewa jiwe la msingi na kipo karibu kumalizika au bado imebakia nyumba tu ya wafanyakazi. Lakini vifaa vimeshatiwa na kitafunguliwa karibuni.

Kituo cha Kinuni nacho kitamalizwa na Serikali pia katika mwaka pengine ujao wa fedha. Kwa hiyo kitafanya kituo hicho hakitokuwa kilomita tano (5) zaidi ya kituo chengine, kitakuwa ni chini ya kilimita tano zaidi ya kingine kwa utaratibu wa Wizara ya Afya hapo bado tumekuwa tupo nje ya lile lengo ambalokuwa tumekusudia. Lakini kulingana na Wingi wa Watu uliokuwepo Pale tumekubaliana na vituo hivyo viwili viwepo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu daktari aliyekuwepo pale alikuwa ni daktari wa mkataba na muda wake wa mkataba umekwisha kwa hivyo hakuweza kuongezewa mkataba mwengine.

Wizara ya Afya ina Chuo cha Afya kimoja ambacho kinatoa madaktari wasaidizi ambao wanatakiwa kuwepo vituoni. Kwa mwaka huu hatukutoa daktari pale, tumepata manesi tu. Kwa hivyo tutakapotoa madaktari pale tunajua kwamba pale pana upungufu wa daktari. Tutakapopata daktari tutampeleka, lakini katika vituo ambavyo vina wafanyakazi wengi kuliko vituo vingi vya hapa Zanzibar, kimojawapo kile kina wafanyakazi wengi ingawa wanazidiwa nguvu na wagonjwa.

Nam. 102

Unyanyasaji wa Kijinsia Kisiwani Pemba

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko la unyanyasaji wa kijinsia hususan kwa watoto wadogo wakiume, ambapo suala hili limeenea sana Kisiwani Pemba.

Je, Mhe. Waziri ni juhudi zipi zinazofanywa ili kuwakinga watoto kuepukana na kadhia hii.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto – Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake Nam. 102 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli vipo vitendo vya unyanyasaji hususan kwa watoto wadogo wakiume. Lakini ukubwa wa tatizo hilo linahitaji kufanyiwa utafiti wa kina ili kujua hali ya ukubwa wa tatizo lenyewe. Wizara imeandaa utafiti wa kina wa tatizo hilo kwa nchi nzima. Aidha kazi ya kuelimisha wazazi na walezi na watoto juu ya athari ya jambo hilo zinaendelea kufanywa na Wizara kwa kushirikiana na wadau mbali mbali kupitia mikutano redio, televishen na magazeti.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa ruhusa kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa suala hili linawaathiri sana watoto wetu na pia hata sisi wazazi.

(a) Je, Mhe. Waziri kuna hatua zipi ambazo zitachukuliwa kwa wale ambao watabainika na vitendo kama hivi.

(b) Wangapi waliochukuliwa hatua za kisheria ambao wamebainika na suala kama hili. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto:

(a) Mhe. Naibu Spika, najua kwamba suala hili la unyanyasaji la watoto hasa wakiume si jambo zuri hata kidogo.

(b) Mhe. Naibu Spika, hatua tutakazozichukua nadhani baada ya kulifanyia jambo hili utafiti wa kina tukaona likoje. Kesi nyingi zinazokuja Wizarani ni kuhusu ubakaji wa watoto wanawake. Lakini suala hili la watoto wa kiume bado hatujalipata. Baada ya utafiti na kuona kuna haja gani ya kuchukua hatua ili tuwakomeshe hawa hilo litafanyika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, katika swali mama kuna unyanyasaji wa kijinsia wa aina mbili. Aina moja ni hii ya jinsia moja ambayo ni mbaya sana. Mhe. Waziri kakiri kuwa suala hili lipo na swali mama lililokuwemo katika karatasi imeelezwa kuwa suala hili limeenea sana kisiwani Pemba, lakini kwangu mimi ni jipya.

(a) Ningeliomba nijibiwe ni Wilaya gani katika Wilaya nne za Pemba inaongoza kwa matatizo haya.

(b) Ni watu wangapi angalau wemeshajulikana. Kwa sababu Mheshimiwa kasema kwamba kesi hajaipata lakini kasema jambo hilo lipo. Sasa hao waliojulikana angalau ni wangapi.

(c) Kwa sababu ni suala lililopingwa kabisa kidini kuna mpango gani hasa wa kuandaa mkakati maalum kuona kuwa vijana wetu hawapotei katika hali hii mbaya. Huu ni mtindo mbaya sana wa luti ambao walifika kuangamizwa. Kwa uzito wa suala hili tusiwaachie vijana wetu wakaingia katika suala hili kama lipo kweli.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwanza ni Wilaya gani hasa inayohusika na mambo haya kusema kweli bado sijaelewa mimi, sina haja ya kuficha, inawezekana sehemu za Mijini ndio zaidi wana matatizo hayo kuliko vijijini. Kwa hivyo tutakapofanya utafiti wa jambo hili ndio tutaelewa hasa ni wilaya gani inayohusika na mambo hayo. Tutajitahidi kuwaelimisha wenzetu kwamba mambo haya si mambo mazuri, wanawaacha watoto wanawake wanakwenda kwa watoto wakiume. Jamani tujitahidini sana juu ya jambo hili. Kuna uhai na umauti kesho mbele ya Mungu tutasema nini sisi.

Mhe. Mussa Ali Hassan: …. huko kisiwani Pemba na kwa vile Serikali ilikawia kuchukua hatua na hivi sasa vijana wale walikuwa wadogo wameshakuwa wakubwa na wanakimbilia Unguja. Je, Serikali inachukua hatua gani ya kuzuia kutoka Pemba ili kuja Unguja.

Pili na hivi sasa inasemekana wameshaingia sana hapa Unguja mchezo huo unaendelea nao si mzuri na wamehamia Kinuni na Mtopepo. Kuna hatua gani Serikali itachukua ya kuwarejesha Pemba.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Serikali haikukawia kuchukua hatua kwa watu wanaowabaka au wanaowadhalilisha watoto wa kiume, maana suala hili mimi kusema kweli thawabu nilikuwa sijalipata. Lakini nimelipata tu kijuu juu kwa sababu hakuna kesi maalum iliyoripotiwa kwetu, lakini nasema tena kwamba suala hili tutalifanyia utafiti na tukilipata uzuri tutalichukulia hatua.

Nam. 142

Ujenzi wa *Football academy* katika kukuza michezo

Mhe. Nassor Salim Ali: Aliuliza:-

Katika kuinua mchezo wa mpira wa miguu kunahitajika kukuza na kuendeleza vipaji vya vijana wa umri mdogo kuanzia miaka kumi hadi kumi na sita. Mfumo bora unaotumiwa na nchi nyingi duniani katika kukuza mchezo huu ni kuanzishwa kwa *Football Academies.*

Mhe. Waziri Je, zipo *Football Academies* ngapi hapa Zanzibar, na kama hazipo Wizara ina mpango gani wa kujenga *Football Academies* hizo kwa kila Wilaya.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, katika kuinua mchezo wa mpira wa miguu ni kweli kunahitaji kukuza na kuendeleza vipaji vya vijana wa umri mdogo kuanzia miaka 10 hadi 16. Na ni kweli nchi nyingi duniani hutumia mfumo kwa kuanzisha *Football Academies* katika kufikia lengo hili.

Mhe. Naibu Spika, kwa hapa Zanzibar hadi sasa kipo kituo kimoja kilichosajiliwa rasmi ambacho ni *Dole Academy* kilichoko Dole Wilaya ya Magharibi Unguja, ambacho kwa sasa kina vijana zaidi ya 40 wanaopata mafunzo ya mchezo wa mpira wa miguu.

Mhe. Naibu Spika, mbali na kukuza vipaji vyao vijana hawa wanapata fursa ya kushiriki mashindano nje ya nchi pamoja na kuipa heshima nchi yetu. Katika mwezi wa tano mwaka huu vijana hawa wameshiriki mashindano ya vijana ya Afrika Mashariki na kufanikiwa kupata nafasi ya kwanza.

Mhe. Naibu Spika, aidha zipo *Football Academies* nyengine ambazo jitihada za Wizara ya Habari, Utamaduni Utalii na Michezo, kupitia Kamisheni ya Utamaduni na Michezo inaendelea ili ziweze kuwa rasmi na ziweze kutambulika kisheria, pamoja na jitihada za kupanua wigo, na kuwezesha kuwepo vituo hivyo katika Wilaya.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana naomba kuuliza swali moja lenye vifungu (a) na (b).
Mhe. Naibu Spika, katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba ni kituo kimoja ambacho kimesajiliwa mpaka hivi sasa je, Wizara ina mikakati gani kuhakikisha kwamba vinasajiliwa vituo vyengine ili kuweza kuendeleza mpira wetu huu wa miguu.

Pili katika kisiwa cha Pemba hakuna hata kituo kimoja cha *Football Academy*. Wizara itashajiisha vipi kuwa na kituo cha Football Academy.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, Wizara yangu ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo itashirikiana na wadau mbali mbali pamoja na BTMZ pamoja na ZFA ili kuviendeleza vituo huko Pemba.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye (a) na (b),
(a) Kwa kuwa mpira wa miguu ni sehemu muhimu kwa vijana, na vijana wetu tunataka wawe na uzoefu na mazoezi mazuri katika kiwiliwili chao. Je Wizara ina mpango gani wa kuweka kila Wilaya kituo hiki ili vijana wetu wasiende kupigana mateke lakini waende kucheza mpira.

(b) Uwanja ule wa Gombani ulipojengwa tuliambiwa una ramani kubwa ikiwa kimoja wapo ni hicho kituo cha *football academy*, lakini mpaka hivi leo hakuna lolote lililofanywa baada ya hicho kiwanja, je ndio kibakie pale pale au mpaka kivamiwe na wananchi kujengwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika swali mama nimeeleza kuwa kutajengwa vituo kila Wilaya vya *academy*. Sasa Mhe. Mwakilishi hii ni mipango ya Wizara pamoja na wadau mbali mbali kama nilivyojibu kwa kushirikiana na wao na kuweza kushughulikia viwanja hivi vya *academy*.

Swali lake la pili kuhusu kiwanja cha Gombani Pemba, ni kweli eneo lipo na limeshatengwa na Wizara kwa ajili hiyo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nikushukuru Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, ambayo ninamshukuru kwa ufafanuzi wake naomba nieleze kwamba, ni kweli ipo haja ya kila Wilaya katika nchi yetu kuanzisha hizi sio *football academies* tu lakini *sports academies* ambazo zitashughulikia mafunzo mbali mbali ya michezo katika nchi yetu. Wizara ina lengo hilo lakini tunapaswa kupata mashirikiano makubwa kutoka kwa viongozi wa Wilaya yenyewe. Kwa hivyo Waheshimiwa Wawakilishi wawe na mipango ambayo itakwenda sambamba na azma ya Wizara katika kufanya kazi hiyo.

Na suala la Kiwanja cha Gombani, ni kweli kwamba ramani ya mwanzo ya kiwanja cha Gombani kilipimwa suala la *football academy*, na tunashukuru kwamba bado kiwanja cha Gombani hakijavamiwa sana, Wizara inajitahidi wakati wote kuona kwamba mipaka ya kiwanja cha Gombani bado inasimamiwa na kuhifadhiwa na Wizara, na kwamba jitihada inafanywa kwa kupitia mipango ya Wizara na kupitia wafadhili wengine ili tuanze kujenga majengo mbali mbali. Hivi sasa tunaanza na uwezekano wa kujenga Hoteli ya kiwanja pale katika uwanja wa gombani tunazungumza na mfadhili lakini hatimaye mambo mengine ambayo yamo katika ramani yatashughulikiwa.

Nam. 81

Upatikanaji wa Maji Safi na Salama Ndijani

Mhe. Mtumwa Kheri Mbarouk: Aliuliza:

Pamoja na jitihada kubwa iliyochukuliwa kwa kijiji cha Ndijani kwa kupatiwa maji safi na salama likiwepo tangi zuri, kubwa na visima vinne. Lakini kwa muda mrefu sasa wananchi wa kijiji hicho wamekosa maji safi na salama.

(a) Je, ni sababu zipi zilizopelekea wananchi wa kijiji hicho kukosa maji safi na salama.

(b) Ni lini hasa wananchi hawa wataondokana na tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi na Nishati:

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo:

Kwanza nakiri na naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba mradi wa maji wa Ndijani tumejenga tangi kubwa, zuri na la kisasa lakini tangi hilo halipati maji kama vile ambavyo ilikuwa inatarajiwa. Sababu zinazopelekea kukosekana kwa maji kwenye tangi hilo inatarajiwa kuchimba kisima chengine kipya kuliondoa tatizo hilo au kulimaliza kabisa.

Mhe. Mtumwa Kheri Mbarouk: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba niulize swali la nyongeza. Mbali ya sababu Mhe. Waziri alizozitaja kwa kuwa ulipomalizika tu mradi wa kijiji hicho wananchi walijenga matumaini makubwa kwa kupata maji mazuri na salama, na kutokana na kuwepo kwa mashine nzuri wakati ule ilipowekwa mashine ile, lakini baadae mashine ile ilichukuliwa na kupelekwa Muyuni ili kwenda kufanyiwa majaribio, na mashine ile haikurejeshwa tena, ndicho chanzo cha kukosa maji wananchi wa Ndijani.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kufanya hivyo ni kuwafanya wananchi kukosa imani na Serikali yao.

(b) Mhe. Waziri kufeli kwa miradi mikubwa kama hiyo je Serikali haioni aibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kuondolewa kwa pampu sio sababu iliyosababisha wananchi hao kukosa maji au kupandisha maji kwenye tangi hilo. Sababu ambayo inasababisha ni ukaukaji wa visima. Visima vilivyochimbwa ni visima vinne. Visima hivyo wakati wa kipindi cha mvua, basi maji huwa yanapatikana vizuri sana, lakini unapofikia tu wakati wa kiangazi, niseme kwamba Serikali haitarajii pale ambapo inapopeleka mradi yakitokea matatizo kama hayo kwamba Serikali kuingia aibu *no,* ni kwamba Serikali inapeleka miradi katika sehemu hizo kwa nia nzuri, kwa malengo mazuri, kwa matarajio ya kuwanufaisha wananchi inaowaongoza.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Katika eneo la Makadara ni eneo la mwanzo lililowekwa mita kwa ajili ya majaribio, na wakati zilipowekwa mita zile walikuwa wananchi wanalipishwa shilingi elfu mbili kwa mwezi. Lakini sasa Mhe. Naibu Spika, inalipwa shilingi 15,000/- , 20,000/- kwa mwezi.

a) Ni sababu zipi zilizofanya wananchi kutoleshwa pesa hizo.

a) Zinapoharibika mita zile wananchi hulipishwa 50,000/-. Je, hili ni kweli na kama ni kweli ni sababu gani walipishwe shilingi elfu 50,000/-.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa hapa utafute utaratibu swali mama linahusu visima Ndijani hamna masuala ya mita tafuta utaratibu uulize.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri katika majibu yale ya msingi amesema kwamba visima vya Ndijani wakati wa kiangazi vinakauka maji, na wakati wa mvua maji yanakuwepo kwa wingi.

(a) Je, ni utafiti gani uliofanywa wa kitaalamu mpaka ikagundulikana visima hivi vikakauka maji.
(b) Kuna utaratibu gani wa kuchimba visima vipya ili watu wa Ndijani kufaidika na maji haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi na Nishati: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:
Utafiti tulioufanya na kugundua kwamba visima hivyo vimekauka, Mamlaka ya Maji imefanya uchunguzi wa kutosha na ikalielewa hilo. Isitoshe tatizo linalopelekea zaidi kwa ukaukaji wa visima katika maeneo hayo ni uharibifu wa mazingira, hususan kukata miti katika vyanzo vya maji.
Swali la pili Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji itachimba kisima chengine muda mdogo tu ujao kwa kushirikiana na Mwakilishi wa Jimbo hilo Mhe. Issa Haji Gavu. Katika kipindi cha mwezi ujao tunategemea kuchimba visima katika eneo jengine ambalo litaunganisha kwenye mtandao unaoelekea kwenye tangi hilo, na tunategemea wananchi wa maeneo hayo watapata huduma hiyo ya maji safi na salama haraka iwezekanavyo.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 - Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa Hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili lipokee, lijadili na hatimae liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya njema na uzima wakati huu tukiwa pamoja katika kikao hiki cha pili cha Bajeti, tangu kuanza kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuongoza nchi yetu kwa uadilifu mkubwa, hekima na upendo. Chini ya uongozi makini wa Dk. Ali Mohamed Shein nchi yetu imeendelea kupata mafanikio makubwa katika nyanja zote, kiuchumi, kijamii na kisiasa. Pia nampongeza Makamo wa Kwanza wa Rais, Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad na Makamo wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa namna wanavyomsaidia vyema Mheshimiwa Rais katika kuiongoza nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Spika, Pandu Ameir Kificho pamoja na wewe Mhe. Naibu Spika, kwa busara zenu za kuliongoza Baraza letu Tukufu kwa ufanisi mkubwa. Nawapongeza Wenyeviti wetu, Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, Mwakilishi wa Viti Maalum na Mheshimiwa Mahmoud Mohamed Mussa, Mwakilishi wa jimbo la Kikwajuni kwa namna wanavyosaidia kuliendesha Baraza letu la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru Wenyeviti na Wajumbe wote wa Kamati za Kudumu za Baraza lako Tukufu kwa ushauri na maelekezo yao. Aidha, shukrani maalum ziende kwa Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa kwa michango yao waliotoa wakati wa kupitia Makadiro ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yetu kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Nawapongeza Wajumbe wote wa Baraza hili Tukufu kwa michango yao mbalimbali ambayo ina lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji wa Serikali na kuiletea maendeleo nchi yetu. Nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa utendaji wao mzuri na kujibu hoja za Wajumbe kwa umakini mkubwa na usahihi. Pia nawapongeza Watendaji wote wa Serikali na wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi kubwa wanazoendelea kuzifanya katika utekelezaji wa majukumu yao. Kwa ujumla Serikali inajivunia sana kuongezeka kwa ufanisi katika utendaji wa Serikali na Baraza, jambo ambalo linachangia katika maendeleo yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia kutumia nafasi hii kumpongeza Ndugu Yahya Khamis Hamad kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Baraza hili, na namtakia mafanikio katika kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Naibu Spika, Baraza lako Tukufu limepoteza Wajumbe wake wawili, ambao ni Marehemu Mussa Khamis Silima aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Uzini na Mbunge wa kuchaguliwa kutoka Baraza la Wawakilishi, na Marehemu Salum Amour Mtondoo, aliyekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Bububu. Wenzetu hawa tutawakumbuka kwa uchapaji kazi wao bora. Namuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahala pema peponi amin.

HALI YA SIASA

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla hali ya kisiasa hapa nchini inaendelea vizuri sana. Viongozi wa Vyama vya Siasa na Wananchi wamesahau tofauti zilizopelekea chuki na uhasama huko nyuma, na kuendelea kushirikiana katika kudumisha amani, utulivu na mshikamano na kuiletea maendeleo nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mnamo tarehe 12/02/2012 Tume ya Uchaguzi Zanzibar iliendesha Uchaguzi mdogo kwa jimbo la Uzini. Katika uchaguzi huo Mheshimiwa Mohamed Raza Dharamsi aliyegombea jimbo hilo kwa tiketi ya CCM aliibuka mshindi. Nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Raza, na namtakia mafanikio katika kuwahudumia wananchi wa Jimbo la Uzini na nchi yetu kwa ujumla. Aidha, Tume ya Uchaguzi Zanzibar hivi sasa imo katika hatua za maandalizi ya kuendesha Uchaguzi mdogo wa Jimbo la Bububu, uchaguzi ambao umepangwa kufanyika tarehe 16/09/2012. Naomba kuchukua fursa hii kuwaomba viongozi wa Vyama vya Siasa na Wananchi kuendeleza umoja wetu kwa kuendesha Kampeni kwa ustaarabu na kufanya uchaguzi kwa salama na amani wakati utakapofika.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na hali nzuri ya kisiasa tuliyonayo katika nchi yetu, hivi karibuni kumejitokeza kikundi cha watu wachache ambao wamejitokeza na hoja ya kupinga Muungano na kutaka kuitishwa kwa kura ya maoni. Kikundi hiki kinachojulikana kwa jina la UAMSHO na washirika wake, kimekuwa kikiendesha mikutano, mihadhara, maandamano bila ya kupata vibali kutoka katika Taasisi husika. Hii inaonesha wazi kwamba hawako tayari kufuata sheria za nchi ziliopo.

Mhe. Naibu Spika, Serikali imesikitishwa sana na vitendo vya vurugu vilivyosababishwa na Jumuia hii ya UAMSHO na washirika wake. Vurugu hizo zilizotokea usiku wa tarehe 26/05/2012 na kuendelea hadi tarehe 28/05/2012 zilisababisha uharibifu mkubwa wa mali za Serikali, nyumba za ibada, na mali za watu binafsi. Aidha, vurugu hizo zilileta usumbufu mkubwa kwa wananchi, na kuwajenga hofu juu ya usalama wao na mali zao na kutishia hali ya utulivu, amani na umoja katika nchi yetu. Serikali inaendelea kuwaasa wale wote wanaojishirikisha na vitendo vya uvunjifu wa sheria, kuacha vitendo hivyo mara moja kwani vinarudisha nchi yetu katika hali za chuki na mifarakano. Serikali inawataka Wazazi kuwaasa vijana wao kutoshabikia vitendo vya vurugu, kwani madhara ya vitendo hivyo ni makubwa kwao, familia zao na jamii nzima ya Wazanzibari na Watanzania kwa jumla.

MUUNGANO

Mhe. Naibu Spika, Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar hivi sasa umetimiza miaka 48 tangu kuanzishwa kwake. Kupitia Muungano huu yapo maeneo mengi ambayo nchi yetu imepata maendeleo. Maendeleo haya ni pamoja kuwapatia wananchi wetu fursa za kuishi kwa amani na kufanya shughuli zao za kiuchumi kwa uhuru bila ya vikwazo katika maeneo yote ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na mafanikio haya, Muungano wetu unakabiliwa na changamoto mbali mbali na Serikali zetu mbili zinaendelea kushirikiana katika kuondosha changamoto hizo. Vikao vya Makatibu Wakuu na Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vinaendelea kufanyika, ili kujadili masuala mbalimbali ambayo yanaleta kero kwa wananchi katika Muungano wetu. Aidha, Kamati ya Pamoja ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar chini ya Mwenyekiti wake Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kukutana na kujadili juu ya namna bora ya kuondosha kero hizi.

Mhe. Naibu Spika, kuanzisha mchakato wa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja ya hatua muhimu zinazochukuliwa na Serikali zetu mbili katika kuondosha matatizo na kero za Muungano wetu, ili kujenga Muungano imara wenye kukidhi matakwa ya wananchi wetu na kuhakikisha maslahi ya kila upande wa Muungano wetu yanalindwa. Naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kushauriana vyema na hatimae kupelekea kuundwa kwa Tume madhubuti ya Taifa ya Kuratibu Maoni na Mapendekezo ya Wananchi kuhusu Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tume hiyo ina Wajumbe sawa kutoka pande mbili za Muungano (Wajumbe 15 kutoka Zanzibar na Wajumbe 15 kutoka Tanzania Bara). Wajumbe hawa 30 wameteuliwa kutoka taasisi mbalimbali nchini, zikiwemo Taasisi za Serikali, Vyama vya Siasa, Jumuia za Kiraia na Waandishi wa Habari. Kuteuliwa kwa Tume hii madhubuti yenye wajumbe makini inakidhi haja na matarajio ya wananchi wetu ya kutoa maoni yao, ili kuwa na Katiba Bora yenye maslahi yao, vizazi vyao na Taifa kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii kuwataka wananchi wote kujitokeza kwa wingi kutoa maoni yao kwa uhuru na bila ya woga wakati utakapowadia. Aidha, nawaomba viongozi wote kuwaelimisha wananchi juu ya utaratibu mzima wa kutoa maoni kwa kuzingatia Sheria Namba 8 ya mwaka 2011 kama ilivyorekebishwa, na Sheria Namba 2 ya mwaka 2012 ya Mabadiliko ya Katiba. Hii ni fursa ya pekee tuliyoipata wananchi wote wa Tanzania tokea kuasisiwa kwa Taifa letu, hivyo ni vyema tukaitumia fursa hii vizuri kwa faida yetu na Taifa letu na ndio njia pekee ya kisheria ya kutoa maoni tunayoyataka kwa mustakbali wa nchi yetu bila kugombana, bila ya kuchukiana na bila ya kuhatarisha amani ya nchi yetu.

HALI YA UCHUMI NA MIPANGO YA SERIKALI YA KUIMARISHA UCHUMI

Mhe. Naibu Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wakati wa kuwasilisha hotuba yake ya Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013 katika Baraza lako Tukufu, uchumi wa Zanzibar umekua vizuri katika mwaka 2011. Pato halisi la Taifa limekuwa kwa asilimia 6.8 na kufikia Sh. 1,198 bilioni (mwaka 2011) kutoka Shs. 946.8 bilioni kwa mwaka 2010. Kasi hiyo ya ukuaji wa asilimia 6.8 ni ya juu zaidi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Miongoni mwa sababu zilizochangia kasi hii nzuri ya ukuaji wa uchumi wetu ni kuimarika kwa sekta ya huduma kulikochangiwa zaidi na kuongezeka kwa uzalishaji na bei nzuri ya zao la karafuu katika soko la dunia, pamoja na kuongezeka uwekezaji rasilimali na kuimarika kwa sekta ya viwanda, yote haya yamewezekana kutokana na hali ya umoja amani na utulivu katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Katika juhudi za kuimarisha zaidi uchumi wa nchi yetu, Serikali itaendelea na juhudi zake za kutekeleza mipango yake ya maendeleo. Juhudi na mipango hiyo ni pamoja na kuimarisha zao la karafuu, kuendeleza kilimo hasa kilimo cha umwagiliaji maji ili kukuza uzalishaji wa ndani, kukuza zao la mwani, kuimarisha shughuli za utalii, kujenga mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji, na kuongeza kasi katika kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuimarisha mifuko ya uzalishaji na kuimarisha vikundi vya Kuweka na Kukopa (SACCOS) viliopo, na kuanzisha Benki za Maendeleo ya kisekta hii ni kuongeza ajira, kipato cha wananchi mmoja mmoja na kuimarisha harakati za uchumi katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, vilevile Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya uvuvi kwa kuwaendeleza wavuvi wadogo wadogo, kuhamasisha ufugaji wa samaki wa kisasa na uvuvi endelevu. Mkazo zaidi utawekwa katika kuwavutia wawekezaji wa ndani na kutoka nje ya nchi kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu. Aidha, Serikali itaimarisha sekta ya mifugo kwa kuendelea kutoa elimu ya ufugaji wa kisasa kwa jamii, kufanya utafiti wa malisho ya mifugo na kuendeleza kazi za upatikanaji wa mbegu bora za mifugo.

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaendeleza mikakati yake ya kupanua wigo wa utalii na kuutangaza kwani ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Kupitia uwekezaji wa Sekta Binafsi nchi yetu ina fursa kubwa ya kuongeza Pato la Taifa na ajira kwa vijana. Kwa kuelewa mahusiano hayo ya kiuchumi, Serikali itaendelea na juhudi zake za kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha Sekta Binafsi kuwekeza

kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ya kiuchumi na utoaji wa huduma. Aidha, Serikali itaendelea kujenga misingi imara ya kukuza ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (Public-Private Partnership), na hatua zitachukuliwa kujenga uwezo wa Wazanzibari kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi nchini.
Mhe. Naibu Spika, katika kuweka mazingira mazuri ya kukuza fursa ya uwekezaji, Serikali kwa kushirikiana na Wahisani mbali mbali itaimarisha miundombinu ya umeme, barabara na bandari ikiwemo ujenzi wa njia ya pili ya umeme kutoka Ubungo Dar es salaam hadi Mtoni Unguja, kuimarisha njia za kusambaza umeme na ujenzi wa vituo vipya vya umeme hapa Unguja, kuendeleza ujenzi wa jengo jipya la abiria katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amaan Karume, uwekaji wa taa katika barabara ya kurukia na kutulia ndege katika Kiwanja cha ndege Pemba na ujenzi wa barabara mbali mbali za mijini na vijijini. Aidha, Serikali itaendelea na juhudi zake za kutafuta fedha kwa ajli ya ujenzi wa Bandari mpya ya Mpigaduri.

UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI NA KUONGEZA FURSA ZA AJIRA

Mhe. Naibu Spika, Serikali inaendelea kuwawezesha Wananchi kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kuongeza ajira kupitia utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo. Kwa kushirikiana na Benki ya Watu wa Zanzibar, Mfuko wa JK/AK hadi kufikia mwezi wa Machi, 2012 umeweza kutoa mikopo kwa Wananchi wapatao 750 yenye thamani ya jumla ya Shs 1,529,884,000. Aidha, mikopo mengine imeweza kutolewa kupitia Mifuko mengine na asasi mbalimbali za kifedha. Kupitia Sekta ya Ushirika, wananchi wanaendelea kuwezeshwa kwa kupatiwa mafunzo ya vitendo.

Mhe. Naibu Spika, katika juhudi za kusaidia vijana kujiajiri wenyewe, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) inatekeleza program ya ***Kazi nje nje***. Lengo la program hii ni kukuza fursa kwa vijana kuweza kujiajiri wenyewe na kuachana na tabia ya kusubiri ajira kutoka Serikalini. Kupitia program hii vijana hupatiwa mafunzo ya ukufunzi wa ujasiriamali na kujengwa mwamko wa kujiajiri.

SEKTA YA HUDUMA ZA JAMII

Mhe. Naibu Spika, katika kuimarisha huduma za jamii, Serikali inaendelea na juhudi zake za kuwapatia elimu bora vijana wa nchi hii na kuimarisha huduma za afya kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya 2020 (*Zanzibar Development Vision 2020*), na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (*MKUZA II*). Miongoni mwa mambo yanayotekelezwa ni pamoja na kuwapatia wanafunzi wote wa Sekondari vitabu vya kusomea kwa masomo yote, vifaa vya maabara na ukarabati wa majengo na ujenzi wa skuli mpya katika maeneo mbalimbali. Kwa upande wa sekta ya afya, Serikali katika mwaka wa fedha 2012/2013 inakusudia kuweka mfumo utakaoainisha mgawanyo wa wafanyakazi wa afya, na kwa njia ya majaribio kutathmini ufanisi wa utendaji wa kazi kwa ngazi ya kituo na hospitali katika wilaya mbili kwa kuzingatia viashiria vya afya. Vilevile, Serikali inakusudia kutekeleza Mkakati wa Afya ya Jamii na kuendelea na ukarabati mkubwa wa majengo ya Bohari kuu ya dawa na Maabara ya Mkemia Mkuu yaliyopo Maruhubi. Pia Serikali katika mwaka wa fedha 2012/2013 inakusudia kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa uchangiaji wa huduma za Afya. Naomba kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uamuzi sahihi wa kutaka mama wajawazito wasihusike katika kuchangia huduma za afya nchini.

Mhe. Naibu Spika, Suala la kuwapatia wananchi maji safi na salama ni suala muhimu sana, na kero inayowaathiri wananchi wetu wengi. Serikali itatilia mkazo zaidi sekta hii kwa kuijengea uwezo zaidi Mamlaka ya Maji na kuimarisha shughuli za maji mijini na vijijini. Serikali inasisitiza zaidi wananchi kutunza miundombinu ya maji na kulinda vyanzo vya maji ili kuliondoa kabisa tatizo la maji nchini. Aidha, wananchi wanaopata huduma ya maji wanahimizwa kuchangia huduma hii, ili kuifanya huduma hiyo kuwa endelevu.

MIGOGORO YA ARDHI

Mhe. Naibu Spika, Serikali inaendelea kufuatilia suala la migogoro ya ardhi ambayo imeibuka katika miaka ya hivi karibuni. Migogoro hiyo imesababishwa na viongozi na baadhi ya watendaji katika wizara husika, mikoa na wilaya. Pia wananchi nao ni sehemu ya tatizo hili kwa kutofuata taratibu na Sheria za umiliki na uhaulishaji wa ardhi. Ofisi yangu kuanzia mwezi wa Januari hadi Machi 2012 imepokea jumla ya malalamiko 35 yanayohusu migogoro ya ardhi. Migogoro hii inahusu zaidi uvamizi wa maeneo ya wazi na uuzaji wa mashamba na viwanja. Baadhi ya migogoro ipo katika vyombo vya sheria na inafanyiwa kazi. Maagizo ya Serikali ni kwamba Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Wizara inayoshughulikia masuala ya ardhi waendelee kutafuta ufumbuzi wa migogoro hiyo ili kurejesha

imani ya wananchi kwa Serikali yao. Aidha, wananchi wazidi kuelimishwa umuhimu wa kufuata sheria na taratibu za matumizi bora ya ardhi. Serikali haitawavumilia viongozi na watendaji wanaojihusisha na kusababisha migogoro ya ardhi nchini, na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

SENSA YA WATU NA MAKAAZI

Mhe. Naibu Spika, Mwaka 2012 ni mwaka wa Sensa ya Watu na Makaazi nchini. Sensa hiyo imepangwa kufanyika tarehe 26 Agosti, 2012 miaka kumi baada ya Sensa ya mwisho iliyofanyika mwaka 2002. Hii itakuwa ni Sensa ya tano kufanyika tangu Tanganyika kupata uhuru na kufanyika kwa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Serikali inafanya sensa ya watu na makaazi ili kupata takwimu na taarifa sahihi zitakazotumika katika kupanga mipango na programu za maendeleo na kutayarisha sera mbalimbali. Nachukua fursa hii kutoa wito kwa viongozi wa serikali na wa vyama vya siasa, taasisi za kidini, makundi mengine ya kijamii na vyombo vya habari kuhamasisha wananchi kushiriki katika zoezi la Sensa hapo tarehe 26/08/2012 na kuendelea. Lengo kuu la uhamasishaji ni kuhakikisha wananchi wote wanaelewa umuhimu wa Sensa ili waweze kutoa ushirikiano unaohitajika kwa maendeleo yao na taifa kwa jumla.

MASUALA YA MTAMBUKA

Mhe. Naibu Spika, katika juhudi za kuendelea kudhibiti UKIMWI katika nchi yetu, Serikali kupitia Tume ya UKIMWI tayari imekamilisha matayarisho ya Mkakati wa Pili wa Kupambana na UKIMWI na tayari Mkakati huo umeshazinduliwa rasmi. Aidha, Mpango wa utekelezaji wa Mkakati huo pamoja na gharama zake tayari umeshaandaliwa. Natoa wito kwa wananchi wote kujiepusha na mambo yote yanayoweza kuleta maambukizi mapya ya UKIMWI na pia nawasihi kuacha unyanyapaa kwa wale wenzetu ambao kwa bahati mbaya tayari wameshapata maambukizi. Ni vyema kwa kila mmoja wetu kuchunguza afya yake ili kujua kama yuko salama au amepata maambukizi ili kuweza kuchukua hatua zinazostahiki.

Masuala ya Watu Wenye Ulemavu

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatoa kipaumbele katika kuyashughulikia masuala ya Watu Wenye Ulemavu. Watu Wenye Ulemavu wanakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo ufikiaji wa huduma za kijamii, zikiwemo afya, ajira na kuyafikia majengo yanayotoa huduma za umma. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeanzisha dawati la maafisa waratibu wa masuala ya Watu Wenye Ulemavu katika taasisi zote za umma. Jukumu kubwa la waratibu hawa ni kuleta ushawishi katika kuingiza masuala ya Watu Wenye Ulemavu katika mipango ya maendeleo ya kisekta. Aidha, serikali imeanza zoezi la usajili wa Watu Wenye Ulemavu ili kuweza kutambua ukubwa wa tatizo la Watu Wenye Ulemavu pamoja na kuainisha maeneo wanamoishi na mahitaji yao.

Mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya

Mhe. Naibu Spika, katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini, Sheria Namba 9 ya mwaka 2009 tayari imeshafanyiwa mapitio na kurekebishwa na sasa inasomwa pamoja na Sheria Namba 12 ya mwaka 2011 ya Udhibiti na Usafirishaji wa Dawa Haramu za Kulevya. Kumalizika kwa Sheria hii kutasaidia serikali katika kuratibu mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Aidha, mwongozo wa kuanzisha nyumba za makaazi kwa wanaotaka kuacha kutumia dawa za kulevya (*sober houses*) umeandaliwa na kukamilika.

Mazingira

Mhe. Naibu Spika, dunia hivi sasa inakabiliwa na changamoto kubwa ya mabadiliko ya tabianchi. Katika kukabiliana na hali hii serikali inaendelea kutoa elimu ya namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa viongozi na wananchi.

Maafa

Mhe. Naibu Spika, mnamo tarehe 10/09/2011, nchi yetu ilipatwa na msiba mkubwa uliotokana na kuzama kwa meli ya MV. Spice Islanders I. Tukio hili lilisababisha vifo vya watu 1,529 na watu 941 kuokolewa wakiwa hai, pamoja na mali kadhaa kupotea. Kwa mara nyengine tena nachukua nafasi hii kuwapa pole wale waliopatwa na maafa haya.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na kuguswa na tukio hilo, taasisi, mashirika na wananchi mbalimbali wa ndani na nje ya nchi walitoa misaada ya kifedha na bidhaa aina mbalimbali ili kuweza kusaidia shughuli za operesheni pamoja na misaada kwa waathirika wa ajali hiyo. Kwa upande wa fedha, jumla ya Shs. 1,248,550,761 zilichangwa.

Mhe. Naibu Spika, uamuzi wa serikali ni kuwa, fedha hizo zote zimegawiwa kwa waathirika wa maafa hayo, ambapo kila abiria aliyenusurika alipatiwa Shs 412,500 na warithi wa abiria waliofariki walipatiwa Shs 550,000 kwa kila maiti mmoja. Misaada mengine ya vyakula viligawiwa katika vituo vya kulelea watoto yatima na wazee wasiojiweza Unguja na Pemba. Hadi tarehe 15 Juni 2012, jumla ya walionusurika 604 (Unguja 164 na Pemba 440) sawa na asilimia 64 ya matarajio walikwishapewa fedha zao zilizofikia Shs 249,150,000. Aidha, ndugu wa abiria waliofariki 1,266 (Unguja 330 na Pemba 936) sawa na asilimia 83 ya matarajio walipatiwa fedha zao zilizofikia Shs 696,300,000. Kwa ujumla fedha zilizokwishalipwa ni Shs 945,450,000 sawa na asilimia 76 ya fedha zote zilizotolewa na wahisani.

Mhe. Naibu Spika, katika zoezi la ugawaji wa fedha hizi, zilijitokeza changamoto mbalimbali, ikiwemo baadhi ya majina kukosekana katika orodha iliyotolewa na Tume ya Rais ya Kuchunguza Ajali ya Meli ya MV. *Spice Islander I*. Majina yaliyolalamikiwa kutoonekana katika orodha ya Tume ni 266 kwa waliofariki (Unguja 97 na Pemba 169) na kwa waliookolewa wakiwa hai malalamiko ni majina 37 (Unguja 20 na Pemba 17).

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Maafa inaendelea kuyahakiki majina yaliyolalamikiwa kwa kushirikiana na Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Masheha na kwa wale watakaothibitishwa kuwa na malalamiko halali utaratibu utafanywa wa kuwapatia fedha zao haraka iwezekanavyo.

Mhe. Naibu Spika, serikali inatoa shukrani kwa wale wote waliochangia kwa hali na mali katika zoezi zima la kuyakabili maafa hayo. Aidha, Serikali kwa upande wake inaendelea na jitihada za kuimarisha uwezo wa taasisi zetu za kukabiliana na maafa ili tuweze kuchukua hatua kikamilifu katika kujiandaa na kuyakabili maafa ya aina mbalimbali. Hatua hizo ni pamoja na kurekebisha Sheria yetu ya Maafa, kuandaa mwongozo wa kutekeleza Sera ya Maafa, kuanzisha vituo vya uokozi na kununua vifaa na kutoa elimu kwa jamii juu ya namna ya kukabiliana na maafa.

MUELEKEO WA VIPAUMBELE VYA OFISI KWA MWAKA 2012/2013

Mhe. Naibu Spika, Mwelekeo wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni kuwa na mpango kazi kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ambao unatekelezeka na utakaozingatia vipaumbele vya ofisi na kufikia malengo yaliowekwa. Miongoni mwa vipaumble hivyo ni kuimarisha kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na kuyafanyia matengenezo majengo ya kiwanda yaliyopo Maruhubi na kununua mitambo mipya ya uchapaji kwa ajili ya kiwanda hicho.

Mhe. Naibu Spika, pia Ofisi yetu kwa kushirikiana na *COSTECH* na wadau wengine itaendelea kuimarisha shughuli za utafiti nchini kwa kuainisha vipaumbele vya utafiti, kuzijengea uwezo kamati za kusimamia masuala ya utafiti, kuwajengea uwezo watafiti chipukizi pamoja na kutafuta fedha kwa ajili ya kazi za utafiti.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile nchi yetu inakabiliwa na sherehe kubwa za Maadhimisho ya Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Ofisi imeweka kipaumbele kwa matayarisho ya sherehe hizo ikiwemo ununuzi wa vifaa mbali mbali na kuandaa mpango mzima wa maadhimisho utakaowashirikisha kikamilifu wadau mbali mbali kwa ajili ya kufanikisha sherehe hizo. Pia Ofisi imeweka kipaumbele katika kuendelea kujenga uwezo wa jamii juu ya kukabiliana na maafa kwa kutoa elimu, kutafuta vifaa, kuanzisha vituo vya dharura na kuandaa majaribio ya kukabiliana na maafa (*simulation exercises*). Mkazo pia utawekwa katika kuwajengea uwezo wafanyakazi kuwapatia elimu, mafunzo na vitendea kazi vya uhakika ili kuimarisha mazingira ya kazi na kuongeza ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, katika maandalizi ya uchaguzi mkuu ujao kipaumbele kimewekwa katika kuimarisha daftari la kudumu la wapiga kura, kutoa elimu kwa wapiga kura, pamoja na upatikanaji wa vitendea kazi zikiwemo gari ili kufanikisha shughuli za Tume. Aidha, mkazo umewekwa katika kuliimarisha Baraza la Wawakilishi kwa kuwajengea uwezo wajumbe wa Baraza hilo na watendaji ili kuwaongezea ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande wa ukusanyaji mapato, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika mwaka wa fedha 2012/2013 imekadiriwa kukusanya Jumla ya Shs. 239,000,000. Fedha hizo zitakusanywa kutoka kianzio cha mapato ya Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

MAJUKUMU YA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa muhtasari wa utekelezaji wa shughuli za serikali kupitia sekta mbali mbali na kuelezea mwelekeo wa vipaumbele vya ofisi kwa mwaka, 2012/2013 sasa naomba uniruhusu kutoa maelezo ya mafanikio ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi yangu kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na malengo yaliyopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ina jukumu kubwa la kusimamia na kuratibu masuala ya Kitaifa katika ngazi mbalimbali hapa Zanzibar. Ofisi hii ni Kiungo na Mtendaji Mkuu wa shughuli zote za Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar. Majukumu Mahususi ya Ofisi hii ni kama ifuatavyo:-

i. Kuratibu Shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na za Muungano, ikiwemo Miradi ya Muungano ndani ya SMZ.
ii. Kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala 2010 – 2015.
iii. Kuratibu na Kusimamia Shughuli za Utafiti
iv. Kusimamia shughuli za Kukabiliana na Maafa
v. Kusimamia na Kuratibu Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na shughuli za kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa
vi. Kusimamia Shughuli za Upigaji Chapa
vii. Kuratibu shughuli za Tume ya Uchaguzi
viii. Kuratibu Shughuli za Baraza la Wawakilishi

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake ilikadiriwa kutumia jumla ya Shs 13,912,299,995 (ikiwa ni pamoja na ongezeko la mishahara). Kati ya hizo Shilingi 13,197,299,995 kwa kazi za kawaida na Shilingi 715,000,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2012, ofisi iliingiziwa Shilingi 10,682,793,499 (sawa na asilimia 77). Kati ya hizo Shilingi 10,256,793,499 kwa kazi za kawaida (sawa na asilimia 83) na Shilingi 426,000,000 kwa kazi za maendeleo (sawa na asilimia 60) [**Kiambatanisho 1A na 1B**].

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kutoa taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha miezi tisa Julai, 2011 hadi Machi, 2012 kupitia idara na taasisi zilizochini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

OFISI YA FARAGHA YA MAKAMU WA PILI WA RAIS.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Faragha ina jukumu la kutoa huduma kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kwa kupitia Ofisi Kuu ya Zanzibar na Ofisi zilizopo Pemba, Dar-es-Salaam na Dodoma.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Ofisi ya Faragha iliidhinishiwa Shs. 336,181,121 (pamoja na nyongeza za mishahara) kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo Shs. 206,061,121 kwa malipo ya mishahara, posho na mchango wa *ZSSF* na Shs.130, 120,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2012, Ofisi ya Faragha iliingiziwa jumla ya Shs. 277,888,605 sawa na asilimia 83 ya fedha zote.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Faragha imeratibu ziara 28 za ndani ya nchi [Pemba ziara nane (8), Unguja ziara 12 na ziara nane (8) katika mikoa ya Tanzania Bara]. Ziara za ndani ya nchi za Mhe. Makamu wa Pili wa Rais zilikuwa na lengo la kuonana na wananchi na kusikiliza matatizo yao, kukaguwa miradi ya maendeleo ya wananchi pamoja na kuwafariji wahanga wa *M.V. Spice Islander I*. Aidha, Ofisi ya Faragha imeratibu ziara tano (5) za Makamu wa Pili wa Rais katika nchi za China, Marekani, Israel, Cuba na Nchi za Falme za Kiarabu. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kwenye ziara hizo ni kupatikana msaada wa fedha kutoka Jamhuri ya Watu wa China wa Yuan milioni 50 sawa na Shs. bilioni 12.5 na kupata msaada wa vifaa mbali mbali kutoka Shirika la *MED International* la Marekeni. Aidha, ziara hizi zimeimarisha mashirikiano na kupata ahadi mbali mbali za misaada katika nyanja za mafunzo, kilimo, uvuvi, afya na vifaa vya kukabiliana na maafa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, Ofisi ya Faragha katika mwaka wa fedha wa 2011/12 imeweza kutekeleza mambo yafuatavyo:-

i. Jumla ya ahadi 39 zilitolewa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa wananchi na kati ya hizo ahadi 27 zimetekelezwa na ahadi 12 zinaendelea kushughulikiwa.
ii. Ofisi imenunua vifaa mbali mbali kwa ajili ya kukiimarisha Kitengo cha Utoaji wa Habari na kuzifanyia matengenezo gari nane (8) kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Faragha.
iii. Ofisi za Faragha Vuga zimefanyiwa matengenezo pamoja na nyumba za makaazi za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais ziliopo Mazizini Unguja, Dodoma na Dar es Salaam na kuwekwa samani mpya.
iv. Wafanyakazi watano (5) wa Ofisi ya Faragha wamepatiwa mafunzo katika fani mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ya Faragha imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuimarisha kazi za ushauri wa masuala ya sheria, uchumi na maendeleo ya kijamii kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.
b) Kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa wafanyakazi.
c) Kuratibu ziara za Makamu wa Pili wa Rais za ndani na nje.
d) Kufuatilia ahadi zinazotolewa na Makamu wa Pili wa Rais.
e) Kuimarisha shughuli za upokeaji na utoaji wa habari za Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.
f) Kuimarisha huduma za usafiri, ununuzi wa vifaa vya ofisi, matengenezo ya magari na kulipa maslahi ya wafanyakazi.
g) Kusimamia matengenezo ya nyumba za Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mazizini Unguja, Dar-es-Salaam na Dodoma.

Mhe. Naibu Spika, ili Ofisi ya Faragha iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2012/2013, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shs. 365,223,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shs. 210,223,000 zitatumika kwa malipo ya mishahara, posho za wafanyakazi na mchango kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) na Shs. 155,000,000 kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ina majukumu ya kusimamia shughuli za utumishi na uendeshaji katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Vilevile, idara ina jukumu la kusimamia shughuli za ununuzi na uhifadhi wa mali za serikali.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shs. 481,391,922 (pamoja na nyongeza ya mishahara) kwa matumizi ya kazi za kawaida ambazo Shs. 351,391,922 kwa malipo ya mishahara, posho na mchango wa ZSSF na Shs. 130,000,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2012, idara iliingiziwa jumla ya Shs. 361,042,908 ambazo ni sawa na asilimia 75 ya makadirio.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Uendeshaji na Utumishi iliweza kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Idara imefanya tathmini ya mafunzo kwa wafanyakazi na kuandaa Mpango Mkuu wa Mafunzo wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.
ii. Idara imenunua vifaa mbali mbali vya ofisi pamoja na kufanya matengenezo ya jengo la ofisi na vyombo vya usafiri.
iii. Idara imeratibu masomo ya muda mrefu na mfupi kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Jumla ya wafanyakazi 57 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi (wanaume 34 na wanawake 23) na wafanyakazi 26 (wanaume 14 na wanawake 12) walipatiwa mafunzo ya muda mfupi [**Kiambatanisho Nam. 2**].

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i) Kusimamia maslahi ya wafanyakazi wa Idara za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

ii) Kusimamia ununuzi wa vifaa vya ofisi na matengenezo ya vyombo vya usafiri.
iii) Kuimarisha huduma za usalama kazini na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya kujikinga na majanga mbali mbali.
iv) Kuimarisha kitengo cha manunuzi na uondoaji wa mali za serikali, huduma za ghala pamoja na uwekaji wa kumbukumbu za ofisi.
v) Kusimamia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa mujibu wa Mpango Mkuu wa Mafunzo wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais (*Training Master Plan*).
vi) Kuratibu na kutekeleza mfumo wa tathmini wa utendaji kazi wa wafanyakazi wa Ofisi.
vii) Kuandaa semina kwa wafanyakazi kuwaelimisha juu ya Sheria na Kanuni za Utumishi Serikalini kwa lengo la kuongeza uwajibikaji na kuleta ufanisi.
viii) Kufanya tathmini ya mahitaji ya wafanyakazi na kuajiri wafanyakazi wapya kwa mujibu wa mahitaji.
ix) Kuandaa semina kwa wafanyakazi juu ya uhamasishaji wa kupambana na UKIMWI.

Mhe. Naibu Spika, ili idara iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2012/2013 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shs. 866,184,000 ambazo Shs. 455,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na Shs. 411,184,000 kwa malipo ya mishahara, posho na mchango wa *ZSSF*.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Naibu Spika, Idara Mipango Sera na Utafiti ni kiungo cha idara na taasisi nyengine zilizopo katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika masuala ya mipango, bajeti, sera na utafiti. Aidha, idara hii ina jukumu la kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kutayarisha ripoti za utekelezaji za miezi mitatu, miezi sita na mwaka mmoja.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, idara hii iliidhinishiwa jumla ya Shs. 188,976,707 (pamoja na nyongeza ya mishahara) kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo Shs. 100,000,000 kwa matumizi mengineyo na Shs. 88,976,707 kwa kulipia mishahara, posho na mchango wa *ZSSF*. Hadi kufikia Machi, 2012, idara ilipatiwa jumla ya Shs. 153,296,237 kwa matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 81. kwa matumizi ya kazi za kawaida

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Idara ya Mipango Sera na Utafiti imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Idara imeimarisha tovuti ya serikali kwa kununua vifaa vipya na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa kitengo katika usimamizi na uendeshaji wa tovuti hiyo.
ii. Idara imeshiriki katika kuandaa Sheria ya Mfuko wa Jimbo.
iii. Idara imegharamia wafanyakazi wanne (4) walioko katika mafunzo ya muda mrefu.
iv. Idara imetoa mafunzo kwa wafanyakazi 11 kutoka Idara mbali mbali za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais juu ya kuibua na kuandaa miradi ya maendeleo.
v. Idara imetoa vibali 136 kwa watafiti wa ndani na nje ya nchi katika sekta za utamaduni, siasa, utalii, kilimo, uvuvi.
vi. Idara imemuunganisha na *COSTECH* mvumbuzi wa gari la aina ya SUGU II na kumuwezesha kupata Tuzo ya *TASTA* (*Bronze*), fedha Shs. 2,000,000 na vifaa vyenye thamani ya Shs. 12,700,000,
vii. Idara imewaunganisha watafiti wa kilimo na *COSTECH* na kuweza kupata fedha za kugharamia machapisho ya tafiti zao (*conference proceedings*) na watafiti watatu kutoka *SUZA* na *IMS* walipatiwa fedha jumla ya Shs. 523,870,000 kwa kufanya tafiti hapa Zanzibar.
viii. Idara imeratibu upatikanaji wa jumla ya Shs. 641,650,000 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya utafiti katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo-Kizimbani.
ix. Idara kwa kushirikiana na *COSTECH* na *SUZA* imeandaa mkutano uliowashirikisha watafiti wa Zanzibar juu ya zoezi la ukusanyaji wa tafiti zilizofanywa Zanzibar.
x. Idara imeratibu kupatikana kwa jengo la Ofisi ya *COSTECH* na Tume ya mionzi katika jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapo Tungu. Ofisi hizo zimefunguliwa rasmi tarehe 11/6/2012 na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.
xi. Idara imeratibu vikao vya kuandaa vipaumbele vya utafiti vilivyowashirikisha wataalamu kutoka katika sekta za mipango, fedha, kilimo, ujasiriamali, uwezeshaji, ulinzi, usalama na uhamiaji.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Mipango Sera na Utafiti imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kwa kushirikiana na *COSTECH* kuvijengea uwezo vitengo vya utafiti vya Wizara za SMZ na kuwajengea uwezo watafiti chipukizi wa Zanzibar.

b) Kushirikiana na wadau wa sekta mbalimbali kuainisha na kuibua vipaumbele vya utafiti nchini kwa mujibu wa mahitaji ya MKUZA II

c) Kuandaa Mpango Kazi wa masuala ya kuendeleza utafiti nchini

d) Kuratibu kazi za Kamati ya Utafiti wa Rasilimali za Nchi na Kamati ya Taifa ya Utafiti.

e) Kwa kushirikiana na wadau mbali mbali kuandaa mikutano, warsha na makongamano kuhusu masuala ya utafiti

f) Kuanzisha mahusiano na taasisi mbali mbali za utafiti ndani ya nchi, kikanda na kimataifa.

g) Kuimarisha vitendea kazi ikiwemo vyombo vya usafiri, vifaa vya ofisi na kulipia maslahi ya wafanyakazi.

h) Kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani za uchambuzi wa sera, mipango na uandaaji wa miradi ya maendeleo.

i) Kuandaa mipango ya muda mrefu na muda mfupi na kuibua miradi ya maendeleo kwa mujibu wa mpango wa MKUZA II.

j) Kuimarisha Kitengo cha Kufuatilia na Kutathmini utekelezaji wa malengo ya ofisi na kuandaa ripoti za utekelezaji za robo mwaka, nusu mwaka na mwaka mzima.

k) Kuandaa mikutano ya kutathmini ripoti za utekelezaji.

Mhe. Spika, Ili Idara iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2012/2013 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shs.223,356,000 kati ya hizo Shs.162,000,000 kwa matumzi ya kazi za kawaida na Shs. 61,356,000 kulipia mishahara, posho na mchango wa ZSSF.

IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ina jukumu la kuratibu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shughuli za Muungano ndani ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ilipangiwa kutumia jumla ya Shs.241,116,952 (pamoja na nyongeza ya mishahara) kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo Shs.110,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na Shs. 131,116,952 kwa mishahara, posho na mchango wa ZSSF. Hadi kufikia Machi 2012, Idara iliingiziwa Shs.181,799,411 (sawa na asilimia 75). Aidha, Idara iliidhinishiwa jumla ya Shs.590,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa SMZ kwa Programu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na miradi midogo midogo ya wananchi. Hadi kufikia Machi 2012, Idara imeingiziwa Shs.333,000,000 (sawa na asilimia 56) ambapo Shs.63,000,000,000 kwa miradi ya TASAF na Shs.270,000,000,000 kwa miradi ya maendeleo ya jimbo (ZCDF).

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Idara imeratibu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 - 2015 katika Wizara za SMZ na Mikoa yote ya Unguja na Pemba na kuandaa taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha mwaka mmoja (Oktoba 2010-Septemba 2011).
ii. Idara imeendelea kuzikusanya na kuzifuatilia ahadi mbali mbali zilizotolewa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano na Ofisi za Mikoa, Wilaya pamoja na taasisi nyengine.

iii. Idara imepokea na kuratibu jumla ya malalamiko ya wananchi 126 na kati ya hayo 9 yanashughulikiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, 92 yanaendelea kushughulikiwa kwa mashirikiano na taasisi zinazohusika na 25 tayari yamepatiwa ufumbuzi.

iv. Idara imeratibu vikao saba (7) vinavyohusu changamoto za Muungano kwa ngazi ya watendaji, vikao vitatu (3) vya Makatibu Wakuu na vikao viwili (2) katika ngazi ya Mawaziri.

v. Idara imeratibu kikao kimoja cha Kamati ya Pamoja ya Waziri Mkuu (SMT) na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichofanyika tarehe 28/01/2012 katika jiji la Dar-es-Salaam.

vi. Idara imeratibu vikao sita (6) vya kisekta vya mashirikiano baina ya SMT na SMZ kwa taasisi zisizo za Muungano.

vii. Idara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Tawala za Mikoa imefuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Jimbo kupitia Mfuko wa Wabunge na kuandaa taarifa.

viii. Idara imeratibu ugawaji wa fedha za miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na Majimbo yote yameshapatiwa fedha hizo.

ix. Idara imegharamia mafunzo kwa wafanyakazi watano (5) walioko masomoni katika fani tofauti.

x. Idara imeratibu vikao vinne (4) vya Baraza la Wawakilishi na vikao viwili (20 vya Bunge vinavyohusu Bajeti na Marekebisho ya Katiba

xi. Idara imesimamia utekelezaji wa miradi 41 ya Maendeleo ya Jamii –*TASAF* (Unguja 26 na Pemba 15) ambayo iligharimu jumla ya Shs.896,165,238.80 fedha hizo zimetolewa na Benki ya Dunia **(Kiambatanisho Nam**. **3A na 3B**).

xii. Idara imetoa mafunzo kwa Kamati 90 za usimamizi na utekelezaji wa miradi. Aidha, Idara imetayarisha makala za magazeti na vijarida 20 (Pemba 10 na Unguja 10) kwa lengo la kuelimisha umma juu ya miradi ya *TASAF* hapa Zanzibar.

xiii. Idara iliratibu ziara ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Wakuu wa sekta za SMZ kwa lengo la kuangalia utekelezaji wa miradi ya TASAF.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kukusanya na kuanda taarifa za utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010-2015.
b) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi za viongozi wakuu wa Kitaifa.
c) Kuratibu malalamiko ya wananchi yanayowasilishwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.
d) Kuratibu vikao vya Baraza la Wawakilishi na Bunge.
e) Kukusanya taarifa za utekelezaji kwa kila Wizara na kuandaa taarifa za utekelezaji.
f) Kuratibu vikao vya Waziri Mkuu (SMT) na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.
g) Kuratibu vikao vya mashirikiano kati ya Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Wizara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT).
h) Kuratibu utekelezaji wa miradi ya Muungano inayotekelezwa Zanzibar, ikiwa pamoja na kuanza utekelezaji wa *TASAF III*.
i) Kuratibu miradi ya maendeleo ya jimbo.
j) Kuimarisha kitengo cha Habari, Mawasiliano na Elimu (*ICE*) kwa ununuzi wa vifaa na kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa kitengo.
k) Kuandaa muongozo wa kuendesha TOVUTI ya Serikali.
l) Kuwajengea uwezo wa kitaaluma katika masuala ya uratibu wafanyakazi wa Idara pamoja na maofisa viungo wa wizara za SMZ (focal Persons).
m) Kuimarisha huduma za usafiri na vitendea kazi vya idara na kulipa maslahi ya wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, ili Idara iweze kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shs.346,377,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo Shs.131,377,000 zitatumika kwa malipo ya mishahara, posho na mchango wa ZSSF na Shs.215,000,000 kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa miradi ya maendeleo naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shs.840,000,000. Shilingi 760,000,000 kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo na Shs.80,000,000 mchango wa Serikali kwa Program ya Mfuko wa Maendeleo ya jamii (*TASAF*).

IDARA YA KUKABILIANA NA MAAFA

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Kukabiliana na Maafa ina jukumu la kuratibu masuala yote yanayohusiana na maafa hapa Zanzibar kama ilivyoainishwa katika Sheria Nam.2 ya Kusimamia Maafa ya mwaka 2003.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Kukabiliana na Maafa ilipangiwa kutumia jumla ya Shs.168,371,475 (pamoja na nyongeza ya mishahara) kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo Shs.68,371,475 kwa malipo ya mishahara, posho na mchango wa *ZSSF* na Shs.100,000,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2012, Idara imeingiziwa jumla ya Shs.148,781,442 sawa na asilimia 88. Aidha, Idara ilipangiwa Shs.50,000,000 kwa kazi za Maendeleo kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi, 2012, Idara imeingiziwa jumla ya Shs.18,000,000 kutoka Serikalini sawa na asilimia 36. Aidha, Washirika wa Maendeleo ambao ni *UNICEF* na *UNDP* walitarajiwa kutoa Shs.395,200,000 na hadi kufikia Machi, 2012, Wahisani hao walikwishatoa Shs.137,319,200 sawa na asilimia 35 ya matarajio.

Mhe. Naibu Spika**,** Idara ya Kukabiliana na Maafa katika mwaka wa fedha 2011/2012 iliweza kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Rasimu ya awali ya Sheria ya Kukabiliana na Maafa imetayarishwa.
ii. Idara imefanya uchambuzi wa awali wa hali ya maafa na uwezo wa Shehia katika kukabiliana na maafa kwa Shehia 13 za Wilaya ya Micheweni na shehia 20 za Wilaya ya Wete, Pemba. (**Kiambatanisho. Nam. 4**).
iii. Idara imeandaa Mipango ya Kujiandaa Kukabiliana na Maafa kwa Wilaya za Wete na Micheweni Pemba. Rasimu za awali za Mipango hiyo zimekamilika na kuwasilishwa kwa wadau wa Wilaya hizo kwa ajili ya kupata maoni yao.
iv. Idara imeanzisha kipindi maalumu kiitwacho **'Tukabiliane na Maafa'** ambacho kinarushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (*ZBC*) Radio ambacho kinatoa elimu ya kukabiliana na Maafa.
v. Idara imekusanya taarifa ya vifaa vya kukabiliana na maafa katika taasisi 42 za Serikali na taasisi tano (5) zisizo za kiserikali.
vi. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeunda timu maalum inayoshirikisha wataalam kutoka taasisi mbalimbali za kukabiliana na maafa ili kuchambua mahitaji ya vifaa na mafunzo kwa taasisi za kukabiliana na maafa hapa nchini**. (Kiambatanisho Nam. 5).**
vii. Kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Kanda ya Zanzibar, Idara imetoa taarifa mbali mbali juu ya mwelekeo wa hali ya hewa hasa ya uwezekano wa kuwepo mvua na upepo mkubwa ili jamii iweze kuchukua hatua zinazostahiki.
viii. Idara imeratibu zoezi la operesheni kufuatia ajali ya kuzama kwa meli ya *MV. Spice Islanders I* ikiwa ni pamoja na kazi za uokozi, mazishi, upokeaji wa misaada, ziara za Viongozi Wakuu kwa ajili ya kutoa mkono wa pole, pamoja na kugawa fedha kwa waathirika wa ajali hiyo Unguja na Pemba. Jumla ya familia 1,526 zilipatiwa ubani (Unguja 500 na Pemba 1,026), ubani huo ulikuwa fedha taslim Shilingi 152,600,000.
ix. Idara imeandaa muongozo wa kufanya tathmini mara tu baada ya maafa kutokea na Rasimu ya awali ya Mwongozo huo imekamilika na kuwasilishwa kwa wadau Unguja na Pemba ili kupata maoni yao.
x. Ili kuhakikisha kuwa Sera ya Kukabiliana na Maafa inatekelezwa na wadau wote, Idara imeendesha warsha za kuitangaza Sera hiyo kwa maafisa Mipango wa Wizara na Wilaya zote Unguja na Pemba. Pia Sera hiyo imewasilishwa katika Mkutano wa wadau wa masuala ya maafa *(Zanzibar sub national platform for disaster risk reduction)* uliofanyika kisiwani Pemba. Pia Idara imetafuta Washauri wa kutayarisha Muongozo wa Utekelezaji wa Sera ya Kukabiliana na Maafa (*National Operational Guidelines for Disaster Management Policy*) pamoja na Muongozo wa Kufuatilia na Kutathmini utekelezaji wa Sera ya Kukabiliana na Maafa (*Monitoring and Evaluation Framework for Disaster Management Policy)*.
xi. Idara imewagharamia wafanyakazi sita (6) katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kukamilisha Sheria mpya ya kukabiliana na maafa.
b) Kununua vifaa mbali mbali vya kukabiliana na maafa.
c) Kufanya matengenezo ya mitambo na redio za mawasiliano.

d) Kutayarisha vipindi vya kuelimisha jamii kupitia redio na TV.
e) Kuendelea kutoa mafunzo ya kukabiliana na maafa kwa Shehia 50 za Unguja na Pemba.
f) Kuandaa majaribio ya kukabiliana na maafa (*simulation exercises*).
g) Kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa wafanyakazi wa idara.
h) Kuimarisha vitendea kazi muhimu vya Ofisi ikiwemo vyombo vya usafiri, vifaa vya Ofisi na kulipa maslahi ya wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, Ili Idara ya Kukabiliana na Maafa iweze kutekeleza malengo yake katika mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinishia jumla ya Shs.210,674,000 kwa kazi za kawaida, kati ya hizo Shs.94,674,000 kwa ajili ya malipo ya mishahara, posho na mchango wa *ZSSF* na Shs.116,000,000 kwa matumizi ya kazi nyenginezo. Aidha, Idara inaomba kuidhinishiwa Shs. 674,000,000, ikiwa Shs.624,000,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Shs. 50,000,000 ikiwa ni mchango wa Serikali.

IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA

Mhe. Naibu Spika**,** Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ina jukumu la Kusimamia na Kuratibu Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa, na kusimamia shughuli za Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, ikiwemo kushughulikia mazishi, hitma pamoja na kutunza kumbukumbu za viongozi hao.

Mhe. Naibu Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ilipangiwa kutumia jumla ya Shs. 870,923,192 (pamoja na nyongeza ya mishahara) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo Shs.40,923,192 kwa matumizi ya mishahara, posho na mchango wa ZSSF na Shs.830,000,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2012, Idara iliingiziwa Shs. 858,646,606 sawa na asilimia 99.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Idara imenunua vifaa mbali mbali vya uendeshaji wa ofisi pamoja na kuweka huduma za mawasiliano (*Internet*).
ii. Idara imegharamia wafanyakazi wanne (4) kwa ziara za mafunzo Tanzania Bara na China.
iii. Idara imeandaa nakala 500 za kalenda za Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa kwa njia ya vitabu vidogo na kuzisambaza kwa wadau mbali mbali nchini.
iv. Idara imesimamia na kuratibu Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ikiwa pamoja na:-

    a) Sherehe za miaka 48 ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizofikia kilele chake tarehe 12/1/2012 katika Uwanja wa Amaan Unguja.
    b) Maadhimisho ya siku ya Mashujaa (*Karume Day*) yaliyofanyika tarehe 07 Aprili, 2012
    c) Idara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu imeratibu sherehe za miaka 50 ya Uhuru wa Tanganyika na sherehe za miaka 48 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

v. Idara imeifanyia mapitio Sheria namba 10 ya mwaka 2002 ya Kuwaenzi Viongozi na tayari Rasimu ya Marekebisho ya Sheria hiyo imeandaliwa.
vi. Idara imeanza maandalizi ya awali ya kukusanya na kutunza kumbukumbu za Muasisi wa Taifa (Marehemu Mzee Abeid Amani Karume) kwa kuratibu kikao cha wadau wa kumbukumbu hizo na maoni yamekusanywa na yanaendelea kufanyiwa kazi.
vii. Idara imeandaa Rasimu ya Mwongozo wa namna ya kusherehekea miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar.
viii. Idara imeratibu mazishi ya marehemu Mussa Khamis Silima aliyekuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi (BLW) Jimbo la Uzini, marehemu Amour Mtondoo aliyekuwa Mjumbe wa BLW Jimbo la Bububu, marehemu Jaji Mkuu Mstaafu Worfgang Dourado, na marehemu Brigedia Jenerali Mstaafu Adam Clement Mwakanjuki.

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kununua vifaa vya sherehe kwa awamu ikiwemo mashamiana, vipaza sauti na mazulia (*red capets*).
b) Kuendelea na matayarisho ya sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar.
c) Kusimamia na kuratibu sherehe za miaka 49 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

d) Kuandaa na kushiriki katika maadhimisho na sherehe mbali mbali za Kitaifa kwa kushirikiana na taasisi husika.
e) Kuendelea na hatua za kukusanya taarifa na kumbukumbu za marehemu Mzee Abeid Amani Karume.
f) Kukamilisha mapitio ya Sheria namba 10 ya mwaka 2002 ya Kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa.
g) Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi wafanyakazi wa idara.
h) Kuanza matengenezo ya maghala ya kuhifadhia vifaa vya kuhifadhia sherehe.
i) Kuratibu na kusimamia dua katika Siku ya kumbukumbu ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume.
j) Kuimarisha huduma za usafiri, kununua vitendea kazi vya ofisi na kulipia maslahi ya wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika**,** ili Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shs. 868,375,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida, kati ya hizo Shs. 68,375,000 kwa malipo ya mishahara, posho na mchango ZSSF na Shs. 800,000,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

IDARA YA MPIGA CHAPA MKUU WA SERIKALI

Mhe. Naibu Spika**,** Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ina jukumu la kuchapisha nyaraka zote za Serikali, ikiwemo hotuba za bajeti, Sheria, Miswada na Risiti za Serikali. Aidha, Idara ina jukumu la kuuza shajala katika taasisi na Idara za Serikali.

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya Shs.528,021,009 (pamoja na nyongeza ya mishahara) kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo Shs.348,021,009 kwa malipo ya mishahara, posho na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) na Shs.180,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2011, Idara imeingiziwa jumla ya Shs.352,684,912 (sawa na asilimia 67). Aidha, Idara ilipangiwa kuchangia shs.136,604,000 katika Mfuko Mkuu wa Serikali na hadi kufikia Machi, 2012. Idara imekusanya na kuwasilisha Mfuko Mkuu wa Serikali Shs.104,016,850 sawa na asilimiwa 76 ya lengo.

Mhe. Naibu Spika**,** Katika mwaka 2011/2012, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali imeweza kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Idara imegharamia mafunzo ya wafanyakazi wanane (8) katika fani mbali mbali.
ii. Idara imezifanyia matengenezo baadhi ya mashine za kiwanda, zikiwemo SOM 225 na Adust na Zirkon 66 kwa ajili ya kazi za uchapishaji.
iii. Idara imechangia shs.104,016,850 sawa na asilimia 76 katika Mfuko Mkuu wa Serikali.
iv. Idara imetoa huduma ya machapisho mbalimbali yakiwemo Miswada ya Sheria, Katiba, Hotuba za Rais, Kalenda, Madaftari ya Mishahara (*Salary Registers*) pamoja na kazi za watu binafsi.
v. Idara imepata eneo kwa ajili ya ujenzi wa Bohari kuu huko Maruhubi karibu na eneo la Kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na kazi za kukusanya taarifa kwa matumizi ya shajala za Serikali imeanza.

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

a) Kuimarisha huduma za usafiri, kununua vitendea kazi vya Ofisi na kulipa maslahi ya wafanyakazi.
b) Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu wafanyakazi 8.
c) Kununua vifaa mbali mbali vya uchapishaji.
d) Kukamilisha uchambuzi yakinifu wa mahitaji ya shajala na vifaa vya Wizara na Taasisi za Serikali.
e) Kukamilisha mpango wa biashara (*Business Plan*) kwa ajili ya Kiwanda na Bohari kuu.
f) Kuandaa mapendekezo ya kuifanya Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kuwa Taasisi inayojitegemea.
g) Kununua na kufunga mitambo mipya ya uchapishaji inayotumia mfumo wa teknolojia ya Digitali.

Mhe. Naibu Spika**,** ili Idara iweze kutekeleza malengo hayo, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya fedha Shs.512,555,000. Kati ya hizo Shs.300,555,000 kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi, posho na mchango wa ZSSF na Shs.212,000,000 kwa matumizi mengineyo. Vile vile, naomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Shs.3,032,400,000 kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo Shs. 1,032,400,000 ni kwa ajili ya kununulia mitambo mipya ya uchapishaji na Shs.2,000,000,000 ni kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Kiwanda na

Utawala yaliyopo Maruhubi ili majengo hayo yawe na viwango vya kuweka mitambo mipya. Aidha, Idara imekadiriwa katika mwaka wa fedha 2012/2013 kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali Shs.239,000,000.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Naibu Spika**,** Ofisi Kuu ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba ina jukumu la kuratibu shughuli za Idara zote zilizo chini ya Ofisi hii kwa upande wa Pemba. Hivyo, utekelezaji wa Ofisi hii ni kama ilivyokwishaelezwa katika Idara mbalimbali za Ofisi.

Mhe. Naibu Spika, katika kutekeleza malengo ya mwaka 2011/2012, Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya Shs.331,455,514 (pamoja na nyongeza ya mishahara) kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo Shs.171,425,514 ni kwa ajili ya mishahara, posho na mchango wa *ZSSF* na Shs.160,030,000 ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2012, Ofisi iliingiziwa jumla ya Shs 237,132,164 (sawa na asilimia 72).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Ofisi Kuu Pemba itaendelea na kazi za uratibu wa kazi zote za Idara mbalimbali za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa upande wa Pemba. Ili kuweza kutekeleza kazi za uratibu wa shughuli hizo naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shs.357,256,000. Kati ya fedha hizo Shs.187,256,000 kwa ajili ya malipo ya Mishahara, posho na mchango wa ZSSF na Shs.170,000,000 kwa matumizi mengineyo.

TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Uchaguzi imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kama ilivyoelezwa katika ibara ya 119 (1) pamoja na Sheria Nam. 9 ya 1992 kwa madhumuni ya kuendeleza Demokrasia kwa njia ya Uchaguzi huru, wa haki na uwazi. Majukumu ya Tume ni kama ifuatavyo:-

i. Kusimamia mwenendo mzima wa Uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.
ii. Kukuza na kuendeleza elimu ya wapiga kura.
iii. Kusimamia ukataji wa mipaka ya majimbo ya Uchaguzi.
iv. Kuendeza Daftari la Kudumu la Wapiga kura
v. Kusimamia na kuendesha kura ya maoni

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shs.921,862,103 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo Shs. 701,859,103 kwa ajili ya malipo ya mishahara, posho na mchango wa *ZSSF* na Shs.220,003,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2012, Tume ya Uchaguzi iliingiziwa jumla ya Shs.702,001,197 sawa na asilimia 76.

Mhe. Naibu Spika**,** katika mwaka wa fedha 2011/2012, Tume ilitekeleza malengo yake kama ifuatavyo :-

i. Tume ilitoa elimu ya wapiga kura kupitia vyombo vya habari (radio na Televisheni) wakati wa Uchaguzi Mdogo wa Jimbo la Uzini.
ii. Tume imeimarisha jengo la Ofisi ya Tume ya Wilaya ya Kati.
iii. Tume imetoa mafunzo ya uchaguzi kwa Wajumbe na Watendaji wa Tume ndani na nje ya nchi.
iv. Tume imegharamia wafanyakazi 16 kwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imepanga malengo yafuatayo:-

a) Kuendeleza Daftari la kudumu la wapiga kura ;
b) Kuimarisha majengo ya Ofisi za Tume ya Uchaguzi za Wilaya ;
c) Kuwapatia mafunzo ya uchaguzi wajumbe wa Tume na watendaji wake;
d) Kuanza matayarisho ya mapitio ya mipaka ya majimbo;
e) Kuandaa Rasimu ya Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar; na
f) Kufanya Mapitio ya Sheria ya Uchaguzi Nam.11 ya 1984.

Mhe. Naibu Spika, ili kuweza kutekeleza malengo hayo naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe Shs.1,084,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo Shs.642,700,000 kwa malipo ya mishahara, posho na mchango wa ZSSF na Shs.441,300,000 kwa matumzi mengineyo.

OFISI YA BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe. Naibu Spika, Baraza la Wawakilishi Zanzibar limeundwa kwa maelekezo ya kifungu cha 63 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na majukumu yake ya msingi yanatajwa kwenye Kifungu cha 88 (1) cha Katiba kuwa ni Kutunga Sheria; Kujadili Shughuli za Wizara wakati wa Mkutano wa Bajeti; Kuihoji Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; na Kuidhinisha Mipango ya Serikali na kusimamia utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya Shs.9,129,000,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, Shs.4,629,925,000 kwa malipo ya mishahara, stahiki nyingine za Wajumbe na Wafanyakazi wa Baraza, pamoja na michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*); na Shs. 4,499,075,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi Kufikia Machi, 2012, Baraza liliingiziwa jumla ya Shs. 6,983,520,017. Kati ya hizo Shs. 3,219,997,876 kwa kulipia mishahara na stahiki mbali mbali za Wajumbe na Wafanyakazi wa Baraza na Shs. 3,763,522,141 kwa matumizi mengineyo (sawa na asilimia 76). Aidha, kwa upande wa kazi za maendeleo Ofisi iliingiziwa jumla ya Shs. 214,882,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (*UNDP*), na katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2011 – Machi 2012) ilitumia jumla ya Shs. 134,614,562 (sawa na asilimia 63).

Mhe. Spika**,** Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza liliweza kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Jumla ya Miswada 14 ya Sheria ilijadiliwa na kupitishwa na Baraza (**Kiambatanisho Nam. 6)**. Baraza lilijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

ii. Baraza liliendelea kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali kupitia Kamati zake na maswali ya Wajumbe.

iii. Kamati za Baraza zilifanya kazi za kuchunguza utekelezaji wa majukumu ya taasisi za Serikali na kuwasilisha Ripoti zao kwenye Mkutano wa Baraza uliofanyika kuanzia tarehe 28/03/2012 mpaka tarehe 20/04/2012.

iv. Pamoja na kazi za Kamati za Kudumu, Baraza liliunda Kamati Teule kufuatilia mambo yafuatayo:-

a) Uhaulishwaji wa Kiwanja cha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Mtoni, Zanzibar;

b) Matatizo ya Uwanja wa Ndege Zanzibar na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuhusu Ulipaji wa fidia kutokana na ujenzi wa uzio, ununuzi wa jenereta, ukodishwaji wa sehemu za biashara, na utaratibu wa ajira

c) Uvamizi wa fukwe na uharibifu wa mazingira kwenye Hoteli inayopakana na Chuo cha Maendeleo ya Utalii Maruhubi Unguja, Hoteli ya Zanzibar *Ocean View* Kilimani Unguja, na Hoteli ya Misali iliyoko Wesha, Pemba;

d) Uhaulishwaji wa Kiwanja kinachopakana na *Livingstone House,* Mbuyutaifa, Unguja;

e) Uhalali wa Mikataba ya Nyumba ya Serikali iliyopo Kiponda;

f) Matatizo ya ujenzi wa Jengo Jipya la Wizara ya Fedha, Pemba;

g) Ubadilishaji wa Matumizi ya *'Starehe Club'* na Jengo la Mambomsiige lililokuwa linatumiwa na Shirika la Meli Zanzibar, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali, na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Zanzibar;

h) Ukodishwaji wa Kisiwa cha Changuu; na

i) Usambazaji wa majenereta ya kusaidia huduma za usambazaji wa maji kwa mji wa Unguja wakati ilipotokea tatizo la kukatika kwa umeme mwishoni mwa mwaka 2009 na mwanzoni mwa mwaka 2011. Kamati iliwasilisha Ripoti yake kwenye kikao cha tarehe 18 April, 2012.

v. Jumla ya maswali 439 ya Wajumbe yalijibiwa na Mawaziri kwenye Baraza, katika mikutano minne ya Baraza kuanzia Julai 2011 mpaka Aprili 2012**.**

vi. Baraza lilipokea Kauli za Mawaziri kuhusu, Siku ya Mtoto wa Afrika; Kuzama kwa Meli ya MV Spice Islanders; Hitilafu za Kiufundi za Vyombo vya Baharini; Taarifa kuhusu Hoja ya Eneo la Bahari la Ukanda wa Kiuchumi (Exclusive Economic Zone (EEZ); Taarifa ya Mikopo ya Elimu ya Juu; na Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu wa Udhibiti na Uhifadhi wa Mali za

Kudumu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010; Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu wa Miradi ya Maendeleo na Miradi ya TASAF kwa Mwaka 2009/2010; pamoja na Ripoti ya Baraza la Manispaa ya Mji wa Zanzibar. Aidha, Baraza lilipokea Hoja za Wajumbe zifuatazo:-

a) Hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma kuhusu Mikopo ya Elimu ya Juu,

b) Hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuhusu Maombi ya Tanzania Umoja wa Mataifa ya kuongezwa eneo la *EEZ*,

c) Hoja ya Mhe. Hija Hassan Hija ya kuliomba Baraza liunde Kamati Teule kuchunguza madai ya kuwepo ukiukwaji wa majukumu ya Shirika la Umeme la Zanzibar (*ZECO*) **(Kiambatanisho Nam. 7).**

vii. Kuwapatia mafunzo Wajumbe kwa njia ya semina kuhusu uandishi wa kisheria, na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA II). Pia Watendaji wa Baraza (Makatibu wa Kamati) walipatiwa mafunzo kuhusu Utafiti wa Mabunge, na Utafiti wa Baraza kwenye Bunge la Kenya. Vile vile, Ofisi ya Baraza iliendesha Mafunzo kwa vijana kuhusu Siku ya Demokrasia Duniani**.**

viii. Jumla ya Wafanyakazi 21 wa Baraza walipatiwa mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi katika fani mbali mbali.

ix. Katika kuimarisha uhusiano wa kimataifa, Baraza liliendelea kushiriki kwenye mikutano na mafunzo ya Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Jumla ya Wajumbe saba (7) na watendaji watatu (3) walishiriki mikutano na mafunzo nchini Ungereza, Canada, India, na Zambia. Pia, Wajumbe 11 walishiriki Mikutano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyofanyika Nairobi, Kampala, na Bujumbura; Wajumbe wanne (4) walishiriki Mkutano wa Jumuiya ya Kamati za *PAC* za nchi za *SADC* chini Zimbabwe; Wajumbe wawili (2) na Afisa mmoja (1) alishiriki Mkutano Kuhusu Palestina, nchini Iran; Wajumbe watano (5) na Afisa mmoja (1) walishiriki ziara ya mafunzo kuhusu vitambulisho nchini Malaysia; na Wajumbe 33 na maafisa wawili walishiriki ziara ya mafunzo China kuhusu Maeneo Maalum ya Kiuchumi.

Mhe. Naibu Spika, Kwa upande mwingine, Afisi ya Spika ilipata heshima ya kutembelewa na wageni mbali mbali mashuhuri wa ndani na nje ya Tanzania. Miongoni mwa wageni hao ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza la Wawakilishi linakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

a) Kuyafanyia matengenezo majengo na vyombo vya usafiri vya Baraza
b) Kulipia huduma za afya kwa wajumbe na wafanyakazi.
c) Kulitangaza Baraza na shughuli zake kwa umma.
d) Kuendeleza uhusiano wa Kimataifa.
e) Kununua vifaa vya kazi za Ofisi.
f) Kuwapatia mafunzo wajumbe na watumishi wa Baraza.
g) Kufanya mikutano minne (4) ya Kawaida ya Baraza pamoja na kuendesha kazi za Kamati za Kudumu na Kamati Teule na Tume za Baraza.

Mhe. Naibu Spika, ili kutekeleza malengo hayo naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Shs. 12,380,186,000 kwa matumizi ya kawaida. Kati ya hizo Shs. 5,771,485,000 kwa malipo ya mishahara, stahiki nyengine za wajumbe na wafanyakazi na mchango wa *ZSSF* na Shs. 6,608,701,000 kwa matumizi mengineyo. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo Baraza limeidhinishiwa matumizi ya Shs. 605,424,000.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, kabla sijamalizia Hotuba yangu, napenda nikushukuru tena wewe binafsi kwa namna ulivyosimamia uwasilishaji wa taarifa ya Ofisi yetu. Aidha, nawashukuru wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa utulivu wao mkubwa katika kuisikiliza taarifa ya utekelezaji wa malengo ya mwaka 2011/2012 pamoja na mipango ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa namna anavyotuongoza, busara zake na maelekezo yake ambayo yamekuwa dira yetu katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii. Aidha, nawashukuru Katibu Mkuu, Dkt. Khalid Salum Mohamed; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Said Shaaban Said; Wakurugenzi; Afisa Mdhamini na wafanyakazi wote wa Ofisi yetu kwa mashirikiano yao makubwa wanayotupatia ambayo yamekuwa chachu ya mafanikio ya Ofisi yetu, na pia kwa kutusaidia kuiandaa hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa mashirikiano na michango ya Kamati za Baraza lako tukufu iliyopelekea utayarishaji wa Hotuba hii. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Washirika wa Maendeleo (*Development Partners*) na Nchi Marafiki kwa misaada yao katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Ofisi yetu katika kipindi cha mwaka 2010/2011, miongoni mwao ni: AL-Yousef Foundation, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *BADEA*, Clinton Foundation, China, Denmark, *FAO*, Finland, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, India, Japan, Marekani, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu, Malaria na UKIMWI, Oman, *UNAIDS*, *USAID*, *UNDP*, *UNICEF*, *UNFPA*, *WHO*, *WFP*, na *WIPO*. Vile vile, naishukuru sana Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mashirikiano ya karibu sana na Ofisi yetu. Pia nazishukuru Taasisi zisizo za Kiserikali kama ZAYEDESA, Jumuiya ya Wafanya biashara, Wenye Viwanda na Wakulima kwa kuendelea kuisaidia Serikali katika kutoa huduma za jamii na kuiletea maendeleo nchi yetu. Aidha, nawashukuru wananchi wote ambao wamefuatilia na kusikiliza Hotuba yetu hii.

Mhe. Naibu Spika, Baada ya maelezo hayo, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe Jumla ya Shs. 22,366,010,000 kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake (Tume ya Uchaguzi na Baraza la Wawakilishi) kwa matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo **(Kiambatanisho Nam. 8A na 8B)**. Mchanganuo halisi wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

- Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - 8,296,400,000
- Ofisi ya Baraza la Wawakilishi - 12,985,610,000
- Tume ya Uchaguzi - 1,084,000,000

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Naibu Spika: Sasa Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamuita Mwenyekiti, kusoma taarifa ya kamati, tumepata ugeni upo hapo juu tangu inasomwa hotuba mpaka hivi sasa. Naomba niwatambulishe ugeni huo.
Tunae Mhe. Balozi kutoka Norway Mhe. Hingun. Pia amefuatana na Afisa anayeshughulikia mambo ya siasa katika Ubalozi huo, Bibi Vesloni Lothe.

Baada ya utambulisho huo namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kusoma hotuba yao. Mhe Ali Salum Haji, kwa niaba ya Mwenyekiti.

Mhe. Ali Salum Haji: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kusoma ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, kwanza hatuna budi sote kwa pamoja kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa kwenye shughuli zetu, kwa ajili ya kujadili masuala muhimu ya kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Mwaka 2012/2013 kwa maslahi ya wananchi wetu na serikali kwa ujumla.

Pili, tunakushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kutupatia ruhusa ya kuwasilisha maoni ya kamati yetu mbele ya Baraza lako tukufu. Tatu tunatoa shukrani zetu za dhati kwa Makamo wa pili wa Rais, Waziri wake, pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano makubwa wanayotupatia wakati wote tunapokuwa katika shughuli zetu za Kamati.

Mhe. Naibu Spika, vile vile tunamshukuru Mhe. Rais wetu wa Zanzíbar kwa kuendelea kutuongoza kwa Amani na utulivu hapa Zanzíbar, na tunawaomba wananchi wetu wote kuiendeleza Amani ilyopo kwani ikipotea si rahisi kuipata tena.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda uniruhusu nimpongeze Mhe Marina Joseph Thomas kwa kuteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Bila shaka kuteuliwa kwake kunaoenesha imani kubwa aliyonayo Mhe. Rais juu ya uwezo na utendaji wa kazi wa Mheshimiwa Marina katika kusimamia majukumu ya serikali.
Mhe. Naibu Spika, pia, tunatoa shukrani zetu za dhati kwa wajumbe wote wa Baraza La Wawakilishi kwa mashirikiano makubwa tunayoyapata kutoka kwao na kuweza kufanikisha kazi zetu.

Mhe. Naibu Spika, shukrani zisizo na kifani ziwafikie wajumbe wangu wa Kamati yetu kwa mashirikiano makubwa wanyonipa wakati wote na ushauri wao pale wanapohisi tunakosea naomba niwashukuru kwa hilo na kwa kua tumebakisha mwaka mmoja kunamaliza muda wa uhai wa kamati zetu, basi naamini wataendelea kunipa mashirikiano makubwa kwani naamini wengi wao tutakuwa kwenye maeneo mengine ya kuzitumikia kamati mbali mbali kama Mheshimiwa Spika atakavyo elekeza. Kwa hiyo kwa ruhusa yako

Mhe. Naibu Spika naomba niwatambue wajumbe wangu wa Kamati yetu kama hivi ifuatavyo. ;-

1.	Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	-	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Ali Salum Haji	-	Mjumbe
4.	Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mohammed Haji Khalid	-	Mjumbe
6.	Mhe. Salma Mohammed Ali	-	Mjumbe
7.	Mhe. Ussi Jecha Simai	-	Mjumbe
8.	Ndg. Rahma Kombo Mgeni	-	Katibu
9.	Ndg. Ramadhan Kh. Masoud	-	Katibu

Mhe. Naibu Spika, baada ya dibaji hiyo sasa naomba nianze kutoa maoni ya kamati yetu kama hivi ifuatavyo;

HALI YA SIASA
Mhe. Naibu Spika, hali ya Siasa nchini kwetu hivi sasa pamoja ya kuwa ni shwari, lakini haiko salama sana kama Serikali haikuwa makini basi vurugu zinaweza kutokea tena kama ilvyojitokeza hivi karibuni. Kamati yangu haijafurahishwa na inalaani vurugu zilizotokea hivi karibuni, katika Mkoa wa Mjini Magharibi naMkoa wa Kaskazini, Unguja kwani umewatia tahruki wanachi wetu ambao walikwisha sahau hali ya vurugu zaidi ya mwaka wa tatu hivi sasa. Kwa hiyo kamati yangu inaomba Serikali kulifuatilia kwa makini suala hili na kutafuta chanzo chake na madhumuni yake ili kuwachukulia hatua wote waliohusika na uharibifu wa mali za Umma, lakini pia tunaiomba Serikali na nyinyi pia kujichunguza hasa Mawaziri muwe na kauli moja katika hili kwani tumeshuhudia hivi karibuni kwenye vyombo vya habari kuwa mkiwa na wananchi pembeni mnaongea vyengine na mkiwa Serikalini mnaongea vyengine na ni moja ya sababu iliyopelekea kutokea vurugu hizo.

Mhe Naibu Spika, sisi sote tulikula kiapo hapa Barazani na tunahitaji tumtendee haki Mwenyeezi Mungu kwa kuwatendea haki wananchi wetu.

Mhe Naibu Spika, kamati yangu inawapongeza wananchi wa Jimbo la Uzini kwa kutuletea Mwakilishi mahiri anaeipenda nchi yake Mheshimiwa Moh'd Raza na tunamuomba aendelee na moyo uleule wa kuwasaidia Wananchi wetu kama alivyokuwa hapo zamani. Tunamumbea kila la kheri katika majukumu yake mapya.
Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaungana na Serikali kuwaomba wananchi wetu kuendelea kuilinda na kuiendeleza amani iliyopo, hasa kwa kua tunategemea kuwa na Uchaguzi mdogo huko BUBUBU, kwa hiyo tunawaomba wananchi wetu kuutumia uchaguzi huo kwa kuimarisha mapenzi baina yetu na kuepusha chuki kwani sote ni kitu kimoja na sote tunatetea Maendeleo ya Nchi yetu.

MUUNGANO NA KATIBA MPYA

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inawashauri wananchi wote kuwa makini sana hasa wakati huu wa kutoa maoni ya katiba mpya, kwani katiba ndio msingi wa Taifa letu kwa hiyo huu ni wakati wa wananchi wetu kuzisoma katiba

zetu zote mbili na kujua mapungufu yaliopo ili kujua kile wanachokifanya wakati wa kutoa maoni yetu, lakini Mhe. Naibu Spika, kamati yangu imegundua kuwa Wazanzibari wengi hawaijui Katiba zote ikiwemo hiyo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa hali hiyo sijui tutegemee ni kipi watakachokuja kukichangia kwenye Tume ya Kukusanya Maoni Kuhusu Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Naibu Spika, tunaitaka Serikali pamoja kuwa tumeshachelewa kujipanga na kukaa pamoja na kuwauliza wananchi wote wa Zanzibar nini tatizo letu, tunahitaji nini na tufanye nini kwa maslahi ya Nchi yetu basi naamini tutaweza kuondoka na jawabu moja na tukiwaelekeza wananchi wetu naamini watatuelewa na watajua wanachokifanya, kwa hiyo kazi hiyo sio ya kuiachia Serikali peke yake, zaidi ni kazi yetu wajumbe wa Baraza la Wawakilishi sote kwani wao ndio waliotuleta hapa ili kulinda na kutetea maslahi yao, na kwa kua sisi kwa muda mrefu tumekuwa tukitumia hizi Katiba ikiwa ndio nyundo na majembe yetu katika kutekeleza majukumu yetu, basi ni lazima tuisaidie Serikali kutoa elimu majimboni mwetu.

Mhe. Naibu Spika, ninasema hivi kwa sababu kama alivyoelezea Mhe. Waziri, katika hotuba yake kuwa tayari wameshakaa katika vikao mbali mbali vya Makatibu Wakuu, Mawaziri na vikao kati ya Waziri Mkuu, Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar lakini bado matatizo yapo pale pale na yanaendelea kuwepo na yanaonekana hayatamalizika.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo muarubaini wa matatizo au Kero za Muungano wetu ni kuwa na katiba ambayo itakayobainisha na kuzitambua haki za kila upande wa Muungano huu na kutofautisha zipi zitashughulikiwa na kila nchi katika Muungano huu na zipi zitashughulikiwa na chombo cha Muungano hapo tunaamini hakuna nchi itakayo mlaumu mwenzie kama aidha ni mzigo au anaonewa na mwenziwe. Sio kama ilivyo hivi sasa kuwa kuna Mamlaka moja imebeba mambo ya kwake na ya Muungano ambapo mwingine anahisi kuwa kuna haki zake za msingi ananyimwa na mwenzake, na hii ndio inayopelekea kuwepo kwa manung'uniko ya kila siku kwa upande mmoja ambapo yamefikia kupachikwa jina na kuitwa kero za Muungano.

Mhe. Naibu Spika, kwa Mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Wizara za Muungano wa Jamhuri ya Tanzania ni chache mno, lakini kiuhalisia Mawaziri wote waliopo Tanzania Bara wanafanya kazi zao kama ni Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Sasa, je! Tujiulize, hii ndiyo sahihi? lakini ukiangalia katika katiba ya Jamhuri ya Muungano, kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Baraza letu la Wawakilishi kwa mujibu wa kifungu cha 64 cha katiba ya Muungano, mamlaka yetu yanaishia hapa hapa Zanzibar tu basi, tafsiri hiyo inabaki kuwa ni sahihi na tumekubali sisi wenyewe kwani tumeshiriki katika kupitisha hayo mambo ya Muungano kupitia wabunge wetu wa Zanzibar ambao tangu mwaka 1964, wanashiriki katika maamuzi makubwa ndani ya Muungano.

Kwa hiyo, kama wananchi na viongozi tunahisi mambo yalivyo kwa wakati huu sio sahihi basi ni lazima tuirekebishe katiba yetu hii na hivi sasa wananchi wako huru kuzungumza wanachokitaka, lakini kwa kufuata utaratibu na sheria za nchi zilizopo na hakuna wakati mwengine isipokuwa ni wakati huu wa kutoa maoni kuhusu katiba tunayoitaka itutawale hapa nchini petu, katiba ambayo kila Mtanzania atajivunia popote Duniani atapokwenda na kuiga mfano wetu.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaamini hayo yote yanawezekana ndani ya Muungano wetu bila ya hata kutengana, kwani huu ni Muungano wetu sote na sitegemei kama atatokea kiongozi atakaetaka kumdhulumu mwenziwe, kikubwa hapo kila mmoja ajenge hoja, itakayomridhisha mwenziwe.

Mhe. Naibu Spika, nawaomba sana wananchi wetu wa Zanzibar wajenge hoja zao kwa kurekebisha vifungu vilivyomo kwenye Katiba na kama kuna tofauti ya mawazo basi ni vyema watu wasipikiane majungu, sijui huyu Uamsho, huyu anabururwa na *CUF*, huyu anabururwa na CCM, haya yote hayatusaidii kwa hivi sasa na hili ndio tatizo letu Wazanzibari, kazi yetu ni kulalamika tu sio kujenga hoja zitakazoisaidia Nchi. Lakini na wao wajenge hoja zao ili kuonyesha namna wanavyohisi wao, kwa hiyo ni vyema kuisoma Katiba kama ilivyoandikwa na kwa sisi Zanzibar ni lazima kuzisoma katiba zetu zote mbili na baadae kuweza kujenga hoja zetu vinginevyo tutapotea.

Mhe. Naibu Spika, tatizo kubwa liliopo hapa kwetu ni kuwa wananchi wengi wanaisoma katiba ya Zanzibar pekee, bila ya kuiangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano na hufanya maamuzi yao kwa kutumia katiba moja tu, wakati hivi sasa tunasubiri kutoa maoni ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Ni lazima watu wetu hasa vijana tuwaelimishe vya kutosha.

HALI YA UCHUMI NA MIPANGO YA SERIKALI YA KUIMARISHA UCHUMI

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ameeleza mipango ya serikali ya kuimarisha uchumi wetu. Tunaipongeza Serikali kwa lengo la kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuja kuwekeza ili kutoa ajira kwa wananchi wetu lakini bado tunaiomba serikali kuwalinda vijana wetu katika suala la ajira kwa kupatiwa mikataba ya kazi. Pia kuna umuhimu wa kuwepo Sheria Maalum ya kuwalazimisha wawekezaji kuwa wanapowaajiri watu ni lazima pawepo na mikataba itakayosimamiwa na Chama cha wafanyakazi katika sekta husika, kwani hivi sasa serikali yetu imefanyakazi kubwa kukaribisha wawekezaji lakini tumeshindwa kuwalinda wananchi wetu kwani wawekezaji wengi huwaajiri wananchi wetu bila ya kuwa na mikataba ya ajira, kitu ambacho hupelekea kuwanyanyasa na kuwafukuza kila siku kama kuku kwani hawana kitu kinachowalinda.

UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI NA KUONGEZA FURSA ZA AJIRA

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inapongeza Serikali kwa kuendelea kutoa mikopo ya AK na JK na pia kutoa mikopo kwa vikundi vya ushirika na Sacos mbali mbali hapa Zanzíbar. Hata hivyo, bado kuna wananchi wengi hawajapata mikopo hiyo. Kamati yangu inashauri Serikali kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo. Aidha, kamati yetu inaona kuna haja kwa Serikali yetu kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Vijana ambayo itawezeshwa na Seriakali kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogowadogo pamoja na wakulima, kwani tumesikia kwa jirani zetu Tanzania bara, katika Bajeti ya mwaka huu wameweza kutenga pesa kwenye Bajeti Kuu na kuipa Tanzania *Investment Bank* ili kuiongezea nguvu waweze kutoa mikopo kwa wakulima na wajasiriamali wao. Pia serikali ijitahidi kuendelea kuutangaza Utalii, ili kuongeza pato la Taifa.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mipango yote hiyo kamati yangu inaitaka Serikali kuendelea na jitihada za taratibu za uchimbaji wa Mafuta na Gesi hapa Zanzibar kwani kama zilivyo Nchi nyingi mfano Oman, Urusi, uchumi wao mkubwa unaowaingizia mapato ni rasilimali ya Gesi ambapo inasaidia kuzalisha Umeme kwa bei ya chini, pamoja na kuuza nje ya Nchi. Tumeona Serikali yetu inavyochukua jitihada ya kuimarisha huduma za Umeme kwa kuweka waya mpya kupitia chini ya bahari lakini bado bei ya umeme ni Kubra, na kamati inaamini kuwa kwa kuwa umeme huo tunaununua nje ya Zanzíbar bei yake itaendelea kupanda na kuwabebesha gharama kubwa wananchi wetu.
Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa suluhisho la tatizo hilo, ni seriakli kujipanga ili ichimbe mafuta hasa ikizingatiwa kuwa taarifa za kitaalam zimetuthibitishia kuwa mafuta yapo Zanzibar.Sio hivyo tu, lakini pia Seriakli iendelee kupigania kuwa ZNZ itangazwe kuwa ni *SPECIAL ECONOMIC ZONE* ili kuweza kuwavutia wawekezaji wengi wa ndani na nje kuja kuwekeza nchini kwetu. Suala hili litaongeza ajira na mapato katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, tumeipokea kwa furaha kauli ya Serikali yetu kuahidi kuwa itashirikiana na sekta binafsi na pia kuzijengea uwezo sekta binafsi hasa za ndani ya Nchi ili kuziwezesha kutoa ajira zaidi kwa vijana wetu. Hata hivyo, kauli hii ya Serikali inatupa mashaka katika utekelezaji wake kwani tayari kuna baadhi ya Makampuni ya kizalendo ikwemo Kampuni ya *ZAT*, ambayo imekuwa ikifanya kazi katika kiwanja cha ndege hapa Zanzibar kwa muda mrefu, tangu kiwanja chetu hakijakuwa na huduma nyingi hadi hivi leo zimeimarika na Kampuni hii imetoa ajira kwa vijana wengi, na imetoa taaluma kwa vijana wengi katika masuala ya *Aviation*. Lakini kwa mshangao hivi sasa tunaambiwa kuwa zinatafutwa Kampuni nyengine eti nao kuja kufanyakazi ile ile, je suala hili sio kuona kuwa badala ya kuwapa moyo Kampuni hii, tunatafuta njia ya kuwanyima kazi? Kwa hiyo tunaiomba Serikali yetu kukaa na uongozi wa Kampuni hii na kuongelea ni mahitaji gani mapya yanahitajika ili na wao wajipange na sio kutafuta Kampuni nyengine.

Mhe. Naibu Spika, pia tunaipongeza Serikali yetu kwa kuendeleza Program yake ya kuutekeleza Mkuza 11 kupitia Klasta ya kwanza kwa kuendeleza miundombinu ya kiuchumi kama kuimarisha viwanja vya Ndege, Bara bara na Bandari n.k. Pia kuendeleza Klasta ya pili kuimarisha huduma za jamii ikiwemo Afya, Maji, Elimu n.k. Kwa kweli ni lazima tuisifu serikali yetu inajitahidi lakini kitu kikubwa tunawataka watendaji wetu bado baadhi yao wanaturejesha nyuma na hili lazima tuliseme na ikifika wizara zao tutawaambia wazi wazi bila ya kuficha kwani sasa ni wakati wa kwenda na sio kurudi nyuma.

Mhe. Naibu Spika, Klasta ya tatu ya Mkuza Serikali kuimarisha utawala bora hapa Serikali yetu inabidi kuipongeza kwani hivi sasa wananchi wamekua huru kutoa maoni yao hadharani na kuelekeza Serikali. Lakini pia tunaomba Serikali isiachilie baadhi ya watu kwa maslahi yao kutumia uhuru huo kwa kuvunja Amani na kutumia uhuru huo kwa kuingilia uhuru na kukashifu wenzao kwani hakuna uhuru usio na kikomo. Lakini bado suala moja katika kuutekeleza utawala bora. Kamati yangu imeona kuwa Serikali imekuwa kimya mmno na kwa watu wachache wanaokiuka maadili ya kazi zao, pamoja na ubadhirifu wa mali za Umma, katika eneo hili Serikali yetu iko kimya

sana, na kama haikuchukua hatua za dharura kukomesha jambo hili basi tutakuwa ni sawa kutwanga maji kinuni. Lakini alau tumeona kuwa kuna dalili ya kuyashughulikia ingawa kwa kasi ndogo, Lakini kiujumla tunapiga hatua.

Mhe. Naibu Spika, pia katika klasta hii ya utawala bora tunaipongeza jitihada za serikali za kujiandaa na kuimarisha Tume ya Uchaguzi kwa kuwapatia mafunzo, vitendea kazi, lakini jambo moja tumeshindwa kushuka kwa wananchi kuwapatia Elimu ya uraia, kwani wazanzibari wengi hawajui haki zao ikwemo kutokuijua Katiba yao, hili ni tatizo kubwa na hivi karibuni tuliambiwa na *UNDP* kuwa wanatoa pesa kwa Tume ya Uchaguzi ili kutoa elimu hiyo sasa wakati umefika kuifanya kazi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaipongeza Serikali kupitia ofisi ya Makamo wa II wa Rais kwa kuendelea kushirikiana na Baraza la Wawakilishi, lakini bado kuutekeleza Utawala Bora kwa vitendo Serikali haipaswi kuliendesha Baraza la Wawakilishi kwani hii ni mihimili mikubwa iliyo na nguvu sawa kikatiba na kila mmoja anatakiwa ajitegemee pamoja na Mahkama, lakini hadi leo serikali inaliongoza Baraza la Wawakilishi. Lakini tunamshukuru Mhe. Waziri kuwa nae hili analielewa, na hivi sasa kwa pamoja tunatafuta njia ya kulirekebisha hili, ili hii *cluster* ya tatu ikamilike kivitendo. Nadhani kabla ya kumalizika mwaka huu itakuja sheria hapa Barazani ya kulipa Baraza mamlaka yake kamili kwa kushirikiana na waziri, na tungelipenda sheria hiyo ikaletwa na serikali yenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nadhani wakati umefika Baraza lako kufuatilia migogoro ya ardhi iliyopo hapa Zanzibar, zaidi kwa maeneo ya uwekezaji ya serikali yaliyochukuliwa kiholela. *(Makofi)*

Vile vile *lease* za wawekezaji zilizofutwa kinyume cha sheria na kuikosesha serikali mapato ambayo yangeliisaidia serikali, pia na maeneo mengine ambayo na sisi tumeletewa malalamiko na wananchi. Kwa kifupi baadhi ya vielelezo hivyo tunavyo ambavyo na Mhe. Makamo wa Rais pia ameletewa.

Mhe. Naibu Spika, tatizo lililopo hivi sasa kuna baadhi ya maeneo kuna watu wamefutiwa hati, wakati tayari walikuwa wamo katika hatua ya kuyaendeleza, kwa hiyo katika eneo moja hilo mwenye hati mwengine na aliyejenga ni mwengine.

Isitoshe kuna baadhi ya *lease* za Wawekezaji zilifutwa na kupewa kampuni hewa, na maeneo hayo yakawa yananadiwa na madalali utadhani sio mali ya serikali, na kwa bei iliyokuwa ikinadiwa tunadhani yameuzwa kwa pesa nyingi tofauti zilizoingia serikalini, na tayari aliyenyang'anywa eneo hilo tayari amepeleka malamiko yake serikalini kupitia *ZIPA*.
Kwa kweli hili ni tatizo, na suala hili la migogoro ya ardhi hata Mhe Rais, amelitolea agizo litatuliwe, lakini kwa kuwa wengine wahusika ndio wao walioharibu hadi leo ni mwaka wa pili hawajayapatia ufumbuzi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, suala la Sensa ni muhimu kwani ndio linaloitambulisha serikali kujua idadi ya watu wake, ili kuweza kupanga mikakati ya maendeleo. Kwa hiyo, tunawaomba wananchi wetu wote kujitokeza kwa wingi, ili kuhesabiwa kwa faida ya maendeleo yetu sote.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Maafa tunawapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya kwa kutoa elimu ya maafa kupitia Kamati za Maafa za Wilaya, lakini katika zoezi linaloendelea hivi sasa la mgao wa kifuta machozi cha *Mv. Spice Islander*, tunawataka kujitahidi kuhakikisha ile orodha ya mwanzo waliopata kupitia kwa Masheha ndio iwe dira yao ya kulipa waliopatwa na mtihani huo, vinginevyo waliohusika wanaweza kuwaacha na kuwalipa watu wengine ambao wasiohusika.

Pamoja na hayo, kamati yangu inawataka idara kujenga jengo lao na kuacha kuendelea kukodi jengo, na kwa upande wa Pemba pia ni vyema wakaandaa utaratibu wa kuwa na jengo lao, pamoja na kuwa na ghala ya kuhifadhia vifaa vya kusaidia maafa pale yanapotokea.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inapongeza jitihada za serikali za kuendelea na matayarisho ya kuhamishia Idara ya Upigaji Chapa huko Maruhubi, tunaamini sasa wafanyakazi wetu watafarijika, kwani kwa muda mrefu wamekuwa kama sio taasisi ya serikali kutokana na mazingira magumu waliyokuwa wakifanyia kazi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaipongeza serikali kwa kushirikiana na *COSTECH* kwa kumuunga mkono kijana wetu aliyetengeneza Gari aina ya Sugu pamoja kutengeneza Puto. Kwa hivyo, tunaomba muzidi kuwa karibu naye na kumpa kila msaada, ili aweze kutimiza ndoto zake za kugundua vitu mbali mbali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika Idara hii ya Uratibu, tunaitaka pamoja na kuratibu Shughuli za Muungano. Vile vile ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa inajenga jego la kuwaenzi viongozi wetu waasisi, kwani hakuna taifa lisilokuwa na historia za viongozi wake waasisi, lakini serikali inaliona suala hili kuwa sio kipaumbele chake. Kwa hiyo, kamati yangu inaitaka serikali kuliangalia kwa upeo mkubwa, kwani lina umuhimu wake kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Faragha tunaitaka kuhakikisha kuwa inayaboresha majengo ya makaazi ya Makamo wa Pili wa Rais, yalioko Dodoma, na pia kujenga makaazi yake ya kudumu huko Pemba na Dar-es –Salaam, kwani kamati yangu hairidhiki na hali ya Makaazi anayokaa huko Dar-es-Salaam na kutokuwa na makaazi ya kudumu huko Pemba. Kwa hivyo, kuweka mikakati maalum ili kujenga majengo hayo.

Mhe. Naibu Spika, Waziri ametueleza kuwa idara imeratibu ziara 28 za ndani ya Zanzibar, 8 Tanzania Bara na 5 za nje ikiwemo ya China safari ambayo imeweza kutupatia kiasi ya shilingi karibu 12 bilioni. Sasa tunaomba ufafanuzi je pesa hizi ni ziada ya zile tulizozipitisha kwenye bajeti iliyopia, au ni miongoni mwa misaada tuliyoipitisha? Kama ni ziada mbona hatukupata maelezo yake kwenye Bajeti Kuu ya Seriakali?

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Utumishi haikutupa takwimu ya idadi ya ajira mpya na wala malengo ya mwaka huu, na pia mahitaji ya ofisi kwa watumishi ikiwa wanatosheleza kwa hivi sasa au la.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaipongeza Idara ya Mipango na Sera, kwa kuandaa Sheria ya Mfuko wa Jimbo na kuileta Barazani na kupitishwa na hivi sasa tumeanza kuitumia. Kwa hivyo, tunaishauri Idara kutoa Timu ya Wataalam kwenda Kenya, ili kwenda kujifunza ni namna gani wenzetu walivyopiga hatua kubwa za maendeleo kupitia Mfuko wa Jimbo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inaipongeza Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ kwa kuendelea kushughulikia Miradi ya *TASSAF*, na tunawaomba wananchi wetu hasa waliopata msaada kupitia Miradi ya *TASSAF* kuitunza miradi yao, ili na awamu nyingine waje kufaidika tena. Vile vile tunaomba Idara ya Vyama vya Ushirika kuifuatilia miradi hiyo, ili kutoa maelekezo kwa pale kwenye matatizo.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako, kwa kuniruhusu kuwasilisha ripoti yetu hii ya kamati yetu na tunawaomba wajumbe wote waichangie na baadae waiunge mkono, ili tumpe nafasi waziri kwenda kutekeleza haya aliyoyapanga. Mwisho kabisa tunawashukuru wajumbe wote kwa kunisikiliza.
Ahsante sana tunaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana kwa niaba ya Mwenyekiti. Sasa tunaendela na mjadala na mchangiaji wa mwanzo ni Mhe. Ismail Jussa Ladhu, akifuatiwa na Mhe. Asha Bakari Makame na baadaye Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tena kuianza wiki hii leo tukiwa hai na wazima, tukiwa tumepokea Bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii. Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba wa bajeti aliofanya asubuhi hii.

Mhe. Naibu Spika, bila ya kupoteza muda kwa sababu ninayo mambo mengi ambayo ninayotaka kuyazungumza. Kwa hivyo, naomba kabla ya kuingia kwenye maudhui ya kina yaliyokuwemo kwenye hotuba hii, basi niiombe Ofisi hii ya Makamo wa Pili wa Rais atakapokuja anisaidie maelezo kwenye buku kubwa la bajeti kuna baadhi ya vifungu vimenipa mashaka jinsi vilivyovimba ghafla kutoka mwaka jana hadi mwaka huu. Kwa hivyo, naomba hivi kidogo wakati atakapokuja anipe maelezo.

Jambo la kwanza liko kwenye Idara ya Uendeshaji na Utumishi, kwenye posho, vikao na kamati ambapo limetoka shilingi milioni 1 hadi milioni 10,390,000/= kwa mwaka huu. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anijibu kwa ujumla serikalini, kwa sababu Ofisi hii ndio inayoratibu Shughuli za Serikali.

Kwa kweli tumegundua kwenye buku hili katika maeneo mengi kwenye kifungu hiki cha posho za vikao na kamati, kuna bajeti yake kuongezeka mno kiasi cha kuitia mashaka, hasa tukizingatia kwamba mishahara imekuwa *consolidated*. Kwa hivyo, hatutegemei katika kazi za kawaida za serikali kwamba kuwe na posho za vikao, na kamati zilizokuwa zinavimba katika kila fungu la wizara mbali mbali. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie kwenye Idara hiyo hiyo kwenye fungu la gharama za mafuta na vilainisho, kwamba nalo limepanda mno kutoka shilingi milioni 10,500,000/= hadi milioni 48,480,000/= kwa mwaka huu, pamoja na kwamba najua mafuta yameongezeka bei lakini siamini kwamba yameongezeka bei kiasi hiki cha kupandisha fungu hili kutoka milioni 10 hadi milioni 48 kwa mwaka huu.

Mhe. Naibu Spika, katika Idara hiyo hiyo kwenye vifaa na huduma za ofisi nimeshtushwa na bajeti ya ununuzi wa magazeti na majarida kutoka shilingi milioni 2,150,000/= hadi milioni 8,820,000/= mwaka huu. Kwa kweli mpaka nikawa ninajiuliza Idara hii inanunua majarida na magazeti gani ambayo yanafika kiasi hiki cha fedha kwa muda wa mwaka mmoja?

Jambo la mwisho ambalo namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja anisaidie maelezo liko kwenye ukurasa wa 79 wa hili buku kubwa la mahesabu katika Fungu la Idara ya Maafa, ambapo kwenye malipo ya kujikimu na malazi bajeti yake imepanda kutoka shilingi 500,000/= mwaka jana hadi milioni 10,880,000/= mwaka huu.

Kwa hivyo, hayo namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika atakapokuja anisaidie, na kama nilivyosema kwamba ofisi hii ndio inayoratibu shughuli za serikali, basi namuomba anisaidie kwa jumla kwa sababu yatakuja kujitokeza mara kwa mara kama tutakavyokuja kuona kwenye wizara mbali mbali tutakapoziingia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo yanayohusu vifungu mbali mbali, naomba nizungumzie machache yanayohusu Ofisi ya Makamo wa Pili katika shughuli zake.

Jambo la kwanza linahusu wajibu wa Ofisi hii kwamba ndiye Msimamizi wa Shughuli za Serikali, na ndio maana kuna Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, na imefafanuliwa vyema kwenye kitabu kuanzia ukurasa wa 30 hadi 35. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hapa kidogo ninalo tatizo. Kwa kweli tatizo ni kwamba bado siridhiki na utendaji wa Wizara nyingi za serikali, na ziko zinazofanya vizuri na ukifika wakati wake tutazipongeza kwa kazi nzuri wanazozifanya. Lakini kama tutazigawa kwa wastani, basi nadhani nyingi haturidhiki na wananchi kwa jumla hawaridhiki na utendaji kuliko zile ambazo zinazofanya wajibu wake vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi nikilitizama hili naona ni kushindwa kuwajibika kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa sababu ndiye msimamizi wa wizara hizi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja atusaidie kuna nini, kwa nini shughuli za serikali tunaidhinisha fedha nyingi hapa, lakini tunapokuja kuangalia utendaji katika wizara nyingi kama nilivyosema hauridhishi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani kama kuna udhaifu fulani serikali ituambie, ili tuweze kuisaidia, ikiwa Idara hii ya Uratibu haifanyi kazi zake ipasavyo na inahitaji kuongezewa nguvu basi tuambiwe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, alipokuja madarakani *Tony Blair*, Waziri Mkuu wa Uingereza, mwaka 1997 nchi ilikuwa na matarajio makubwa sana ya mabadiliko, kama ambavyo matarajio waliyokuwa nayo wananchi wetu ilipokuja Serikali ya Umoja wa Kitaifa.
Kwa kulitambua hilo katika Ofisi ya Waziri Mkuu Tony Blair wakati ule aliweka Waziri Maalum aliyekuwa akiitwa *Cabinet Enforcer*, yaani Waziri wa Nchi katika Ofisi yake, jukumu lake ilikuwa ni kusimamia maamuzi ya Baraza la Mawaziri na jinsi utekelezaji wake utakavyofanywa katika serikali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya CUF tulikuja na pendekezo sisi, kwamba tungeongoza sisi serikali basi tungekuwa na kitu tunachokiita *Chief Inspector of Government Services*, yaani huyu angekuwa Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Utendaji wa Serikali. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Naibu Spika, tunayo Serikali ya Pamoja, ambayo ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Nadhani si vibaya kuangalia uzoefu kama huu, na kuongeza nguvu katika Ofisi hii, ili kuona ule uratibu unafanyika ipasavyo na wala sio uratibu tu kwa kufanya vikao visivyokwisha, lakini kuhakikisha unasukuma na kupeleka mbele utendaji na maamuzi ya serikali ambayo yanafanywa hasa yanayokuja katika Baraza hili.

Suala hilo naliomba sana Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kama nilivyosema kwamba tutamchosha Rais tukimfanya yeye ndiye awe Rais Mkuu wa Nchi, lakini pia akajitwika jukumu la kuwa ndiye Mkuu wa Usimamizi wa Shughuli za Serikali, na wala hili halipendezi Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine la jumla naomba pia niombe Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwamba ichunge na itazame sana serikali, kwa jumla kama ndio Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali juu ya watendaji wengi, wakiwemo watendaji wakubwa wa serikali ambao bado hawaonekani kuikubali kwa dhati dhana ya muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mfumo huu haukuletwa na mimi wala wewe Mhe. Naibu Spika, pamoja na kwamba ulikuwa ni mjumbe wa Kamati wakati ule iliyosimamia, lakini ulipelekwa kwa wananchi na walichagua kwa asilimia 66, yaani theluthi mbili za wapiga kura wa Zanzibar waliridhia kuja kwa mfumo huu. *(Makofi)*

Sasa kama kuna mtu ambaye hawezi kufanya kazi katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa, Mhe. Naibu Spika niiombe Ofisi ya Makamo wa Pili kwa heshima na taadhima imtake akae upande, ajuwe kwamba anapokwamisha shughuli hamkwamishi waziri fulani, isipokuwa anaikwamisha serikali na mwisho atakayekuja kuhukumiwa ni Rais ambaye ndiye mwenye ridhaa ya kuiongoza serikali hii. Kwa hivyo, hilo naliomba sana. *(Makofi)*

Kwa kweli ile kazi iliyofanywa na Rais Mstaafu Mhe. Amani Abeid Karume, na wakati ule akiwa Katibu Mkuu wa *CUF* Maalim Seif Sharif Hamad na hivi sasa ni Makamo wa Kwanza wa Rais, tuithamini kwa kuona kwamba tunalea mfumo ule na sio tunaufanyia hujuma kutoka ndani ya serikali yenyewe, na hili Mhe. Naibu Spika halikubaliki hata kidogo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye hotuba, kwanza nataka niungane na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kaka yangu Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, na pia Hotuba ya Maoni ya Kamati kwa kulaani vurugu na fujo ambazo zilitokezea hivi karibuni ambazo zinaathiri hali nzuri ya utengamano ambayo imefikiwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, sitaki kutaja nani ambaye amehusika kwa sababu mpaka leo sijui na kesi iko mahakamani, kwani kuna maneno mengi yanasemwa huko. Lakini yeyote aliyefanya nazilaani vurugu na fujo zile, na ninaomba wananchi wa Zanzibar wakatae kutumika kufanya vurugu, wakiwa vyovyote ikiwa ni wananchi wa kawaida, ikiwa wamo kwenye vyombo vya ulinzi, ikiwa wamo kwenye makundi maalum wanaotumika kwenye shughuli hizi, basi wote nawaomba wakatae kutumika na kuturejesha tulikotoka, kwa sababu tulikataa mfumo ule. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika hili pia nilikuwa na angalizo kwa Ofisi ya Makamo wa Pili. Kwa kweli ofisi hii inaongozwa na mtu mkubwa sana, isiwe wepesi mara nyengine kwa kusukumwa na baadhi ya mambo Mhe. Naibu Spika yanaleta taathira na hisia mbaya kwa wananchi. Kwa mfano, katika vurugu zilizotokezea, kwenye mambo mengi yaliyotokezea ni pamoja na hujuma tulizoambiwa za kuchomwa na kubomoa makanisa. Mimi binafsi nalaani yeyote aliyefanya shughuli hii, lakini jinsi serikali ilivyo-*react*, na hata Ofisi hii Mhe. Naibu Spika imeleta maswali mengi kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nakusudia nini? Ninachokusudia ni kwamba kwanza mara nyengine tunapotumbukiza matamshi ya kisiasa haraka, basi tunaweza kuathiri hata zile namna za kesi ambazo ziko mahakamani. Vile vile wananchi wanajiuliza kwamba kwa nini kunakuwa na *double standards*? Hakuna atakayefurahia kuchomwa makanisa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka kusema kwamba Zanzibar asitokee mtu nje ya Zanzibar kuja kutufundisha jinsi ya kuwa na uvumilivu wa kidini hapa, kwa sababu uvumilivu wa kidini umekuwepo hapa zaidi ya karne mbili. Kanisa la mwanzo Afrika ya Mashariki limejengwa Zanzibar, na siku zote tumeishi kwa salama na amani kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba asitokee mtu akatufundisha namna ya kuishi kwa pamoja, kwa uvumilivu, kwa sababu wanasema kuna watu inawezekana wana lengo maalum kulivuruga hilo. Lakini ninachosema Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ijihadhari na hili Mhe. Naibu Spika, kwa sababu gani nikasema hivyo, inajengeka dhana kwamba kuna watu wanapopatwa na matatizo, basi tunakuwa wepesi mno wa kwenda pale na kwenda kutoa matamshi ya kisiasa mazito.

Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari wanajiuliza kama kuchokoza hisia za dini ni jambo kubwa ambalo serikali hailipendi na sote hatulipendi, mbona palitokea kadhia hapa ya kuchomwa Msahafu na wala hatukuiona serikali iki-*react* kwa nguvu ile ile, na wala viongozi wa dini ya Kiislamu katika Zanzibar hawakutumia tukio lile kulifanya tukio kubwa la kisiasa na kujaribu kuhalalisha mambo mengine ambayo wanayoyataka kupitia mgongo wa serikali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mambo haya yanaonekana kama ni *double standards*. Kwa hivyo, nasema na nchi hii asilimia 99 ni Waislamu, kwa hiyo tungetegemea kama nguvu ingekuwepo na wala hatuzungumzi nguvu ielekezwe pahala pamoja, lakini tunachokitaka ni haki sawa kwa wote. *(Makofi)*

Sasa kama msingi ndio huo, basi Ofisi isikurupuke. Na hili lilitokea pia katika tukio la Pwani Mchangani Mhe. Naibu Spika, palitokezea athari pale ambapo pia tunailaani kwa sababu haikubaliki, lakini kuna vyombo vya habari kwa malengo yao fulani, wakajaribu kuionesha kama vile ilikuwa imelenga watu wa jamii fulani. *(Makofi)*

Lakini tafiti zilipokwenda kufanywa kumbe si kweli, na watu walikuwa wamechoshwa na biashara ile na wala hawakutizama watu fulani, ndio maana vibanda vilivyochomwa vilikuwa ni vya Wazanzibari na wasiokuwa Wazanzibari, lakini picha iliyojengeka kama vile imewalenga watu fulani.
Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema niiombe Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais katika hili wawe waangalifu, kwa sababu wanaweza kuja kumvunjia hadhi kiongozi mkubwa anayeongoza Ofisi hii, kwa sababu ya ushauri mbaya anaoupata kutoka kwa watendaji katika matukio kama haya. *(Makofi)*

Kwa hivyo, yanapotokea tunahitaji ku-*react,* lakini nasema isituchukulie tukenda katika hamasa kubwa na kupelekwa katika hisia ambazo wananchi wengine wakasema mbona yanapotukuta sisi Ofisi hii na serikali kwa jumla, hatuioni kuchukua hatua kama hizi na kuwaita Masheikh na kutafakari na kupewa maazimio kama ambavyo ilivyotokeza hivi karibuni? Mhe. Naibu Spika, naliomba sana suala hilo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa nizungumzie kuhusu suala zito la Muungano, na hili limeguswa katika ukurasa wa 5 mpaka 7 katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwamba siridhiki tena na maelezo yasiyokwisha kila mwaka kuja kuripotiwa kuhusu Kamati za Mashauriano baina ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Kiongozi huko nyuma na sasa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hizi zimekuwa kama ni ngonjera ambazo hazina tija yoyote kwa Wazanzibari. Kwa kweli wala tusidanganyane kwamba kunapatikana ufumbuzi na hakuna ufumbuzi Mhe. Naibu Spika. Kwa mfano, juzi tulizungumza hapa kwamba pamezungumzwa masuala kama vile ya kutozwa kodi mara mbili, viongozi wanatoa kauli kwamba limekwisha, lakini ukenda katika hali halisi lipo pale pale na mengi mengineyo na sitaki kutumia muda wangu Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ninayo mambo ya msingi ambayo nataka kuyazungumza katika suala la muungnao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ninachosema ni kwamba tutakaa vikao hata milioni, lakini masuala haya kwa utaratibu huu hayamaliziki. Kwanza vikao hivi haviko kikatiba, yaani havina nguvu ya kikatiba, ni vikao vya mashauriano tu. Pili, hivi kweli kwa utaratibu kama huu ndio tunamaliza matatizo ya muungano? *(Makofi)*
Mhe. Naibu Spika, katika hili Mhe. Mwanasheria Mkuu wetu ametusaidia sana kutambua kiini cha tatizo, na katika waraka wake maarufu “Maswali yasiyo na Majibu katika Muungano” na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walipata nakala ya kitabu hiki. Kwa hivyo, tunalishukuru Baraza la Katiba kwa kusaidia kutuletea

nakala ya kitabu hiki kwa Waheshimiwa Wawakilishi wote, chini ya *Professor* Abdul Sheriff, wamechapisha waraka ule Mhe. Naibu Spika naomba kunukuu kidogo.

Waraka wa "Maswali Yasiyo na Majibu katika Muungano" ukurasa wa 35 na 36 wa kitabu unaeleza hivi, Mhe. Mwanasheria Mkuu anasema, lakini wakati huo alipoandika waraka huu hakuwa Mwanasheria Mkuu:

"Sifa ya pili ni kuwa Muungano umekuwa na kitu kinachotambuliwa na kukubaliwa na wote, wale wanaoupenda na wasioupenda, kwamba una kasoro nyingi, na lugha ya siku hizi huitwa kero za muungano. Fedha, wataalamu, na muda mwingi umetumika katika kutafuta suluhisho la kasoro au kero hizo, lakini mafanikio yamekuwa madogo mno kama yapo. Wapo wanaosema kuwa kasoro au kero za muungano zimekuwa zikiongezeka badala ya kupungua. Wanaosema hivyo mimi nawaunga mkono. Naamini yeyote atakayetafakari kwa makini atawaunga mkono."
Hivyo, suala la msingi ni kwa nini kipenzi hiki cha taifa la Jamhuri ya Muungano kinachoitwa Muungano, ambacho sote tunakubali kuwa kinaumwa tokea uchanga wake hadi leo (na alipoandika *paper* hii ilikuwa) ni miaka 41 tokea kizaliwe (sasa ni miaka 48 tokea kizaliwe), kimeshindwa kupatiwa dawa pamoja na Watanzania kuwa na mabingwa wa dawa za kisiasa, pamoja na juhudi kubwa za mabingwa hao bado muungano unaumwa zaidi. *(Makofi)*

Wapo wanaodai kuwa dawa ipo na inajulikana, lakini pengine inaonekana ni chungu sana kupewa kipenzi hicho cha Watanzania. Ni maoni yangu kwamba muungano una kasoro za msingi za kimaumbile". *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, haya nasema mimi haya naomba tupige mstari hapo ni kwenye maoni yangu kwamba, muungano una kasoro za msingi za kimaumbile. *(Makofi)*
Anaendelea: "Kasoro hizo ni miongoni mwa sababu za muungano kuwa na kero sugu. Kasoro hizo za maumbile ni kuwepo kwa masuala ya msingi ya kikatiba ambayo hayana majibu, ama kutoka ndani ya Katiba, Sheria, Sera na hata kutoka kwa watendaji". Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimekinukuu hicho kwa sababu kinatoka kwa mtu mzito, na mimi ukiniuliza kama vile upande wa Tanganyika nikimtaja *Professor* Issa Shivji kama Mwanasheria aliyebobea katika masuala haya, basi kwa Zanzibar ningempa sifa hii Mhe. Othman Masoud, kwa nyaraka zake nyingi alizoandika katika suala la muungano. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa nini na katika waraka huu hajatufafanulia sana matatizo ya kimaumbile, lakini mimi nataka kuichukua hoja hii nielekeze zaidi Mhe. Naibu Spika.

Kwa mtazamo wangu Mhe. Naibu Spika, mimi kama Ismail Jussa Ladhu, matatizo ya kimaumbile ni kwa sababu walioandaa muungano huu hawakuwa Wazanzibari wala Watanganyika, isipokuwa walikuwa ni wageni maofisa wa Kiingereza, aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Tanganyika, ambaye alikuwa na asili ya Kiingereza Bwana Roland Brown na wengine wanamtaja pia bwana P.R.N. Fifoot ambaye alikuwa *Chief Parliamentary Draftsman* wa Tanganyika wakati ule.

Mhe. Naibu Spika, kuna ushahidi wa kihistoria wa maandiko mbali mbali kwamba, hawa katika kuandaa muundo wa ule muungano walikwenda kuangalia mahusiano ya Uingereza na Ireland ya Kaskazini, na hapo ndipo penye tatizo Mhe. Naibu Spika. Kwa kweli Ireland ya Kaskazini lilikuwa ni koloni la Uingereza na hili Mhe. Naibu Spika limethibitishwa na watu wengi, kwamba huo ndio uliokuwa mfumo. *(Makofi)*
Mhe. Naibu Spika, nikitaja kwa uchache kwa mfano ukisoma kitabu hiki maarufu tena ninacho hapa, Mhe. Naibu Spika naomba kunukuu kidogo "*We Must Run While They Walk: A Portrait of Africa's Julius Nyerere"* ukurasa wa 176 kinaonesha hiki kwamba aliyetumwa kwenda kuandaa kwa siri kama alivyokuwa akiagizwa na Mwalimu waraka huu ni Roland Brown.

Vile vile katika waraka maarufu wa marehemu Jaji Wolfgang Dourado, ambao umechapishwa hivi karibuni kwenye kitabu cha "*Zanzibar and the Union Question"* na waraka huu aliuandika mwaka 1983. Mhe. Naibu Spika, amethibitisha kwamba walioandaa waraka huu walikuwa ndio hawa mabwana wawili.

Lakini uthibitisho wa hilo la matatizo ya kimaumbile na mahusiano hayo umo katika nyaraka za siri za Marekani zilizokuwa zikiripoti yaliyokuwa yakitokea mwaka 1964. Balozi wa Marekani ambaye alikuwa Tanganyika anaarifu kwao Marekani, kwamba: *"The model agreed in principle was for The Tanganyika-Zanzibar Union to be like the relationship between Her Majesty's Government and Northern Ireland."*

Mhe. Naibu Spika, hata aliyekuwa Mshauri mmoja, ambaye ni muhimu sana wa Chama cha Afro-Shirazi *Professor* Thomas Frank kutoka Canada, amethibitisha kupitia kwenye kitabu cha "*Zanzibar: Background to the Revolution"* kilichoandikwa na Michael Lofchie, kwamba alipozungumza na waandalizi wa haya walimwambia kwamba mahusiano yaliyotizamwa yalikuwa ni ya Uingereza na Ireland ya Kaskazini.

Mhe. Naibu Spika, kwanza hili ni tusi kubwa kwa Wazanzibari, kwa sababu sisi hatujapata kuwa ni eneo lililotekwa na Tanganyika. Kwa hivyo, kwenda kuchukua mahusiano ya Uingereza na Ireland ya Kaskazini ukaja kutuundia sisi mahusiano ya nchi mbili huru zilizokuwa sawa zenye viti Umoja wa Mataifa tayari, yaani Tanganyika na Zanzibar, yalikuwa ni makosa ya kimsingi ya kimaumbile tokea mwanzo Mhe. Naibu Spika.

Pia naliona tatizo jengine la msingi katika muungano huu, kwamba hatutaweza kulitatua kwa Vikao vya Mashauriano, kwamba muungano huu haukuchukua kila kitu kikafanywa ni cha muungano. Mhe. Naibu Spika, Mkataba wa Muungano ni huu hapa ambao umetambua mambo 11 ya asilia, na leo yameongezeka kwa nambari 22, lakini ukiyanyambua yanafika 35. *(Makofi)*

Sasa ukisema kuna mambo ya muungano na ukayataja, maana yake yaliyokuwa sio hayo si mambo ya muungano. Lakini katika utekelezaji kwa sababu ya matatizo ya muundo huu, kuna tatizo Mhe. Naibu Spika,. tatizo liko wapi, ni kwamba moja katika yale mambo ya asili ni suala la Mambo ya Nje kuwa ni suala la Muungano. Kwa hivyo, hili kwa maoni yangu mimi ndio moja katika makosa makubwa sana tuliyofanya kuchukua Mambo ya Nje kuyaingiza katika Muungano. Kwa nini nasema hivyo Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, katika *International law* kuanzia mkataba wa *Westphalia*
kuja katika *Vienna Convention, Montevideo Convention* nchi inahisabika kuwa ni nchi ikiwa na sifa nne:

1) Iwe na eneo la jiografia linaloeleweka (*defined territory)*

2) Halafu iwe na watu wanaotambulika (defined population)

3) Iwe na serikali inayofanya kazi (functioning government)

4) Iwe na uwezo wa kuingia katika mahusiano na nchi za nje (Power to enter into foreign relations).

Tungelikuwa nalo hili sisi tungelikuwa ni nchi inayotambulikana ndani na nje ya mipaka yetu. Hayo matatu tunayo ya mwanzo tunayo tuna *defined territory*, tuna *defined population*, tuna *functioning government*, lakini tumekosa *Power to enter into foreign relations* kwa sababu tumeyachukua Mambo ya Nje tumeyatumbukiza katika mambo ya Muungano.

Sasa athari yake ni kwamba hata mambo yasiyokuwa ya muungano tukivuka mipaka ya Jamuhuri ya Muungano yanakuwa ya Muungano. Ndio maana michezo sio suala la Muungano lakini Zanzibar ikitaka kucheza katika World Cup iwe ni mwanachama wa FIFA iliambiwa huwezi kwa sababu wewe sio *Sovereign* State, sio mwanachama wetu.

Afya sio suala la Muungano lakini Zanzibar haiwezi kwenda *WHO* Shirika la Afya la Dunia kama mwanachama kamili. Elimu sio suala la Muungano lakini Zanzibar haiwezi kwenda kwenye *UNICEF*, ikasema kwamba nataka kuwa mwanachama wa *UNICEF* kwa sababu inaambiwa sio nchi kamili inayotambulikana.

Lakini hata karibuni Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2004 nadhani hapa tulikataa usafiri wa baharini kuwa ni suala la Muungano, Baraza hili hili mimi nilikuwa sijaingia, ilikuwa katika semina kina Mhe. Shamuhuna, kina Mhe. Haji Omar Kheir, kina Mhe. Abubakar walikuwa wakali kweli kweli. Wakazuia na wakaikataa sheria ile ya *Merchant Shipping Act* ya muungano ikatungwa *Maritime Transport Act* ya Zanzibar. Baada ya kufanya maamuzi yale, tulipokwenda katika uwanja wa kimataifa wa Zanzibar imeweza kuwa mwanachama wa Shirika la Usafiri Baharini Duniani (*IMO*) *International Maritime Organisation*? Hatukuweza pamoja na jitihada zote kwa sababu sisi hatutambuliki kimataifa. Mfano wa mwisho ninaotaka kuzungumza katika hili ni suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Jumuiya ya Afrika Mashariki Mhe. Naibu Spika, ina mambo 17 kama sio kwa kuokoa muda ningeliyasoma, yanayosimamiwa na Jumuiya hiyo. Katika hayo 17, ni manne tu ndiyo kwa Tanzania ni mambo ya Muungano, 13 sio mambo ya muungano. Kwa mujibu wa Mkataba wa Muungano na kwa mujibu wa Katiba ya Muungano

iliyokuwepo hivi sasa Serikali ya Muungano haina Mamlaka ya kusimamia mambo yasiyokuwa ya Muungano juu ya Zanzibar. Ndio kusema haina mamlaka ya kusimamia wala kuisemea Zanzibar katika mambo haya. Lakini kwa sababu sisi hatutambuliki kimataifa hatuna uwezo wa kuingia mahusiano ya nchi za nje katika Afrika Mashariki tunawakilishwa na Jamuhuri ya Muungano kwa mambo yasiyokuwa ya muungano wanatukandamiza.

Mhe. Naibu Spika, hoja yangu ilikuwa ni kwamba kwa sababu ya kuchukua mambo ya nje kuyaingiza katika mambo ya muungano tumefanya kosa kubwa sana la kujinyima mamlaka ya kutambulikana kama ni dola ndani na nje ya mipaka ya Zanzibar na ya Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, lakini si hayo tu matatizo ya muungano wetu yapo pia katika kukiukwa huo mkataba wenyewe wa muungano juu ya matatizo yake yote uliyokuwa nayo, sitaki kuyazungumza hapa, yameshaandikwa mengi naamini watu watayatizama.

Mhe. Naibu Spika, tunafanya nini? Umekuja mchakato wa Katiba mimi niungane na wote waliosema na nawapongeza wote waliobadilisha misimamo yao kwamba sasa wamekubali kwamba sasa Wazanzibari twende tukatoe maoni yetu. Na mimi niwaombe Wazanzibari katika hili tukenda tukazungumze kwa kauli moja. Tukenda kwa misingi ya vyama tutaivuruga Zanzibar, tukenda kwa jumuiya zilizokuwa na misimamo yao, tutaivuruga Zanzibar. Ni lazima turatibu na tukawambie Wazanzibar nini madai yetu katika mchakato huu.

Katika hili mimi nataka kuiomba sana serikali yetu sana, naipenda sana Serikali ya Umoja wa Kitaifa katika waliotoa mchango mkubwa kuileta mmoja ni mie. Wengine kila mmoja alitoa mchango wake lakini hata Wajumbe wa Baraza lililopita, lituongoze katika hili.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba tatizo lilikuwepo kwa sababu tumechukua mambo ya nje tukapeleka kule na hilo litaendelea kuwepo hata tukibadilisha idadi ya serikali. Katika hili ili lifahamike naomba tena nimalizie nina nukuu mbili nataka nizisome ni muhimu sana, nimnukuu tena Mhe. Mwanasheria Mkuu wetu katika *paper* yake hii maarufu. Kwa sababu ya muda nitaisoma sehemu ndogo tu. Anasema katika ukurasa wa 51.

> "Niliyoyaeleza ni mifano tu ya masuala hayo mengi. Kinachojidhihirisha ni kuwa tatizo sio la idadi ya Serikali tu lakini ni zaidi ya hapo. Tatizo la msingi ni lile la Kanuni za Msingi za Muungano kutozingatiwa na kutopatiwa majibu. Kutokana na kasoro hizo ndio maana muungano wetu kama ulivyo hivi sasa hauwezi kuhimili mabadiliko ya kisiasa. Hakuna Muungano madhubuti ambao unategemea kulindwa na sera za chama. Muungano madhubuti ni ule unaolindwa na misingi madhubuti, uwazi na wenye majibu kwa masuali yanayohusu nguzo kuu za Muungano huo."

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema limekuja wazo naomba Wazanzibari walizingatie. Kwanza nisema moja mimi siamini kwamba Zanzibar ina sababu ya kukataa mahusiano yote na Tanganyika. Hilo haliwezekani Mhe. Naibu Spika. Hata tukiwa tunajitosheleza kwa kila kitu lakini kihistoria Zanzibar kwa hapa ilipo ilivyoumbwa na Mungu ikawekwa imekuwa inaogopwa. Hata wakati wa kutoa uhuru Mhe. Naibu Spika, ninazo nyaraka za Waingereza wakati wana mazungumzo ya kuelekea katika uhuru hapa walikuwa wanasema humu kwamba wao hawana maslahi yoyote katika suala la kuiachia Zanzibar kupata uhuru wake. Lakini hofu yao, *policy* yao, sera yao ni kile wanachokiita *Strategic Denial* kwamba Zanzibar isije ikaangukia katika mikono ya Dola khasim dhidi ya dola za Magharibi. Na hii haikuwa *concern* ya Waingereza tu leo ni *concern* hata ya nchi zilizo jirani zetu hapa.

Kwa hivyo tunahitaji kuwa na mahusiano ili kuondosha hiyo khofu kwamba Zanzibar inaweza ikatumika ikaharibu usalama wa nchi nyengine. Hofu hiyo lakini si lazima iwe gharama ya kuibinya Zanzibar, kuikaba roho na kuifanya isiweze kupata pumzi.

Mhe. Naibu Spika, katika dunia ya leo kuna mfumo mzuri sana, mfumo wa muungano wa mkataba. Mifumo ya Muungano wa Mkataba imekuwa na nguvu kwa sababu inakwenda na ridhaa ya waliyoungana. Ninachokusudia kwamba tuwe na serikali mbili ya Tanganyika na ya Zanzibar kila moja ikiwa na mamlaka yake kamili ndani na nje ya nchi. Halafu serikali hizi ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar nayo Jamhuri ya Watu wa Tanganyika ziingie katika mahusiano kupitia Mkataba kama walivyokuwa Umoja wa Ulaya.

Lakini pia tutajifunza kwa wenzetu wamefanya makosa wapi ili na sisi tusiyarejee hayo. Naamini Mhe. Naibu Spika, tukifika hapo Zanzibar itarejesha, itakuwa na kiti chake Umoja wa Mataifa, itakuwa mwanachama wa

Jumuiya ya Madola, itakuwa mwanachama wa Umoja wa Afrika, itakuwa mwanachama wa Afrika Mshariki na itaweza kusimamia haki zake zote kabisa.

Mhe. Naibu Spika, hili kulisema hivi nisitafsirike kwamba ni maradhi au ni kosa kwa Wazanzibari. Mmoja katika waasisi wa Muungano huu, Mwalimu Julius Nyerere anaeleza katika kitabu hichi ambacho yeye mwenyewe kakibariki katika utangulizi alikikubali kwa sababu kilikuwa na *record* sahihi ya mahojiano yake na mwandishi wa Kimarekani William Edgett Smith alichokiandika hichi. "*We Must Run While They Walk: A Portrait of Africa's Julius Nyerere"*

Anasema katika ukurasa wa 185 katika kitabu hichi chapa ya mwaka 1971. Anasema Mhe. Naibu Spika: ''*The people of Africa are more sacred then those boundaries*. *I have two bits of a union. Even if Zanzibaris are not rejected by Tanganyika if they simply felt the union was of no use to them and broke away and this was the genuine feeling of the Zanzibaris I could not possibly kill Zanzibaris, If they came in freely they can leave freely, We did not conquer Zanzibar and if they remain it must be of their own free choice"*

Naomba nitafsiri halafu nikae kitako Mhe. Naibu Spika. Anasema kwamba 'Watu wa Afrika ni muhimu zaidi kuliko mipaka iliyokuwa imeachwa. Na yeye ana mitazamo ya aina mbili kuhusu muungano. Hata ikiwa Zanzibar hawatakataliwa na Watanganyika ikiwa wao wenyewe tu wataona muungano hauna maslahi nao tena na wakaamua kujitoa na ikiwa hayo ndiyo matakwa halisi ya Wazanzibari, mimi sitoweza kuwaua Wazanzibari. Ikiwa walijiunga kwa hiyari na kwa uhuru, wana haki ya kujiondoa kwa hiyari na kwa uhuru.Sisi hatukuiteka Zanzibar na ikiwa watabakia (yaani katika Muungano) wanapaswa wabakie kwa uhuru wao na kwa hiyari yao.

Kwa hivyo hii ni nukuu Mhe. Naibu Spika, ni muhimu kwa wale wote ambao wanadhani kwamba muungano huu ni wa Tanganyika na Zanzibar ni mgeni mualikwa tu. Tuna haki sawa sawa, tuna kauli sawa sawa katika kuamua hatima ya muungano huu.

Nimalizie Mhe. Naibu Spika, nawaomba Wazanzibari, tutulie, tuende katika Tume ya Katiba tukasema kwa kauli moja tunachokitaka, tuirejeshee Zanzibar mamlaka yake ya kitaifa na ya Kimataifa halafu tukae kwa mashirikiano na Jamhuri ya Tanganyika chini ya Muungano wa Mkataba.
Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kutuamsha katika hali ya afya njema, kwa mintarafu ya kupanga mambo ya nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze sana Makamo wa Pili wa Rais, Waziri wake, watendaji wake, kwa jinsi walivyokipanga kitabu hiki cha bajeti katika mtiririko ambao ukilinganisha kipindi cha mwaka uliopita na mwaka huu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakuja suala la mwanzo nyeti la ardhi. Katika kitabu hiki kumeandikwa hapa mgogoro wa ardhi. Mimi nashukuru kwamba Serikali Kuu imetambua kwamba kuna mgogoro wa ardhi. Lakini sikufarahi kwa sababu ardhi katika mambo matatu ukishakuyakusanya, lakini na ardhi ni muhimu imezungumziwa hata *page* moja haikufika.

Naiomba Serikali Kuu na Wizara husika na hasa nina imani sana na Waziri aliyeteuliwa kwa kipindi hichi, ifanye tathmini ya mikoa yote mitano ya Unguja na Pemba. Kwa kila Wilaya, kwa kila Mkoa kwa kila Jimbo ili kuhakikisha ardhi yetu imefikia kiwango gani, na nini na nini tunakitaka na kitu gani tukifanye vipi. Suala hili Mhe. Naibu Spika, hii sijui mara ya ngapi nalizungumza. Naiomba Serikali tena kwa heshima kubwa. Kwa sababu naiyona ardhi haina mwenyewe, tunasema kwamba ardhi ni mali ya serikali, lakini mimi nathubutu kusema kwenye Baraza hili kwamba ardhi haina wenyewe. Ni kwa sababu zangu.

Mhe. Naibu Spika, nimelipigia kelele suala hili, kwanza wananchi wanakosa imani na serikali yao kuhusu suala la ardhi. Naiomba sana serikali, hebu tuache tuliyonayo tujaribu kuhakikisha ardhi yetu matakwa yetu ni kitu gani na gani. Hichi ni kisiwa Mhe. Naibu Spika, ni tofauti na nchi nyengine tukifanya mchezo hapa badala ya kusema Kisiwapanza kinadidimia, tutadidimia kisiwa kizima cha Zanzibar.

Namuomba sana, Makamo wa Pili wa Rais, kwa sababu yeye ndiye mtendaji Mkuu katika serikali hii. Tulizungumza suala hili hapa tukasema Mombasa pamevamiwa, tukazungumza kwa hamasa tukamwambia Makamo wa Pili aende, akenda. Matokeo yake hakuna chochote kilichotokezea pale, watu wamezidi kujishauwa na kujenga, sasa wamejenga nyumba za kuishi. Serikali iko wapi? Na tulizungumza kwenye Baraza hili tukufu. Wananchi Mhe. Naibu Spika, wametokwa na imani kuhusu suala la ardhi.

Naomba sana, tena hii narejea sijui mara ngapi, naomba kwa kweli tuwe *serious* na mambo mengine. Serikali nakusudia Serikali Kuu yenyewe itathmini, imeambiwa humu kwamba watachukuliwa hatua na nini na nini. Wallahi hakuna mtu atakayechukuliwa hatua. Kwa sababu kuna mambo mengine yapo wazi tumeyazungumza humu nani kachukuliwa hatua. Mimi naomba kuna baadhi ya mambo tuwe *serious* na mambo yetu. Tunayabeza mambo mpaka dakika ya mwisho yanatushinda kuyachukulia hatua. Suala hilo moja la ardhi, kwa sababu wananchi wana haki zao.

Mfano kama mimi nimekuja kumkuta mama yangu au baba yangu karithi ardhi za mababu zake, najua kwamba ardhi ni mali ya serikali, lakini na mimi niliyerithi nina haki. Leo utamkuta mtu kiwanja kimoja kimeuzwa na watu wane, watano, wanapasiana tu, kwa sababu ardhi haina mwenyewe. Naomba sana tuwarudishie matumaini wananchi kwa serikali yao. Mimi nakwambieni sisi ndio tunaotembea huko, tunayaona mambo na ndio tunaoshtakiwa. Wananchi wametokwa na matumaini juu ya serikali kuhusiana na habari ya ardhi. Tuambizane ukweli.

Mhe. Naibu Spika, mpaka makaburi jamani jinsi tulivyotokwa na imani. Makaburi tunayachukua tunayajenga. Watu wa vijijini wametengewa sehemu zao na wazee wao kwamba hapa mtazikana. Leo anatoka mtu na ubabe wake na kujifanya yeye ndiye anakwenda anavunja anawasulubu. Tumeona kwenye televisheni watu, tunaomba jamani. Kwanza serikali iweke kila sehemu kwamba hapa patazikiwa watu. Iweke kila sehemu kwamba hapa mfano Mkoa wa Kaskazini Pemba kule Mtambwe kutawekwa 1, 2, 3, 4 ambavyo sehemu zinazohitajiwa na wananchi. Tupange mipango yetu kwa mintarafu ya wajibu wa mambo yetu tunayoyataka katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, mimi Muungano siuzungumzi kwa sababu nimeshazungumza kipindi kilichopita. Lakini nataka kuwaomba Waheshimiwa Wakilishi wa CCM na *CUF*, nchi hii wananchi wanatutizama sisi. Nchi hii ipo katika mikono yetu wanachama wa Chama cha Mapinduzi na wa *CUF*, vyama vyengine hapa havitawali. Nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wa vyama viwili, kwa sababu sisi ndio tuliohodhi madaraka ya Zanzibar, hakuna mwengine hakuna CHADEMA wala nani hapa. Wananchi wana matumaini makubwa kwetu, na wamejenga imani katika serikali yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa, kwamba tutawaweka pahala pazuri. Namuomba Makamo wa Pili wa Rais, ni imani yangu kwamba kuna wengine hata hawafahamu mfumo wa Umoja wa Kitaifa.

Namuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais atufanyie semina Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa wenzetu ambao wametembelea na wanajua, akina Mhe. Ali Mzee yumo, Mhe. Haji Omar Kheir alikuwemo, Mhe. Naibu Spika, wewe mwenyewe ulikuwemo, Mheshimiwa ambaye sasa hivi hayupo si mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Abubakar ambaye yeye ndiye alikuwa akikereketwa sana. Sasa hawa watupe semina tena sio semina ya siku moja watuelimishe maana gani ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Naona kati yetu hatuelewi, ndio maana ikawa tunalumbana baadhi ya mambo ambayo hayana sababu.

Naomba sana Makamo wa Pili wa Rais. Na kila chama kielimishe wanachama wake nini mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Hilo naliomba lifanyiwe kazi kwa sababu sisi ndio wenye dhamana ya wananchi wa Taifa hili la Zanzibar. Ndio maana nikasema siuzungumzi Muungano, kwa sababu muungano nimeshauzungumza. Nauzungumza Muungano wa Wazanzibari wenyewe. Imani yangu kwamba hapa ilipotoka asilimia 60 kwamba watu wanataka serikali ya Umoja wa Kitaifa bado magurupu yapo, mtu anamtizama Asha Bakari. Asha Bakari alitaka Serikali ya Umoja wa Kitaifa ngoja tumkomoe. Hamumkomoi Asha Bakari, mnaikomoa nchi yenu. Niseme hapa katika muungano nazungumzia *another way*.

Mhe. Naibu Spika, niipongeze sana Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa suala la serikali. Serikali haidaiwi katika Zanzibar Leo, na niipongeze, lakini pia nitoe ushauri kuhusu gazeti letu la Zanzibar Leo. Kwanza niwapongeze sana vijana ambao wanafanya kazi katika gazeti letu hili. Mwanzo walifanya kazi kwa mazingira magumu, tunakwenda tunazungumza nao, lakini baadaye kwa kweli pamoja na mazingira magumu baadaye wakafanya kazi nzuri. Nawapongeza sana kwa moyo wao wa uzalendo walionao.

Naiomba Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, mlitupie jicho la huruma hili gazeti. Badala ya kuchapishwa Bara jamani lisichapishwe Bara, lichapishwe hapa hapa Zanzibar. Naiomba sana Serikali. Gharama tunazozipata na uzuri

wenyewe likitoka tu Zanzibar limeshafika. Ni watoto hawa wanafanya kazi ya ujasiri kwa kweli. Hili suala hili lifanyiwe hapa hapa, kwa sababu nitagusia hapo katika uchapaji pia maana yake linakwenda sambamba.

Niipongeze Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwamba suala la Kiwanda cha Uchapaji lilikuwa ni la miaka mingi tokea miye sijakuwa Naibu Waziri mpaka nikawa Naibu Waziri, fedha nyingi sana Serikali ilipoteza. Nichukue nafasi hii serikali niipongeze Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, jinsi kelele zetu zilivyosaidia humu na kuona kwamba kuna haja sasa hivi ya kuwa na sehemu ambayo ya kuhakikisha kwamba mambo yetu yasitoke nje, maana siri zetu zote zilikuwa nje jamani. Tunachukua vitabu tunavichapisha wapi, *madude* gani tunayachapisha wapi ya siri siri, hebu tuache mambo haya tuhakikishe kwamba kiwanda chetu tunakifanyia kazi.

Niipongeze Serikali kuona kwamba imefanya nini, imewapatia eneo ambalo watawajibika vizuri katika shughuli zao. Pia niipongeze pamoja na matatizo waliyonayo, na hawa na wao wanastahili kupongezwa kwa jinsi wanavyofanya kazi zao.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala zima la vikosi vya SMZ katika uchumi wa karafuu. Ni lazima tukubali kwamba vikosi hivi vilifanya kazi katika mazingira magumu na hakuna asiyejua. Uzuri wenyewe mmesifiwa humu mamilioni na mabilioni ya fedha zilizopatikana. Namuomba Mhe. Waziri aje anieleze ni kiasi gani ambacho vikosi hivi walisaidiwa wakati walipokuwa kazini. Maana kuna malalamiko kwamba katika miezi mitano waliyofanya kazi ni Sh. 50/- tu mtu kapewa. Namuomba afanye aje anieleze vikosi hivi vimesaidiwa kiasi gani. Kwa sababu wao ndio waliolinda karafuu zikaweza kupatikana. Tukifanya mambo shoti mengine tuyaangalie.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Mfuko wa Jimbo. Naipongeza sana Serikali imesaidia sana wajumbe wetu wa Baraza la Wawakilishi ambao wenye majimbo, lakini nitaiomba Serikali Kuu, wanawake na wao wanafanya kazi ngumu vile vile. Mwanamke yeye hana jimbo, kuna wa Kitaifa kuna wa Mkoa, anapochangia yeye hachangii kwenye jimbo anachangia Mkoa Mzima, na wa Kitaifa anachangia Taifa zima kutoka Zanzibar hadi Bara, kwa sababu jumuia ni ya watu wote. Naiomba sana Serikali Kuu hatuombi kama hizo walizopewa wenzetu wa jimbo, angalau kwa sababu mwanamke ndiye muwajibikaji mkuu katika familia na katika mambo ya kuleta maendeleo, na yeye aonewe huruma huyu mwanamke. Ili itiwe na yeye japo si Mfuko wa Jimbo lakini mtajua nyie wataalamu namna gani ya kuweza kuhakikisha kwamba na wanawake wawakilishi na wao wanapatiwa fedha za kuwasaidia katika shughuli zao za akina mama.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika Baraza la Wawakilishi. Kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze Katibu wetu aliyepita ndugu Ibrahim jinsi alivyofanya kazi na sisi na kwa mashirikiano makubwa. Lakini pia nichukue nafasi hii nimpongeze Katibu wetu ambaye tunae sasa, pia nimpongeze Katibu Msaidizi ambaye aliyeondoka ambaye sasa hivi ni Naibu Katibu Mkuu katika Wizara ya Mambo ya Sheria. Kabla sijazungumza ninayoyataka kwanza niwapongeze. Niwapongeze wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi. Wafanyakazi hawa hawana wakati, wafanyakazi hawa wanajitolea, wafanyakazi hawa wanafanyakazi katika mazingira magumu. Kuanzia Maofisa, Makatibu Wasaidizi, mpaka wahudumu.

Hapa nitoe pongezi kidogo maana yake tembo ukilisifu mgema hulitia maji. Kuhusu usafi, toka tulipozungumza huyo aliyewekwa akaongoza suala la usafi nampongeza anasimamia kidogo ipasavyo, azidishe bidii bado usafi wa vyoo na baadhi ya mambo azidishe bidii, nimesema hiyo niwashukuru.

Nakuja katika Baraza la Wawakilishi. Mhe. Naibu Spika, kuna mihimili mitatu mmoja ukiwa ni huu Baraza la Wawakilishi. Kwa mfumo tulionao sasa, Baraza la Wawakilishi halina muhimili hata mmoja unaojihimili, ni kama Idara nathubutu kusema. Naomba Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa sababu yeye ndio limo Baraza la Wawakilishi kwenye hotuba yake, na yeye ndiye bosi wetu. Hili suala bajeti inayokuja lisiwemo tena, iwe ni muhimili ambao unajihimili wenyewe kwa mujibu wa taratibu na sheria. Sasa hivi kila tunachotaka tuombe kama Idara. Hatuwezi tukatumia na tulikubaliana kama mnakumbuka wajumbe wenzangu kwamba Wizara ya Fedha, lakini itabidi tubadilishe baadhi ya mambo ya Katiba na taratibu, tulisema itutengee kima maalum kama wenzetu Wabunge kiingie katika mkusanyo wa mapato kila mwezi. Lakini kutokana na mfumo uliobadilika kwamba tupo katika Utawala Bora mambo yale yamefuia kama embe iliyopigwa na mafua.

Naomba sana Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, namuomba Mhe. Waziri pamoja na Mwenyewe mtendaji Mkuu wa Serikali, suala hili tuliweke pahala pale kwa mujibu wa katiba inavyosema.

Mhe. Naibu Spika, kuna baadhiya mambo mengine huwa tunayapitisha humu kwenye Baraza la Wawakilishi lakini matokeo yake hatua za kisheria huwa hazichukuliwi. Naomba Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kila pahala tulipopatungia sheria, basi sheria ichukue mkondo wake. Si hivyo mambo yetu yatakwenda shaghala baghala, sitaki nizungumze mengi. Sisi tunapitia sehemu mbali mbali, ukiwemo wewe mwenyewe Mhe. Naibu Spika, wewe ni Mwenyekiti wa Kamati, Kamati tunaona mambo mengine ni aibu kwa Serikali, sitaki mengine niyataje maana itakuwa ni aibu. Tukijaribu kusema kwamba huyu ni mtoto wa shangazi na mjomba, huyu ni rafiki huyu ni nani, serikali hii haitofika pahala. Kuwa ni kuondoa mihali linalotufikisha mahali pabaya Mhe. Naibu Spika, ni kuwa na muhali, hebu muhali tuuondoe ili tuendoshe mambo yetu vizuri.

Mhe. Naibu Spika, ukishakuona uso wa Asha Bakari haah yule mtu wa zamani, kasaidia Serikali hii. Achana na kusaidia, mchukulie hatua inayofaa kwa mujibu wa taratibu kama kaisaidia ndio aibomoe Serikali. Hapa mimi natoa indhari Mhe. Naibu Spika. Mie huwa nasemwa sana, mie katika nchi hii kwanza siogopi chochote kwa makamo haya niyofika, tokea nilipoanza uongozi najua jema nalijua baya najua nifanye nini. Kwa hiyo siogopi isipokuwa mwenyewe Mwenyezi Mungu tu, na simtimizii yote huyo Mungu.

Mimi kwa mujibu ninavyoona kichwa changu kinavyonielekeza kwamba, hili ni la maslahi ya nchi mtu nataka aniseme mpaka anifukie. Tena nimeshasema awe CCM au CUF, tunataka kujenga nchi katika Serikali ya Mfumo wa Umoja wa Kitaifa na ndio maana nikasema tutolewe mafunzo. Kwa hivyo mie hapa nilipo nangojea siku yangu Mungu akinijaalia, kwa hivyo mtu akisema akifanyaje, mimi sim- *mind* na-*mind*, uzalendo nilionao katika nchi yangu. Kama mtu si mzalendo ni mnafiki basi ujue mnafiki yeye huyo. Lakini kama ni mzalendo kweli ni lazima utaitakia mema nchi yako. Kusema ukweli siku zote ukisema kweli ndio unaonekana mbaya. Mimi mtu na anione mbaya, lakini sitokuwa mnafiki katika nchi yangu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais *mia fil mia*.

(Saa 7:00 Mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii jioni ya leo kuweza kuchangia hotuba ya bajeti ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nitoe pongezi za dhati kabisa kwa Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri sana yenye muelekeo mzuri wa usimamizi ya Wizara zake hapa Zanzibar. Lakini Mhe. Naibu Spika, kabla sijaendelea kusema kwanza, naomba nitoe fikra zangu kama ni Mwakilishi wa wananchi hiyo ambayo itaweza kutusaidia katika matayarisho ya safari yetu ya mbele.

Kwanza ninaomba kumwambia Mheshmiwa wangu Makamo wa Pili nimeona katika kulala kwangu na fikra zangu kuwa Zanzibar sasa hivi iko haja ya kuweza kuundwa Wizara ya Vikosi peke yake. Mhe. Naibu Spika, hilo ni jambo la msingi na lina maendeleo na tutawawekea heshima hawa askari wetu, wakiwa na wizara yao basi ninaamini sasa hivi watakuwa askari wetu wa vikosi na wao watajengeka heshima. Lakini sasa hivi tunakwenda kuwatia katika tawala, kwa kweli Mhe. Naibu Spika, hatuwajengei heshima ile ya kiaskari na huko tunakokwenda hatujui vipi huko Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo jambo lolote tunaweza tukaji-*prepare* mapema tukawa na Wizara yetu *special* hiyo inayohusiana na askari wetu Wizara maalum ya vikosi. Fikira yangu hiyo nimeona kwanza niitoe.

Mhe. Naibu Spika, lakini niende katika kuchangia sasa ukurasa wa 12 migogoro ya ardhi Zanzibar. Mheshimiwa Makamu wa Pili mwanzo ulikuja vizuri sana na mimi nikasema nipo nitakusaidia kazi. Mhe. Naibu Spika, watu wa Zanzibar walikuwa na matumaini mazuri sana na wenigne wakawa wanapiga kofi lakini japo kofi nyengine zilikuwa hazilii, lakini zilikuwa katika *action* ya kupiga kofi, Mheshimiwa ulifika pahali ukaogopa. Mhe. Naibu Spika, hiyo ni moja ambayo Wazanzibari wengi walifika pahali wakaweka shingo upande kama nilivyoweka shingo upande mimi mchangiaji wao leo kutokana na hali hiyo.
Mhe. Naibu Spika, bado migogoro iko mingi sana ya ardhi na hasa wanaonyanyaswa ni wananchi wetu wa Zanzibari. Mhe. Naibu Spika, Migogoro hiyo ina *face* mbili. Ina *face* ya kwanza ya *investor* wananyanyaswa katika nchi yetu hilo kweli tuseme, hawana ulinzi wa kutosha, mtu akishafutiwa *land lease* yake basi ndio *is okay*

ameshapoteza mabilion ya fedha yake tena *foreigner* anakuja kununua ardhi kwa mwananchi halafu baadae anakuja kufutiwa *land lease* bila kutoa *notice* indhari na *official letters* Mheshimiwa tunakwenda wapi. Mheshimiwa mnakwenda nje kutafuta *investor* mnawaleta hapa itakuwa sawasawa tunawarubuni mimi nitasema mnawarubuni wakija hapa tunashindwa mwananchi ananufaika ananunua ardhi yake kwa bei anayotaka mlivyotoa fursa, akitoka pale yule anakwenda kutafuta pesa nchi za nje ili kuja kuwekeza, sasa akiwekeza ananufaika nani? Tunaonufaika ni sisi wananchi wa Zanzibari ambao leo walala hoi wengi hawana ajira. Ndio maana nikasema tufike pahali tuseme ukweli tusifichane.

Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki ninakinukuu "Serikali haitowavumilia viongozi na watendaji wanaojihusisha na kusababisha migogoro ya ardhi nchini hatua za kisheria zitachukuliwa ikiwa pamoja na kuwafukuza kazi". Je, tuko tayari. Kifungu hichi Mhe. Makamu wa pili uko tayari kukitumia kifungu hiki? Uthibitisho tunao, kamati zenu zimeundwa kwa mujibu wa kanuni. Na tunapokwenda kufanya kazi tunafuata Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano na kanuni inavyotuelekeza ya Baraza.

Mhe. Naibu Spika, hiki kifungu sijui ilikuwaje hata mkakitia mimi nashangaa kweli Mheshimiwa kifungu hiki ni hatari si kitu cha mchezo. Kwa sababu tunayo hayo mabomu kabisa tunayo nimekuja na *briefcase* nzima. Mhe. Naibu Spika, nimeshasema mara nyingi sana, lakini nikishamaliza ninaonekana kama nimekaa hapa Khadija Kopa nimetoa hadithi mchezo umekwisha ndio kawaida yetu tunavyofanya. Mhe. Naibu Spika, naomba hichi kifungu kifanye kazi. Na mimi sitouiunga mkono hotuba hii kama sijasikia bomba kesho wahusika wote wameshafukuzwa kwa kifungu hiki kabisa wenyewe kitabu hiki wala mimi Mshimba sikutoa kwenye kichwa changu wenyewe kitabu hiki kifungu hiki kimo. Leo ukija kule Buyu watu wananyanganywa ardhi, wananchi wa Buyu kila leo wanapelekwa Mahkamani jamani kura zetu hizo tunaziadhibu wenyewe? Maana yake mambo mengine tufikirie safari yetu tunayokwenda huko kwenye *challenge* kubwa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, suala hilo ambalo mimi nimeliona *investor* Zanzibar sasa hivi watafika pahali watatusema vibaya sana, watatu-*notice* vibaya sana. Mimi nikisema Mheshimiwa *wallahi* hukaa nikalia nikisikia bango kitita mnakwenda kumpelekea Mhe.Rais tunamdanganya tena tunamdanganya.

Mheshimiwa Makamo nitakupa kazi moja leo hii, nenda katika maabara ya saratani ya kutoa nyama kuchunguza *cancer* kuna vifaa feki nenda kavitizame kesho uje kunambia Mshimba kweli au uongo, watu washakula pesa. Maana yake leo hebu jiulize Mheshimiwa Makamo tangu vifaa hivi vije nchini mpaka leo hii kwa nini visifanye kazi, basi hamujiulizi vile vitu havikutimia *sio complete* bwana, havikutimia kabisa watu wanaendelea kwenda zao *ocean road* tunakosa mapato sisi halafu *still* mtu huyo anaomba pesa amaliziwe mawe, pesa hizi hatukubali. Mheshimiwa huyu mtu atueleze si utani kabisa.

Ndio mimi nikasema kwa Rais, siku moja nilimuuliza kaka yangu hapa Dokta Mwinyi, mwalimu wangu nilimuuliza swali vizuri na akanijibu kwa fasaha sana akasema ala inawezekana mtu atajiuzulu akigundulikana sasa nione tayari bomu hilo wajiuzulu watu tuone. *Wallahi* Mhe. Jakaya Kikwete mimi nashangaa sijui tuna *difference* gani Bunge na Baraza la Wawakilishi, hujiuliza hebu mwanasheria nisaidie. Wanatunga sheria na sisi tunatunga sheria, tofauti wao wana Katiba ya Muungano sisi tuna Katiba ya Zanzibar. Lakini sijui tuna tofauti gani katika maamuzi. Karibuni tu Mheshimiwa alilipangua vibaya vibaya baraza la mawaziri, na alilipangua kuanzia Waziri, Naibu na Makatibu wake aliwatoa.

Sisi tunapiga kelele kila leo ardhi wee ardhi wee tunakwenda kule kwa Rais tunamwambia tuna mpango hivi fulani mara hii *vision* 2020 tuna hivi na hivi masikini ya Mungu wakiondoka pale, mimi ningemuomba Mhe. Rais siku wanapokuja na bango kitita Wizara anapoziita pale pale awastopishe halafu atoke ende *visit* yenyewe akaangalie nini atakachokikuta kwa yale yaliyozungumzwa pale. Mhe. Naibu Spika, Baraza lako tukufu Makamo wa pili tunangojea watu wajiuzulu mara hii *otherwise* bajeti ngumu hizi.

Mhe. Naibu Spika: Zungumza na kiti,

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante naelekea huku huku Mhe. Naibu Spika. Sasa hiyo Mhe. Naibu Spika, ndio lengo ambalo tunalisema kuwa migogoro kila siku tunaieleza lakini haiishi. Leo mtu *lease* ya dola 13,000 U.S. inakwenda kufutwa anapewa mtu akalipe dola 3,000 hatujapoteza uchumi. Lakini mtu yule yule anapewa mtu *special agent* anakwenda kuyauza maeneo yale ukipiga *total* hapa, watu wamenufaika mabilioni ya fedha leo walala hoi masikini ya Mungu wafanyakazi mshahara wao wa laki mbili, laki moja hawaongezeki. Kuna wengine

hawapewi *allowances* zao humo hospitalini, wengine wanashindwa kupewa pesa za likizo kumbe fedha zinakwenda kwa watu binafsi. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli inanisikitisha sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuendelea mimi namuomba Mhe. Waziri anambie *total* wale ndugu zetu walemavu ukurasa wa 14 wangapi wameajiriwa katika Serikali hii na ikiwa kidogo kwa sababu gani na wao wana haki yao nataka nijuwe kabisa, kwa sababu kila siku tunawaeleza hawa ndugu zetu na wao katika jamii lakini utakuta hatuwatendei haki. Kwa hivyo naomba anipe *total* kabisa katika Serikali hii imewaajiri watu wenye ulemavu sawa sawa kama sisi watu tuliokuwa wazima aniletee taarifa hiyo.

Mhe. Ukurasa wa 15 dawa za kulevya, Mhe. Naibu Spika, kuna kitu kinaitwa *Sober House*. Mhe. Naibu Spika, kuna mama mmoja nimemsahau kwa jina ameanzisha kitengo hiki na leo nimeona hapa *paragraph* hii Mhe. Naibu Spika, tufanyeni haraka ziko fedha nyingi tu. Tuwaokoe hawa ndugu zetu kwa kutafuta eneo la kuweza kujenga *special* nyumba hizo, wenzetu Bara washatupiga teke jamani wameshaanza wao tayari na wao wamekuja kusoma kwetu lakini la kuchekesha tayari wao wameshaanza, naomba sana Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze sana huyu mama aliyeanzisha *Sober House* tena ninampa hongera kubwa sana, kafanya jambo la msingi la kuwasaidia vijana wetu kuondokana na tatizo hilo la dawa za kulevya. Wengine sasa hivi wanaelezwa vizuri wamekuwa walimu wa kuwasomesha wale wenzao ambao bado wanaendelea kula madawa ya kulevya.

Mhe. Naibu Spika, haraka sana zitafutwe ardhi tutafute wafadhili, fedha hizo zinazoibiwa ibiwa tuzikamate zirejeshwe ili ziweze kujengwa hizo nyumba zao za kuweza kuishi, wawe na kituo maalum ili cha kuweza kukatazana masuala haya ambayo hayana msingi. Mhe. Naibu Spika, hilo ninaliomba sana.

Mhe. Spika, nakwenda ukurasa wa 30 Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali shughuli za muungano, Mhe. Naibu Spika, hapo ndio safari yangu. Mhe. Naibu Spika, juzi nimemsikia Mheshimiwa Waziri, Afisi ya Makamo wa Pili ameeleza maelezo mazuri sana na alikubali kama makoseo yapo, mimi ninachompendea hapo. Ukifika pahali sema ukweli wala usifiche. Watetezi wa haki sisi tupo wa kukusaidieni. Mhe. Naibu Spika, leo nilipofika niliunguza macho sana kuisoma Katiba hii. Nakubaliana Katiba hii ina mapungufu makubwa sana na hasa kwa upande wa Zanzibar. Mwanasheria atanisaidia kama nasema uongo, Katiba hii muundo wake ni mwepesi sana haujaeleza muundo hasa wazanzibari tutafanya kazi vipi katika muungano ni hii hapa kama ninasema uongo na anibishie. Tena ni sehemu chache tu ni ndogo sana Mhe. Naibu Spika. Lakini ukurasa wa 128 kuna suala la gesi asilia, kuna asilia masuala ya mafuta, sasa Mhe. Naibu Spika, hapo ndipo ninapopataka mimi.

Unaambiwa ukigusa Katiba utashtakiwa mhaini unavunja Katiba lakini Mhe. Naibu Spika, ninataka vipi hebu jamani tufike pahali tuseme ukweli, tusiogope tunajua hofu yetu wawakilishi wenzangu mimi nitakuwa sirudi pengine kama sikusema hivyo unapata dhambi kwa Mungu. Kwa sababu hutetei haki, yule unayemdai kwa mujibu wa sheria wanavyuoni wapo unaambiwa ukikataa hukumdai unapata dhambi wewe kwa sababu haki yako unajinyonga wewe mwenyewe na hivyo ndivyo inavyotakiwa tufike pahali tusiogope kuwatetea wananchi wetu wa Zanzibar kwa kuwa nini hutopata uwakilishi, aaa kwani wewe umezaliwa nao uwakilishi, mimi sikuzaliwa nao wala sikupewa tarehe kwamba ukitoka duniani Mshimba utapewa uwakilishi sikuambiwa hivyo. Lakini imefika pahali nimesoma nimetambua, sasa nataka niwaelimishe na wale wenzangu waliolala usingizi tutetee haki yetu kwenye Muungano wetu tulipwe haki zetu.

Mhe. Naibu Spika, wengine wanasema huko aaa bora Muungano ukatike mimi sisemi ukatike kwa sababu mimi nadai haki yangu niipate kwanza najua nikidai wewe utanuna. Lakini ninachotaka mimi tukae kitako tupewe haki yetu na nimesema jamani, kama sheria ipo tuonjosheni kidogo mtupeleke kule tukachukue na *wallah* tutarudi na pesa zetu sisi. Kwa sababu vitu vimo kwenye Katiba sisemi mimi. Mhe. Naibu Spika, maisha yote ukiwa mdhaifu basi watu watakupumbaza pumbaza, lakini ukiwa madhubuti hupumbazwi ng'o. Sisi sasa hivi si dhaifu tena ndio maana tunadai haki yetu kwenye Muungano.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi nilipokuwa katika Kamati ya Katiba na Sheria shahidi wangu mzee Ali hapa lakini hayupo kasha ondoka, tulipofika kule kwenye Wizara ya Mambo ya ndani tukadai visakina *escot* ya Zanzibar ilikuwa inasukumwa nimeiona kwa macho yangu lile gari kubwa tulipofika kule tukadai jioni yake tunapigiwa simu visakina vitatu vimeletwa vipya na ndio haki yetu kweli mpaka tukadai hivyo? Sasa Mhe. Naibu Spika, angalia hivi leo goma zima lile pale.

Mhe. Makamo wa pili angalia boma letu njia mbovu, nyumba mbovu tangu za Said Khalifa isitoshe mtu anakwenda unamuona yule anakwenda chooni, tunawatendea haki kweli Mhe. Naibu Spika, usiku asiwashe taa. Mtu anakwenda *long distance* kwenda chooni ni mwanamke tena ana mume basi sisi tumelala tu.

Mhe. Naibu Spika, naomba ufanye ziara kwa makusudi nenda katika bomani ukaone hali halisi utalia machozi. Wenzetu kule Chang'ombe wamejengewa nyumba za ghorofa za kisasa zina familia mbili mpaka tatu *of course* kitu kama hiki. Halafu leo mtu ukae hapa upige kofi *paa* uondoke usiwatetee watu, usiseme kama unatuonea jamani tutakuwa hatuwatendei haki.
Mhe. Naibu Spika, hili tulione kwa makini sana tusifanye masikhara muungano wetu tunautaka lakini Mhe. Naibu Spika, hatuwezi kuukataa waturejeshee pesa zetu. Kuna *TRA* kuna masuala mengine, kuna bilioni kumi na nane wewe mwenyewe umekiri bilioni kumi na nane sasa hata hizi zinashindwa kupatikana, nitieni kwenye boti, Mhe. Makamo usione utani nitieni kwenye boti nipeleke nina uchungu wa Zanzibar haki yetu inanyimwa watoto wanakosa skuli kusoma tupelekeni haki yetu wenyewe kwanini tunagopa kuisema, kwa kuwa mtaniweka kwenye maadili *never* hakuna tatizo lolote, nimeshajitolea nitakwenda kupiga makongwe kwetu nitalima mihogo nitalima lakini kwa suala hili sitoliacha Mhe. Naibu Spika.

Tupelekeni waheshimiwa tutakuleteeni pesa zenu hapa, lazima tawatetea wazanzibari haki yao kwenye muungano. Wenzetu wanaanza kufanya *study* kuchimba mafuta kuyatafuta, wenzetu sasa hivi trilioni ya pesa za gesi wameshazipata. Leo niambie Mhe. Makamo kuna ofisi inayohusiana na masuala ya pesa hizo tena zidai sasa. Mheshimiwa naomba Waziri unambie akaunti yako imetiliwa pesa ngapi za gesi si hivyo lah hii siipitishi. Unambie mimi hapa Mhe. Mshimba unamjibu kwa maelezo mazuri tu akaunti yangu katika pesa za Muungano za gesi asilia nina trilioni na mimi, hapo mimi nitakupitishia bajeti yako lakini hivi hivi tu tutachoka. Wenzetu wanakwenda maeneo kila leo kule nenda Dar es Salaam *half London* sisi tukizipata hizo pesa kidogo 4.5 tu tutageuka Dubai hapa ninaamini hiyo wala hatutopiga kelele. Watu watapata mishahara mizuri, havitonunuliwa vitu feki lakini hatuzipati kwa wakati.

Sasa naomba mimi ninakuamini sana Mheshimiwa wangu Waziri ninakuomba sana katika mawaziri umo na wewe ninaokupendeni mnaofanya kazi vizuri. Sasa na hili uje kunijibu kabisa, nina watu wangu wanne watano najua hilo ni jeshi la kuotea mbali. Ninaamini ukija hapa utanambia akaunti yako inasema hivi, mgao wa gesi kutoka Jamhuri ya Muungano Katiba inaeleza una asilimia kadhaa mimi nitaridhika.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kwa kuendelea kumaliza Kamati teule hapa iliamua, mimi niseme kitu kimoja siku moja mimi nilipokuwa ninasafiri nilimkuta Waziri wangu *wallah* siku ile watu walipokwisha kupiga makombora makubwa Waziri alifatilia haki ya Mungu ninakwambieni. Lakini katika kitabu chake hakusema tu jamani ee hapa ndipo ninapolaumu mimi hamna humu sijui misingi yake ikoje. Kwa sababu tunasikia kisiri siri eneo la Mtoni alilochukua Muekezaji lisharejeshwa, hakusema humu hebu kama kweli njoo unambie kama kweli lisharejeshwa na utuoneshe hasa kweli limerejeshwa.

Na kama limerejeshwa wapeni watu wa UUB wapate kuekea zana zao warejeshee wenyewe na masuala mengine mengine lakini humu Mheshimiwa hakutoa ripoti zake la Mtoni la Mawasiliano lililorejeshwa la Bakhresa nasikia karejesha toba sikio lakini nasikia kitu hicho kimefanyika. Sasa kama kimefanyika tupeni *official* sasa hapa kama kweli tuone ukweli wa Serikali yetu kama alivyosema Mhe. Asha inafanya kazi ya utekelezaji.

Lakini siku hiyo nilimuona anatoka jasho anahangaika uwanja wa ndege kutafuta yale yaliyosemwa humu, mwengine sijamuona la hasha. Lakini pale nimemuona kweli Mhe. Naibu Spika, anahangaika Mheshimiwa Waziri wetu, lakini humu hakuandika simlaumu au sijui kama kompyuta kama imerusha vipi sijui, imo hiyo inawezekana pengine imeruka.

Mhe. Naibu Spika, lakini niseme kuhusu habari ya yule mzee niliyekuwa nikimtetea, tulisema kamati yule mzee alipwe milioni ishirini, lakini nayo vile vile haimo humu Mhe. Naibu Spika kuonesha yule mzee kama keshalipwa ama vipi. Lakini ninasikia mpaka leo hajalipwa sasa tumesema kuwa kama hajapewa pesa zake yule mzee basi haki kwanza isitolewe, alipwe pesa zake halafu tena haki itoke.

Lakini Mhe. Spika, nikirudi tena hapo hapo kwa kumalizia askari wetu sasa hivi wanakatwa pesa hawa Polisi pesa za kufiwa. Mheshimiwa hii mimi namba Mhe. Makamo wa Pili aichukuwe isiwe lazima, anayetaka ndie achangie. Lakini wanasikitika sana wanasema pesa hizi ukizitaka wewe ushafiwa ulishie ndio uzipate ndio zake mwenyewe.

Kwa hivyo mimi naomba Mhe. Naibu Spika, hebu wateteeni wanyonge wetu, kuwafanya hichi kitu kama si cha lazima na kama cha lazima walikuwa na kiwango cha milioni moja wanapewa askari wetu lakini sasa wanapewa laki tano. Sasa na hii naomba chini ya Wizara yako Mheshimiwa wewe ndio wa Muungano mratibu wa Muungano lifatilieni hili suala tuwasaidie wanyonge wetu. Mtu haki yako mwenyewe ukaitafute kwa rushwa.

Lakini namalizia Mhe. Naibu Spika, sasa hivi tuna Polisi Jamii na siku zote ninaisema hii, lakini Polisi Jamii hii sijakusikieni kauli yenu kui-*support* kama nyinyi hapo waratibu mnasimia masuala ya Muungano. Polisi Jamii Mheshimiwa sasa hivi inatenda haki vizuri sana. Polisi jamii imezuia mambo mengi sana nimshukuru sana Kamishna wa Polisi Zanzibar kwa kuunda kikosi hicho cha Polisi Jamii akiongozwa na amiri jeshi wake IGP.

Mhe. Naibu Spika, ni kitu kizuri sana tuseme ukweli hapa na pale, lakini kinakosa *support* ndani ya Serikali ya Zanzibar. Kwa maana hiyo sasa Mheshimiwa ichukuwe kwenye Wizara yako, wanafanya kazi ya hatari wale. Wanafanya kazi *without* sheria tuwalindeni tuwatengezeeni sheria ili iweze kuwalinda na kuwepo na fungu maalum la kuwatekelezea kazi kwa sababu wale wanapambana ana kwa ana na wahalifu. Leo mimi sijasikia tamko rasmi la Serikali kusema leo tunaipokea Polisi Jamii na tunawapongeza waundaji, mimi hiyo sijaisikia. Mhe. Waziri ninakuomba sana sana hiki kitu ukifatilie kwa makini.

Mhe. Naibu Spika, na mimi ninahitimisha sasa, hitimisho langu Mheshimiwa namalizia na Katiba yangu kama nilivyosema nimejitolea kabisa kuitetea Katiba hii kwa kupata maslahi yetu ya Wazanzibari, naomba sana Mheshimiwa. Katika hayo marekebisho Wazanzibari tuendelee kufanya marekebisho lakini huku tunadai haki yetu tulipwe wenyewe, ili tuweze kukwamuka katika umaskini na sisi vile vile tukajitambua tunakula haki ya tunda hili Mheshimiwa. Tusinune twende tukatoe maoni yetu tusende na chuki tupambane kabisa ili haki yetu tuipate kwa mujibu wa sheria ya Katiba hii. Hii tayari ishatupa haki kabisa Mhe. Naibu Spika, na wanasheria wenyewe wanajua. Ni haki yetu kwa mujibu wa Katiba hii, lakini ninataka na hiyo inayokuja Mhe. Jusa amesema tuwe na muundo mwengine si vibaya tukiwa na muundo wa mikataba hakuna tatizo lolote kwa nini tuone tabu. Lakini tunaufanya *strong* na tunaelewa sasa *agreement na special date*, *expire date* watu wanakua wanajua. Sasa kwa hayo nakuomba Mheshimiwa kuwa hilo tufahamu.

La mwisho Mheshimiwa Makamo wa Pili fuatilia wajasiri tupo pamoja na wewe tutakusaidia ili kuwasaidia wazanzibari kuondokana na umaskini na Afya usiache kwenda, nenda kule kuna bomu kuna manyago mashine mbovu, mashine ya saratani mbovu hazifai ushapigwa changa la macho pesa wameshazila.

Kwa hayo machache nakaa kitako. Ahsante sana.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ili alau na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii muhimu sana ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba niitumie fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili na mimi niwe mchangiaji wa pili katika jioni hii. Mhe. Naibu Spika, naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Makamo wa Rais kwa namna anavyomshauri Mhe. Katika kutekeleza majukumu yake ya kulitumikia taifa letu hili. Sisi kama Wawakilishi tunaahidi kwamba tuko pamoja nae kuona kwamba gurudumu letu hili linaendelea na linakwamuka pale lilipokwama.

Mhe. Naibu Spika, naomba nianze na ukurasa wa tano katika hotuba hii ukurasa ambao umejikita katika kuzungumzia masuala ya Muungano. Katika suala la Muungano nitazungumzia katika maeneo mawili, eneo la kwanza ni eneo linalohusiana na kero zinazotokana na Muungano na eneo la pili nitaingia katika suala zima linalohusiana na mchakato wa Katiba mpya.

Mhe. Naibu Spika, kwa muda mrefu katika nchi yetu kuna maneno yamekuwa yakisikika nayo ni namna ya kupatiwa ufumbuzi kero za Muungano. Msamiati wa kero za Muungano si mgeni katika masikio ya Wazanzibari walio wengi, ni kitu kilichozoeleka na inavyoonekana ni dhahiri kwamba upatikanaji wa ufumbuzi juu ya kero za

Muungano ni ndoto. Kero za Muungano zitaendelea kuwa ni kero kwa sababu kuna misingi iliyopelekea kuwepo kwa kero za Muungano na kuna misingi pia iliyopelekea kero za Muungano kutokupatiwa ufumbuzi.

Sasa katika mambo hayo ambayo dhahiri jawabu lake halipatikani, mimi kwa muda mwingi pamoja na wananchi wengi tumekuwa tukijiuliza, hivi nchi zetu ziliungana au kilichotokea ni upande mmoja kuutawala upande mwengine kwa kivuli cha Muungano? Tumekuwa tukijiuliza maswali hayo. Kwa sababu walioungana kuna sifa za kuungana lakini vile vile kuna sifa za nchi moja kuitawala nchi nyengine.

Wataalamu wanatwambia moja kati ya sifa ambazo nchi zilizoungana kwanza kunakuwa na kitu mkataba na ni kawaida ya jambo lolote, kuweko na mkataba. Hata ndoa ya watu wawili mke na mume huwa kuna kitu mkataba. Kwa hivyo, kwa vyovyote vile sifa kuu ya Muungano ni mkataba kwa kile ambacho mmekubaliana kuungana. Lakini sifa ya pili kunakuwa na suala zima linalohusiana na kushauriana kati ya yale mambo ambayo mlikubaliana Muungane bila shaka binadamu si vikombe laitani vikombe navyo hupata muda vikagongana achilia mbali wanadamu.

Kwa hivyo, inapotokea kugongana kati ya mambo ambayo mmekubaliana kuungana kitu muhimu ni mashauriano kati ya mambo ambayo mmekubaliana kuungana. Lakini sifa nyengine ya tatu ni kuweko kwa maridhiano, maridhiano kwa yale mambo ambayo mlikubaliana kwamba hili na hili tushalitatua sasa tunaridhiana na mbali ya maridhiano kunakuwa na kitu utekelezaji way ale mliokubaliana. Kinyume cha hayo Mhe. Naibu Spika, ni ile sifa ya nchi moja kuitawala nchi nyengine.

Katika hali hiyo kunakuwa hakuna suala la kushauriana, kuambiana wala hakuna chochote kwa sababu hapo ni ubabe tu kwenda mbele. Sasa ni dhahiri tukiangalia sifa hizi mbili inaonekana kwamba kati ya walioungana kulikuwa na tofauti ya kimtazamo na kimawazo, mmoja aliamini kwamba tumeungana lakini upande wa pili uliamini kwamba tumewatawala upande mwengine kwa kivuli hiki cha Muungano.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, tofauti zetu zilizopo sisi Zanzibar tunaamini kwamba tumeungana na wenzetu wa Tanzania Bara, lakini nadhani na wenzetu wa Bara nao wanaamini kwamba wameitawala Zanzibar kupitia kivuli hiki cha Muungano na ndio maana wao katika kadhia yote hii hunyamaza kimya, lakini sisi Zanzibar kwa sababu tunaamini kwamba tumeungana ndio maana mara nyingi sisi tunakuwa tunalalamika tunapiga kelele, ni kwa msingi huo. Kwa sababu tunaamini kuwa kwa ridhaa yetu tuliungana na wenzetu kwa maana hiyo panapotokea jambo lolote tukae tushauriane tupange kwa yale mambo ambayo tumekubaliana lakini ni tofauti kabisa na wenzetu walioko upande wa pili.

Mhe. Naibu Spika, katika hali hiyo kuna mambo kwa kipindi kirefu ambayo yanaitwa kero na inaonekana kwamba hakuna mwelekeo wa kupatikana ufumbuzi ambayo wenzangu wameyataja tangu tuanze bajeti hii yamekuwa yakitajwa moja baada ya jengine, siwezi nikayataja kwa sababu naogopa kuchukua muda wako mwingi lakini yako mengi na ni katika yale maeneo ambayo Zanzibar inanufaika moja kwa moja katika masuala mazima ya kiuchumi. Mambo hayo ambayo kwa kweli yamedhibitiwa na wenzetu wao hawako tayari kusikia kabisa na hawako tayari kuyapatia ufumbuzi kwa maslahi ya nchi yetu. Lakini kuna mambo ambayo ni ya Muungano yako upande wetu Zanzibar na katika kipindi hiki Mhe. Naibu Spika, tumeshuhudia namna ambavyo na nchi yetu nayo imekuwa ikitekeleza.

Sasa ninachokusudia kukisema hapa ni hiki, kwamba kati ya mambo ambayo wenzetu yako kwenye mamlaka nayo na ambayo sisi Zanzibar hatuna uwezo nayo ndio hayo ambayo tumekwama. Lakini katika mambo ambayo ni ya kimuungano ambayo yako ndani ya uwezo wetu Mhe. Naibu Spika, kuna baadhi ya mambo serikali yetu imeyafanya wala hakuna mzinga wowote kwa sababu tunaamini kuwa sisi tumeungana na wenzetu. Katika muungano wa nchi mbili Zanzibar sisi ni sehemu ya Muungano huo bila ya kuwepo Zanzibar hakuna Tanzania, kati ya pande mbili huu ni upande mmoja. Kwa hivyo, wakati sasa umefika wa kujiamini Wazanzibari kwamba sisi ni sehemu ya Muungano, kwa kipindi kirefu kuna mambo ambayo tumeyatekeleza.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka kuna suala la Elimu ya Juu ni suala la Muungano, lakini wakati ulipofika Komandoo Dr. Salmin Amour Juma aliamua kuanzisha Chuo chake Kikuu hakuna bomu hata moja lililotuangukia.

Mhe. Naibu Spika, mambo ya ulinzi ni mambo ya Muungano lakini tulipofika pahala tukaona kwamba Zanzibar nasi tuwe na vyombo vyetu tulianzisha vikosi haidhuru tuliviita Idara Maalum lakini vile ni vyombo vyetu vya ulinzi tulivyonavyo Zanzibar. Lini tulipigwa bomu?

Bandari ni mambo ya Muungano lakini tulipofika pahala tukaona aa, tukaunda bandari yetu na hakuna bomu lolote tulilopigwa. Lakini Mhe. Naibu Spika, kama ikiwa mtu anapigwa kwa chake basi kwa hili tungelipigwa. Tulipofanya mabadiliko ya 10 ya Katiba ya Zanzibar mabadiliko yaliyotokana na hoja ya Mhe. Abubakar Khamis Bakary sisi wengine wengi tulijua kitakacholetwa ni kipengele tu kile kinachohusiana na kuundwa kwa serikali ya pamoja, lakini baadae tulipokaa katika Baraza hili mabadiliko tuliyoyapoata kutoka Baraza la Mapinduzi ni kuwemo pamoja na kipengele kwamba Zanzibar ni nchi.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano inatueleza wazi kwamba Tanzania ni nchi moja nayo ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini tulipoamua tulithubutu na katiba yetu tulithubutu kusema kwamba Zanzibar ni nchi atakae ni hivyo na aliyekuwa hataki ndio hivyo kwa lazima. Sasa katiba ya Tanzania itakayokuja Katiba ya Jamhuri ya Muungano lazima iridhie kuwepo kwa kipengele hicho kwa sababu tayari Wazanzibari tumeamua kukiweka hicho.
Sasa katika hali hii Mhe. Naibu Spika, hujiuliza kwa nini mambo mengine tunathubutu lakini kwa nini mambo mengine tunakosa ujasiri, tatizo liko wapi? Nasema inawezekana kuwa miongoni mwetu kuna kitu kinachoitwa kigeugeu, tunasumbuliwa Mhe. Naibu Spika, na ugeugeu wetu au undumila kuwili wetu. Ikiwa sisi tumeungana na wenzetu tuna uwezo wa kufanya chochote na hakuna chochote kitakachokuja.

Mhe. Spika, kwa hivyo katika hili nashauri kwa yale mambo ambayo hatuna uwezo nayo tuendelee kuyazungumza, lakini kwa yale mambo ambayo tuna uwezo nayo ndani ya mikono wetu ni wakati sasa wa kuamua kuyatekeleza. Suala la kuanzisha Shirika la Mafuta kwa ajili ya kutafuta mafuta tuliyonayo hilo halina mjadala tuna uwezo nalo sisi wenyewe wala hatusibiri kila kitu ni chetu pamoja, tuliungana pamoja kwa hiari zetu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba kila linalowezekana kulitekeleza ni wakati sasa tulitekeleze bila ya kuogopa chochote kama mtu anapigwa kwa chake acha tupigwe kwa chetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba Mwalimu Nyerere aliwaambia Watanzania, kuonea ni zambi kubwa lakini kukubali kuonewa ni zambi kubwa zaidi, tufuate ushauri huo aliotuelekeza Mwalimu. Wazanzibari sasa hivi umefika wakati tuache kulalamika, desturi ya mtu mlalamikaji ni mtu muoga, lazima sasa tuache maana yake sifa yetu Wazanzibari kwa kweli ni watu wa kulalamika sana, mwanamme halalamiki sana ni mtu huamua tu.
Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kadiri sisi tutakavyolalamika ndivyo ambavyoa wao wenzetu hata habari na sisi hawana, Waswahili husema, “Kelele za Chura hazimnyimi Tembo kunywa maji”, wala “kelele za mlango hazimkoseshi mwenye nyumba kupata usingizi”. Kelele Wazanzibari hazitotusaidia tuamueni wakati sasa umefika.

Mhe. Naibu Spika, baada ya suala hilo la kero za Muungano sasa naomba niingie kwenye mchakato wa Katiba mpya. Lakini kabla ya kuanza mchakato wa katiba mpya naomba niseme kwamba katika nchi yetu wananchi wamekuwa wamekuwa wana wasiwasi mkubwa, na kwa nini wakawa na wasiwasi, wamekuwa na wasiwasi kutokana na tulikotoka mpaka hapa tulipofika. Wasi wasi umewapata baada ya kuona kwamba kila tunalofanya na wenzetu ndani yake huwa kuna kitu hadaa, kwa hivyo kutokana na msingi huo ndio unaopelekea wananchi kuwa na wasiwasi. Watu wanasema, “atafunwaye na nyoka akiona unyasi hushituka”, na desturi ya mtu mwenye akili huwa hatafunwi na nyoka kwenye shimo moja mara mbili. Kwa hivyo, ujio wa Katiba mpya umewapa wasiwasi wananchi juu ya namna ambavyo tunaweza tukafanikiwa au tukarudi hatua nyingi nyuma.

Sasa katika hali hiyo ya wananchi wetu kuwa na wasiwasi ni jukumu la serikali sasa kuwafahamisha wananchi, si wananchi tu bali hata baadhi yetu Wawakilishi tunakuwa tuna wasiwasi, nani sasa atakayetutoa wasiwasi? Au twende barabarani tukatolewe wasiwasi, nani atakaekuwa na dhamana hiyo? Nadhani serikali kama chombo chetu wananchi ni wakati wake kututoa wasiwasi. Miongoni mwa watu ambao wana wasiwasi wa kwanza ni mimi na leo naomba nitumie fursa hii ili wanaojua mambo waje wanitoe wasiwasi kwa niaba ya wananchi.

Suala la kwanza najiuliza hivi tatizo letu sisi hasa ni kitu gani? Tatizo letu ni Katiba au ni mfumo? Kwa fikira zangu nadhani Mhe. Naibu Spika, tatizo letu la msingi ni mfumo na hata ukiwasikia viongozi, wawakilishi, ukiwasikia wataalamu mbali mbali wote wanazungumzia mfumo. Kwa sababu mimi naamini kwamba mfumo ndio unaotengeneza katiba, lakini katiba haiwezi kutengeneza mfumo. Kwa hivyo, ninachoamini kwamba tatizo letu ni mfumo na Mhe. Naibu Spika, laitani kama tungelikuwa na Muungano wa haki basi katika mchakato huu wa katiba kwanza tungelianzia na kuzitaka nchi mbili zilizoungana tuelezewe namna ya mfumo tunaouhitaji. Kwa sababu

naamini narudia tena, kwamba imani yangu ni kuwa mfumo ndio unaotengeneza katiba, mkataba huzaa katiba lakini katiba haiwezi kuzaa mkataba.

Mfumo ndio unaotengeneza katiba na katiba haiwezi kutengeneza mfumo, hatuwezi tukachukua cha kwanza tukakifanya cha pili na cha pili tukakifanya cha kwanza, tulipaswa kwanza tuanze na mfumo. Kwa hivyo kama tungelikuwa na muundo wa haki wa Muungano kwanza tungelikuja kwenye nchi mbili zilizoungana masikini Tanganyika haipo mwenzetu, laiti Tanganyika ingelikuwepo tungeliwaambia Watanganyika kwanza wapendekeze mfumo wao na Wazanzibari wapendekeze mfumo wao, tungelikwishakubaliana kwenye mfumo kwamba sasa twende mfumo huu ndio baadae tukapata katiba, kwa sababu katiba mmbele ya mkataba katiba ni kanuni tu ya mkataba.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa hilo limekosekana mimi naomba niseme kwamba hata hii Sheria Nam. 8 ya mwaka 2011 kwa maoni yangu ina matatizo yake, kwamba tayari katika kipengelele cha 9 kama ukikisoma vizuri kuwa kati ya mambo ambayo tume imeambiwa isiyazingatie kisheria kwanza ni suala la kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano, lakini vile vile kuwepo kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano na kuwepo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa mimi huwa najiuliza, kwamba ikiwa ndani ya sheria imeshatamkwa hivyo kuwa kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano kusihojiwe wale walioambiwa kwamba wende mbele ya tume na wakasema serikali wanazozitaka itawasaidia nini? Hivyo ikiwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwepo wale wanaotaka serikali moja hiyo itawasaidia nini? Wale waliokuwa hawataki wa kuwa na Bunge lile tulilonalo wao itawasaidia nini? Kwa fikira zangu naomba nielimishwe kwamba tayari kifungu kile cha 9 kimekwisha kuacha mfumo huu kuwa mfumo huu uendelee kuwepo.

Mhe. Naibu Spika, unaposema Muungano usijadiliwe, unapokataa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iwepo, Bunge la Jamhuri ya Muungano liwepo, Baraza la Wawakilishi katika sheria ya Kiswahili sikuliona pengine wamesahau, maana yake nini? Maana yake ni kusema kwamba mfumo utakaokuwepo ni mfumo huu tulionao sasa hivi ndio maana yake, vyenginevyo Mwenyekiti wa Tume akawaambie watu njooni mseme mtakavyo na mimi nitawasilikiza huko ni kuwapumbaza watu wenye akili.

Sasa Mhe. Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo naomba niseme kwamba, pamoja na mazingaombwe yote yaliopo lakini Wazanzibari hatujachelewa bado muda tunao, pamoja na yote lakini muda tunao. Nataka niseme kwamba jazba haitatusaidia, wala kuisusia tume nako hakutatusaidia na kufanya fujo hakutotusaidia. Kinakachokuwepo kwa vyovyote vile Waswahili walisema Mhe. Naibu Spika, “Chuzi la vivyo hutoelewa vivo”, Ng’ombe alalavyo ndivyo achinjwavyo”, na “goma lipigwavyo ndivyo lichezwavyo”. Madhali sasa hilo tumelishuhudia naomba nitoe rai kwa Wazanzibari wenzetu kwamba tujipangeni kwa muda huu, tushauriane muda huu, twendeni mbele ya tume pamoja na mambo mengi mtu atakayoyazungumza lakini twendeni pale ku-*set* mfumo wa Muungano wetu. Hilo linawezekana kabisa kabisa.

Nataka niseme Mhe. Naibu Spika, kwamba suala hili tusilichukue vyama vya siasa tu, suala hili ni kubwa zaidi ya vyama vyetu, suala hili tunalolizungumzia ni suala la Zanzibar ni suala la khatima ya nchi yetu ya Zanzibar. Vyama vyetu hivi ni vidogo mbele ya nchi yetu, vyama vilikuja juzi, vyama vitaondoka lakini Zanzibar haitoondoka. Kwa hiyo suala hili tusilichukue katika vyama kwa sababu *CUF* akizungumza kwenda kulia na CCM akizungumza kwenda kushoto, *CHADEMA* akasema twende kaskazini nakuhakikishieni kwamba tutakuwa tumefeli kabla ya kufika mbele ya tume.

Vile vile suala hili Mhe. Naibu Spika, tusiliingize katika dini, pamoja na wingi wetu wa Waisilamu Zanzibar lakini tukumbuke kwamba na Wakristo nao wapo, nao wana haki kamili, Waisilamu lazima waheshimiwe kwa wingi wao lakini na Wakristo nao wasidharauliwe kwa uchache wao, lazima twende pamoja katika hili, lakini vile vile Zanzibar kama ilivyo kuna wananchi wenzetu Wazanzibari ambao nao huabudu katika mizimu. Mabuda wapo, wanaokwenda kwenye mahekalu wapo, hawa wote ni Wazanzibari na wana haki kamili, ni wakati sasa umefika wa suala hili Mhe. Naibu Spika, tulizungumze kama Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, katika hapa nataka niilaumu serikali, kwamba hili suala tunalichukua kwa uzito mdogo sana, unawaambia Wazanzibari nendeni kwenye tume wende wakazungumze nini, kama hujatwambia nendeni mkazungumze hiki. Kwa sababu suala hili ni la nchi si suala la mtu mmoja mmoja tu. Nakumbuka tulivyoanzisha Mfumo huu wa Serikali ya Pamoja Baraza letu hili liliunda kamati ya watu sita Kamati ya Mhe. Ali Mzee Ali, walifanya kazi nzuri sana Unguja na Pemba, walitembea katika wilaya zote wakenda katika taasisi zote za kidini na

zilizokuwa si za kidini na taasisi nyengine. Tulifanya kazi moja nzuri na matokeo yake kwa kweli haya ambayo leo tunayafurahia katika Baraza hili.

Lakini kwa nini suala hili muhimu tunaliachia tu, Mhe. Ismail Jussa asubuhi kapendekeza lakini na mimi naomba niongeze nyongeza katika pendekezo lake. Ikiwezekana hata hiki chombo cha wananchi kwa sababu hiki ndio chombo cha wananchi, iundwe kamati itakayopita katika wilaya zote, vichochoro vyote Unguja na Pemba kulielimisha suala hili, vyenginevyo vyovyote Mhe. Naibu Spika, suala hili tutalichukulia kwa uzito mdogo na ninawahakikishieni Wazanzibari tutafeli Zanzibar kabla hatujenda mbele ya tume. Wakati bado upo lazima tuutumie vizuri ili tuone kwamba tunakwamuka pale ambapo tumefanikiwa. Mimi naamini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu Wazanzibari tutafanikiwa, lakini lazima tuondoshe tofauti zetu zilizopo za kivyama, kidini na mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kueleza hayo sasa kwa ufupi sana naomba kwenye suala linalohusiana na uwajibikaji wa serikali. Mhe. Naibu Spika, Makamo wa Pili wa Rais ndiye mtendaji mkuu, ndiye mtendaji wa shughuli za serikali katika Baraza letu. Mimi binafsi siridhiki na utendaji wa shughuli za serikali, kunakuwa na matatizo makubwa, kunakuwa na dharau kubwa uwajibikaji ni mdogo sana. Hii yote maana yake ni kwamba, serikali haiyafanyii kazi mapendekezo tunayoyatoa katika Baraza hili. Napendekeza mara nyengine itakapokuja hotuba nyengine mbali ya kuambia mambo ambayo tumeyaeleza kama ni utendaji katika Baraza hili, basi Mhe. Makamo wa Pili atakapokuja atwambie kati ya mambo ambayo tumeyapendekeza kwa watendaji wa serikali ni lipi na lipi limefanyiwa kazi na lipi na lipi halifanyiwa kazi na kwa sababu gani halijafanyiwa kazi.

Sambamba na hilo Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kitu chengine, kuwa juzi wakati Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo akizungumza alizungumza kitu ambacho mimi binafsi sikuridhika nacho na kwa sababu kinakwenda kinyume na utaratibu. Alisema kwamba “serikali ina uwezo wa kufanya vile inavyotaka katika masuala ya uendeshaji”.

Mhe. Naibu Spika, serikali yetu haituambii hivyo, serikali haina uwezo wa kufanya inachotaka kwa mujibu wa Katiba kifungu cha 5 kimepewa mamlaka serikali ya kuwa na shughuli za utendaji, lakini Baraza hili limepewa mamlaka ya kuisimamia serikali. Kwa hivyo kama kuna suala lolote kama ilivyozungumzwa la kuuzwa majumba ya serikali naomba ikumbukwe tu kwamba hakuna ruhusa ya kutumia fedha yoyote ambayo Baraza hili halijaidhinisha. Kwa hivyo, kama ikiwa kuna majumba yanataka kuuzwa ni lazima tufike pahala tuambiwe ni nyumba ipi na ipi inataka kuuzwa na inataka kuuzwa kwa thamani gani, ili mwisho wa siku tujue tulichokiidhinisha ni nini na kilichotumika ni nini. Kinyume na hilo basi mimi naomba nitangaze *query* kabla huyo mdhibiti hajaja kwamba hiyo itakuwa ni *query* katika ofisi yake.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru *Allah* kwa kutupa uhai, uzima na *taufiq* ya kuzungumza. Pili, naendelea tena kuwapelekea salamu za Baraza wananchi wote wa Jimbo la Ziwani kwa umahiri wao na taarifa iliyokwishatoka kwamba Tume ya Kuratibu Maoni haya ya Muungano itaanza katika Mkoa wa Kusini Pemba. Kwa hivyo, tunawaomba sana wajitayarishe ili itakapokuja waweze kusema yale ambayo yamo ndani ya nyoyo zao kuhusu suala zima la maoni ya Katiba.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuunga mkono yale ambayo wamezungumza wenzangu waliotangulia kuhusu masuala ya Muungano mimi sitaki niingie sana huko naomba nizungumze mambo machache sana.

Mhe. Naibu Spika, Muungano ulio wa kweli katika kuendelea kwake unaweza ukapimwa na nia njema iliyopo kati ya wale walioungana. Hakuna Muungano wowote duniani uliokuwa haina matatizo. Hivi karibuni katika *European Union* kulitokezea matatizo ya kiuchumi katika baadhi ya nchi nyingi za *European Union*. Na kwa sababu ya nia njema ya ule muungano wao wakaanza kuweka *fund* maalum wenyewe wanaita *bail out* ili kuzisaidia zile nchi ambazo zimeingia katika migogoro ya kifedha. Laiti kama muungano ule ulikuwa hauna nia njema basi ilikuwa ni rahisi kuziachia nchi zile zikaporomoka na nyengine madhali ni tajiri zikaendelea kukua, kwa sababu wangeliwanufaisha raia wao.

Lakini naamini kutokana na njia njema za ule muungano wenyewe utaratibu ule ukawafanya bado wabaki katika muungano wao au mkataba ule wa *European Union*.Pamoja na mashaka mengi tunayoyatoa, lakini dalili zinaonesha

kwamba Muungano huu tulionao baadhi ya viongozi walio katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano hawana nia njema na Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninao ushahidi mwingi lakini nitatoa mambo mawili tu katika hii sentensi niliyoisema. Katika mwaka 2009 ilipandishwa bei ya umeme, Tanzania Bara Shirika la *TANESCO* lilipandisha bei ya umeme kwa asilimia 21.6, kwa Zanzibar shirika hilo hilo la umeme lilipandisha bei kwa asilimia 168, umeme ambao ile njia ya kuchukulia umeme ni fedha za Zanzibar zilizotumika na pia hawau-*service* ule umeme wao wanauza *bulk* umeme. Pamoja na jitihada zote zilizofanywa mpaka juzi nasikia kwa Zanzibar kujizuia kulipa zile, ikawa inalipa kile ambacho kilitarajiwa. Ndio likaanza kuambiwa Serikali ya Muungano imesaidia Zanzibar. Itaisaidia vipi wakati sheria za ulimwengu za kuuza umeme zipo? Sio sisi tu ndio tunaonunua umeme nje ya nchi.

Nchi za Afrika ya Mashariki kama Uganda inauza umeme, Ethiopia inauza umeme katika nchi nyengine na nchi chungu nzima duniani. Sheria za kimataifa zipo za kuuza umeme na za kukubaliana lakini *TANESCO* iliopo hapa hapa Tanzania ilijifanya kwamba *twenty one times* ngapi hata upate *one sixty eight*, ilituuzia Zanzibar umeme mara nane kuliko ambavyo wameuza Tanzania Bara, wakati *service* yote haifanywi na *TANESCO*, hapa lipo Shirika la *ZECO*.

Sasa aangalie hapo kama Muungano wetu ulikuwa na nia njema wangetufanyia hivi wakati suala hili liliingiliwa mpaka na Waziri, Raia mwenyewe, *still* deni likawepo pale pale. Juzi baada ya kuona Zanzibar wamekuwa sugu na hakuna njia nyengine labda na hii Katiba mpya inayokuja, ndio wakaanza hiyo kupunguza kwa kutia ulaini, kwa sababu ukishaona umekwama unaweza ukatia grease katika gari.

Sasa mimi ninawaambia Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari tujitazame uzuri na muungano huu. Mimi mwenyewe nikiwa ni mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza lililopita, tulikwenda katika Benki Kuu ya Tanzania tukakutana na mwenyewe Gavana mwenyewe na timu yake. Zanzibar ikiwa na kiwanda chake inatarajia iuze asilimia 21 tu ya kinachozalishwa kwa Tanzania Bara, chengine chote hakiruhusiwi kuuzwa kwa mujibu wa utaratibu wao kwa sababu ni viwanda vya ndani na zipo katika *free zone*.

Sasa nikawauliza mimi, sisi tunaagiza mazao mengi sana ya chakula na mboga mboga kutoka Tanzania Bara, kwa nini hamuweki basi kwa sababu wakati huo tulikuwa na nakisi ya bajeti ya kiasi shilingi bilioni 19; yaani biashara yetu na Tanzania Bara ilikuwa sisi tunaagiza vingi zaidi kuliko wanavyoagiza wao kwa shilingi bilioni 19.

Kwa nini basi hamuzidishi hii asilimia kutokana na huu ukuruba tulionao sisi kwamba na sisi tunaagiza hizi bidhaa ambazo soko wazi lipo huku? Aah! maana yake haya ni masuala ya kisera, sijui nini, hawakufanya hivyo. Na ndio chanzo kimoja cha kufa viwanda Zanzibar, kwa sababu vile vinavyokuja haviruhusu kusafirisha bidhaa yake kwa kiwango chote au kwa kiwango kikubwa katika Zanzibar. Na wale wanaopata *transit* pale ndio wanaambiwa wanakipitisha pale kwa ujanja kwenda Burundi na kwengineko.

Lakini suala la pili ambalo ninalo ushahidi wake Mhe. Naibu Spika, katika hii Katiba ya Jamhuri ya Muungano ibara ya 103 (1) inasema hivi, “Kutakuwa na Serikali ya Zanzibar itakayojulikana kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo itakuwa na mamlaka”, hii ni Katiba juu ya mambo yote yasiyo ya muungano kwa mujibu wa sharti ya Katiba hii.

Ninataka tukipitie uzuri kifungu hiki, kutakuwa na mamlaka juu ya mambo yasiyokuwa ya Muungano. Mhe. Hamad Masoud na wengineo juzi walikuja kutupa ripoti hapa kwamba tayari imeshatiwa saini mkataba wa kujenga barabara ya Chake-Chake hadi Wete, nani aliyetia saini ni Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano. Wao sio waliosema ndani ya Katiba hii kwamba Zanzibar itakuwa na mamlaka yasiyokuwa ya muungano? Hii barabara ni mambo ya muungano?

Kama wao wanaifuata hii Katiba, katika hali hii iliyo kwa nini wasimuache Sheikh Omar Yussuf Mzee akatia saini kwa niaba ya Zanzibar? Akaekwa mkiani humu wenyewe wanatia saini. Kama kweli kuna nia njema hata katika kipindi hiki kwenye Baraza hili hili tulisema kwamba Baraza lililopita lile basi ikiwa Tanzania imeingia katika sera ya mambo ya nje ya kiuchumi, basi balozi za Tanzania ziweke Zanzibar *ATH* wa kiuchumi, yupo wapi katika balozi?

Kulitaja lile neno la Zanzibar katika balozi zao hawataki. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ni jambo ambalo halitaki tochi. Muundo huu wa muungano hautufai, tutafute njia nyengine ya kushirikiana na wenzetu, ndio dunia ilivyo. Dunia huwezi kuishi peke yako, lazima utafute majirani zako mushirikiane lakini uwe na uhuru wako, uwe na utambuzi wako na heshima yako.

Mimi sisemi haya kwa kutokezea haya mambo ya Katiba juzi. Mimi nimeshauliza katika Baraza hili *protocol* ya Rais wetu wa Zanzibar ipo wapi, hakuna na hapana popote. *Protocol* ya Rais wa Zanzibar ni ya kupewa, kusaidiwa, asaidiwe mueke hapa, mtafutie upenu akae, mtafutie kiti hiki akae basi lakini Rais wa Zanzibar hana protocol katika Tanzania kwa sababu hayumo katika *high rank* ya uongozi. Hilo la kwanza nimemaliza.

Mhe. Naibu Spika, katika kazi za kawaida za utekelezaji wa shughuli za Makamo wa Pili wa Rais, ninapenda nitoe pongezi kubwa sana kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Mhe. Naibu Spika, uchungu wa kufanyiwa mambo tunayofanyiwa ulinifanya nisahau kumpongeza ilikuwa tokea mwanzo lakini kwa hili atanivumilia.

Nampongeza Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwa mambo mawili makubwa. Kwanza ni kiongozi wa mwanzo wa shughuli za serikali aliyeruhusu na halafu akanyanyua mkono kuundwa kwa Tume teule za Baraza la Wawakilishi. Mimi ninaamini sana kwamba kaiva sana na kazi za Wawakilishi, kwa hivyo kwa hili ninampongeza na tunamtakia kila heri.

Lakini la pili, yeye ni muongoza njia, kwa hivyo baada ya kuingia katika kazi na kuitizama Zanzibar aliona kwamba matatizo ya ardhi ni makubwa, akaanza kuonesha njia, nini kilichotokea kwa wafuasi na watendaji wake wakati utahukumu, lakini yeye tunamshukuru sana kwa kuonesha njia.

Kuwa njia tunayokwenda njia sio, migogoro hii ya ardhi hii ambayo inayosababishwa na wakubwa, wenye vyeo na pesa wacheni mambo haya. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ninakushukuru sana na mimi mara hii utaniona nitakavyokuja. Kuna watu wanazuia hata yale maslahi ya nchi kwa sababu ya ubinafsi katika masuala ya ardhi na mengine yanayohusiana na hapo.

Baada ya pongezi hizo, ninakwenda kwenye Kitengo au katika Idara ya Sherehe na Maadhimisho. Mhe. Naibu Spika, moja katika kazi za bajeti ni kuangalia mipango ya serikali namna inavyokusanya fedha na inavyozielekeza. Lakini pia kuna vipaumbele. Inawezekana unaelekeza fedha lakini sio kipaumbele.

Zanzibar ina kipaumbele chake katika bajeti. Tukija katika hii Ofisi ya Sherehe na Maadhimisho, mimi nina maswali matatu katika uchunguzi nilioufanya ghafla. Kwanza Idara ya Sherehe, mishahara ni shilingi milioni sitini na nane nukta tatu saba. Lakini Idara ya Uendeshaji, Sera, na Utafiti ni shilingi milioni sitini na moja.

Sasa mimi ninajiuliza hivi kweli Idara hii ya Sherehe tu ambazo zinatokea kwa kipindi mara moja au mara mbili, na mambo mengine matokeo yanatokea ghafla hivi iwe na mshahara zaidi ya kile kitengo ambacho kinafanya kazi kwa kila siku. Ni watu wangapi walioajiriwa kwenye sherehe?
Katika mfumo tulionao hivi sasa, tunahitaji watu wote hao kushughulikia sherehe tu? Wana-*consume* shilingi milioni sitini na moja na sitini na nane, wakati Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina shilingi milioni sitini na moja. Sizungumzii zile fedha zilizotumika kwenye sherehe bado huko, ninazungumza ile mishahara, jee kuna wafanyakazi kweli wanaowapita Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kiwango hicho?

Lakini katika hichi kitabu kikubwa kuna kitu mimi nimekiona. Pahali penye kifungu cha 22060 ndio sijui litakuwa fungu hilo? samani za ofisi, mapazia, makapeti, viti na makabati ni shilingi milioni thalathini na tatu. Hii kidogo inatia wasi wasi.

Mapazia, makapeti vipi, viti na makabati ni shilingi milioni thalathini na tatu. Hapa kidogo ninataka maelezo hapa. Ni viti vipi vina usingizi ndani yake, vinachombeza au vina muziki chini? Sifanyi masikhara shilingi milioni thalathini na tatu kwa vitu vinne hivi kwa mwaka mmoja kwa ofisi ya Mapambo na Sherehe hadi tupate maelezo.

Halafu Mhe. Naibu Spika, ukija katika kifungu chengine cha misharaha kuna *special allowance*. Hebu tueleze katika hawa, posho maalum aje atueleze Mhe. Waziri hili posho maalum ni lipi katika Idara hii ya Sherehe? Na lilipanda.

Kwanza kabla sijaenda mbele, hii samani mwaka jana ilitengewa shilingi milioni tatu, mia tatu hamsini elfu. Hapa tungekuwa safi kabisa lakini mwaka huu shilingi milioni thalathini na tatu na laki tatu. Sasa hapa kidogo tupulize kidogo.
Katika kifungu 21100 mishahara, kuna posho maalum shilingi milioni ishirini mia tatu hamsini na nane. Wakati wa saa za kazi, malipo ya kujikimu, posho la kushika wadhifa, posho la vikao tayari, hili posho maalum tu ni shilingi milioni ishirini ambalo ni nusu ya mishahara yote iliyowekwa hapa.

Sasa maana yangu nini mimi. Maana yangu ya kumwambia Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri pamoja na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwamba, hivi ndivyo serikali yetu inavyoibiwa. Tuangalie humu ndani na ndio hawa wenzetu waliochangia wakasema zifuatiliwe hizi taratibu, kwa sababu kuna baadhi ya mambo hayalingani kabisa. Tunajua kuwa kila kitu kinataka kutumiwa. Kama ingelikuwa hii wizara imejenga jengo jipya, sasa wanataka kununua kila kitu, kweli shilingi milioni thalathini na tatu sio kubwa kwa sababu unataka ku-*furnish* lile jengo jipya. Lakini tunataka tuje tupate maelezo hizi shilingi milioni thalathini na tatu ni za jengo gani katika mwaka huu 2012/13.

Mhe. Naibu Spika, ninakuja katika Kitengo cha Kuratibu na Kusimamia Shughuli za Utafiti. Kuna mambo yameelezwa mengi na ninashukuru kwamba ule mchanganuo wa mambo ni mzuri, lakini kuna mambo ya kitaifa na hii ofisi ndio inayoshughulikia wizara zote.

Kuna utafiti uliofanywa na Wizara ya Kilimo, jambo ambalo mpaka hivi sasa limeathiri hata uchumi wa Zanzibar kwa sababu hakuna anayethubutu kusafirisha tunda lolote hivi sasa, kutokana na wadudu hao walioingia wa matunda, walianza kwenye embe. Ninamuuliza Mhe. Waziri huu utafiti umeunganishwa vipi na kitengo kikuu huko, ili kuhakikisha kwamba Zanzibar inaondokana na tatizo hili na linapangiwa mwaka gani. Kwa sababu bado Wizara ya Kilimo haijafika, lakini majibu yao ya nyuma yalikuwa hayakutosheleza kabisa, kwa sababu tuliwapa rai nyingi lakini hawakuzifuata, wakasema kwamba mitego imeshapatikana. Lakini kwa njia nyengine ya utafiti hao wadudu waharibifu wa matunda ambao ndio tegemeo la Zanzibar.

Zanzibar ardhi yake ni ndogo, kilimo chetu kitanufaika zaidi kwa matunda, lakini ikiwa hata matunda hatuna uwezo wa kusafirisha au kuyauza, tunategemea nini. Sasa mimi ninafikiria kwamba utafiti wa wadudu hawa waharibifu wa matunda, ni utafiti muhimu sana kwa uchumi wa Zanzibar na kwa maendeleo ya ustawi wa jamii kwa jumla.

Maembe yanazaa bila ya kutiliwa maji, hayataki umwagiliaji wowote lakini ikiwa *population* ya embe karibu laki moja kila muembe zote zina mafunza, mwananchi unamwambia vipi na serikali ndio wajibu wake kuhakikisha kwamba mambo yale yanapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Naibu Spika: Bado dakika tano kwenye muda wako.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ninakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, nitazitumia vizuri sana.

Suala ambalo linalofuata ni suala la Idara ya Uratibu. Uratibu huu mimi ninakusudia ni vitengo vya Muungano kwa sasa. Kuna baadhi ya Wizara, kwa mfano Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Kitengo cha Leseni na Mambo ya Barabarani, kuna askari *traffic* wao ni askari wa Serikali ya Muungano.

Kitengo cha Leseni ni kitengo kinachoshughulikiwa na SMZ, lakini hawa watu wawili ni lazima wakubaliane ili huko barabarani kupatikane usalama na mambo mengine. Jee, Mhe. Waziri hujapata malalamiko haya kwamba Idara hii haipati ushirikiano wa kutosha kutoka katika Jeshi la Polisi? Na ikiwa umeshapata ni hatua gani uliyochukua ili raia wetu barabarani wawe salama?
Mhe. Naibu Spika, jambo la mwisho ninalotaka kuzungumza mimi ni Tume ya Uchaguzi. Mara hii kumetajwa tu kuwa ni Tume ya Uchaguzi lakini hatujui kwamba kutayarisha, kuongeza kunangojewa mpaka 2014/15 au hili ni suala la kila mwaka kuongeza majina, na serikali ina hatua gani? Tunavyoona sisi na juzi tumezungumza hapa suala la vitambulisho vya Mzanzibari, Zanzibar tumezoea kutesana vile vile.

Kwa sababu kama Tume ya Uchaguzi ingelikuwa na utaratibu wa kuongeza daftari kila mwaka hata ule msongamano ingelikosekana. Lakini tunakaa kimya mwaka 2010 ndio umeshapita uchaguzi, 2011, 2012 hapaulizwi mtu kwenda kujiandikisha. Lakini mpaka ule uchaguzi ufike tena utasikia tena Tume haina pesa, haina nini, wakati bajeti ndogo za kila mwaka zingetosha kuandikisha watu elfu moja au mbili wanaoongezeka kila mwaka.

Lakini kwa nini hapaongezwi imekaa tu Tume. Hebu tupe habari Mhe. Waziri Tume hii ipo vipi haina watu wengine hivi sasa, waweke wengine kama wamejiuzulu. Lakini utueleze kwamba mara hii tumepanga kusajili wote waliotimia umri na waliokuwa bado. Lakini tukingoja mpaka mwaka 2014/15 ndio matatizo yanapotokezea. Utasikia Tume haina pesa, hivi wananchi hawaendi kuchukua vipande vyao.

Kuna kisingizio siku hizi vipande vya uandikishaji ati watu hawaendi kuvichukua. Mimi binafsi siamini. Kuwa mtu ataandikisha kipande cha ukaazi asiende kukichukua, wakati akienda benki anaulizwa kipande, akienda kurithi anaulizwa hicho hicho, akitaka pasipoti anaulizwa, akitaka mshahara wake anaulizwa. Haya kwa nini asiende.

Hebu niambie Mhe. Naibu Spika, Mawaziri wengi wapo hapa, madereva tumo tele humu njiani. Ni dereva gani leseni yake iliyokuwa ipo kule Ofisini hajaenda kuichukua. Basi itakuwa ajabu ni hicho kitambulisho cha Mzanzibari tu kuwa ndivyo havichukuliwi. Ni cheti gani cha kuzaliwa kinakaa kule kikawa mtu haendi kukichukua. Siku zote tunapiga kelele hapa vyeti havitolewi, lakini usije kusema kitambulisho cha Mzanzibari utasikia watu hawaendi kuvichukua. Basi hawa Wazanzibari mimi ninasema tusiwadhalilishe. Maana yake katika mtu kumwambia hajaenda kukichukua ni punguani, kuwafanya Wazanzibari punguani.

Mhe. Naibu Spika: Malizia mheshimiwa.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ninakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa niaba yangu binafsi na kwa wananchi wa Jimbo la Ziwani, nitapenda sana kuunga mkono hoja hii iwapo mambo mazuri niliyozungumza yatapata maelezo mazuri ya Mhe. Waziri.
Lakini mwisho kabisa kwa sababu Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, yeye ni mshauri mkuu katika washauri wawili wa Mhe. Rais, pongezi nzito zaidi ninazitoa kwa Mhe. Rais Dk. Ali Mohamed Shein kwa uvumilivu wake na kazi yake anayoionesha kwa Wazanzibari juu ya namna gani ya kuendesha nchi.

Ninakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa jioni hii. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na kutufikisha hapa.

Pili, napenda kumshukuru Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Waziri wake pamoja na watendaji wake kwa kutuletea bajeti hii ilioko mbele yetu. Vile vile Mhe. Naibu Spika, napenda kumpongeza Rais wetu wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kutusikiliza kilio chetu cha Wazanzibari kuhusu wazazi, yaani kinamama wajawazito katika suala la operesheni.

Mhe. Naibu Spika, sisi wana kamati tulikuwa tukilipigia kelele sana suala wakati tunakiwa kwenye kamati na Mwenyezi Mungu katujaalia Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kaliona na kulitilia mkazo kwamba huduma hii itolewe bure.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu tatizo la ardhi katika eneo la Kizimkazi sehemu ya Mchangamle. Sehemu ile ni ya Wazanzibari wenyewe wazaliwa wa Kizimkazi ambao walikuwa na konde zao, wakatokea watu wenye nguvu wakenda kuwapora, wakati wananchi wale walikuwa wanalima vilimo vyao, waliwaondoa na kuchukua ardhi ile wakajenga nyumba za wageni na hawakuwapa fidia ya aina yoyote. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningeiomba wizara yako ilitizame suala hili na ilichukulie hatua.

Mhe. Naibu Spika, watu wale mpaka hivi sasa bado hawana sehemu ya kulima na ile sehemu ni yao wenyewe, wana hati miliki na kila kitu. Kwa hivyo, ningeiomba serikali ilione suala hili na kulichukulia hatua.

Mhe. Naibu Spika, jengine nije katika suala la maafa. Mhe. Naibu Spika, mwaka 2010 siku ya tarehe 29 Oktoba, kulitokea maafa kwenye maeneo ya Hakunamajiwe Jambiani. Maafa yake ilikuwa watu wanaondoka Jambiani kuelekea katika kampeni ya CCM, gari ilipinduka na wengine walifariki pale pale, wengine mpaka leo ni vilema. Kwa hivyo, ningeiomba serikali imtizame yule ambaye ni kilema na kilema kile kimemtokea pale. Tumehangaika mpaka nikaiomba serikali ili afanikiwe mtu yule kupatiwa mkono wa bandia. Lakini mkono ule haufanyi chochote, *Alhamdulillah* si haba serikali imemuona na kumtia mkono ule kwa milioni 6. Lakini Mhe. Naibu Spika, mkono ule haumsaidii chochote. Kwa hivyo, ningeiomba serikali umuezeshe ili aendeshe maisha yake.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye suala la Muungano. Mimi sina la kuzungumza kwa vile wenzangu wengi wamezungumza kuhusu suala hili. Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari wana hofu na hii tume ambayo itakuja kuchukua maoni. Je, hii tume ina ukweli gani na itatuhakikishia vipi kwamba kweli Wazanzibari wamefikia kima hiki cha kutaka Uzanzibari wao, waziri utatuhakikishia vipi tume hii kwamba ina ukweli kiasi gani na itakuwa na uadilifu gani. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri akija kufanya majumuisho atueleze kuhusu tume hii, atutowe wasi wasi wananchi Wazanzibari wasiwe na wasi wasi. Hivi sasa hawana wasi wasi isipokuwa wana wasi wasi na tume. Hii tume ina ukweli kiasi gani.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi ili nichangie katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tukakutana katika mwaka mwengine, kwa ajili ya kuchangia kwenye kikao hiki cha bajeti kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya katika nchi yetu, kwenye kazi ya kuwatetea Wazanzibari na kuitetea nchi ya Zanzibar. Mhe. Makamu wa Pili anaonekana yuko mbele sana katika hili. Nikushukuru sana Mhe. Makamu wa Pili.

Vile vile nimshukuru Mhe. Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kutusomea bajeti hii, niwashukuru watendaji wa wizara hii kwa mashirikiano yao wote wakaweza kufanikisha hotuba hii na kuweza kuwasilishwa hapa na sisi kuweza kuichangia.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze mchango wangu kidogo kwa kunukuu katiba, kwenye kifungu cha 5(a) (1), kinasema

Kifungu cha 5(a) (1)

> "Zanzibar itafuata mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati ya mamlaka tatu. Mamlaka ya utendaji, mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma na mamlaka ya kutekeleza utoaji haki".

Mhe. Naibu Spika, nikienda nambari (2) kinasema,

Kifungu cha 5(a) (2)

> "Mamlaka ya utendaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma ni Baraza la Wawakilishi, lakini mamlaka ya kutekeleza utoaji haki ni Mahakama".

Mhe. Naibu Spika, nimeanza hapo ili niweze kuendelea kutoa michango yangu. Mhe. Naibu Spika, juzi nilitoa mchango wangu katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, nilizungumzia juu suala la uuzwaji wa majengo yale. Nashauri sasa kwamba ikiwezekana ni vyema majengo ya aina ile au mikataba ile mzito inapotaka kufungwa kule na serikali, basi iletwe kwenye Baraza kwa kupitia hata kama ni kwenye kamati za Baraza, ili tuweze kuiangalia.

Mhe. Naibu Spika, ningefurahi kama Mhe. Waziri wa Fedha angekuwepo, kwa sababu alisema kwamba hilo ni suala la serikali, kazi ya kuuza na kununua ni masuala ya serikali. Mimi sijakataa, lakini ninachomuambia, sikuwa na maana serikali isifanye hivyo, hapana. Nilikuwa na maana kwamba ile kazi ya Baraza ya usimamizi, basi tuweze kuisimamia vizuri, hiyo ilikuwa ndio hoja yangu.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia kwenye kitabu hiki cha *Public Procurement Act.* Humu ndio yanaelezwa masuala ya ununuzi. Sasa hoja ilikuwa sio kwamba serikali isinunuwe au isiuze, lakini hoja yetu ilikuwa ni namna ya kuzisimamia hizi sheria, kwa sababu tumeona namna gani serikali inavyokua inafanya mambo yake bila ya kufuata hizi sheria za manunuzi.

Kwenye ripoti ile ya Kamati Teule Mhe. Naibu Spika, tumeonesha mule, ni namna gani sheria za manunuzi zilivyo kiukwa sio suala la kwamba labda serikali imenunua tu au imeuza hapana. Tulichokua tunakizungumza pale ni sheria namna zilivyokiukwa. Sasa kama serikali imeshindwa kufuata zile sheria ambazo sisi tunaziweka, basi ni

vyema kwa mambo kama yale sasa yawe yanaletwa kwenye Baraza hili, ili tuweze kuyaona na kuchangia michango yetu pale, aidha kamati au Baraza. Lakini mimi nafikiri ni vyema ingekuwa inapita kwenye kamati husika.

Kwa mfano, kwenye masuala haya ya mauzo hasa ya majengo ya serikali, au ile mikataba mikubwa kabisa, ambapo hata wenzetu wanafanya, bungeni pale nafikiri wanafanya hivyo. Mikataba ya madeni na mikataba mikubwa inapelekwa bungeni na kamati husika zinakaa na kuangalia ile mikataba na kutoa ushauri wake. Kwa hivyo, serikali inapokwenda kufanya, inakuwa lile Baraza au Bunge lenyewe tayari limeshaona ile mikataba na limeridhia, inaondosha hata ile migongano ya namna hii.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alikuwa mkali kidogo akasema hili ni zito. Mimi namuambia hili sio zito, kwa sababu wenzetu tayari wanafanya na nyinyi kama serikali, tumeona mule katika ripoti ya Kamati Teule mmeshindwa. Sheria zipo, lakini kuzifuata mmekuwa wagumu, sasa kama ni wagumu Baraza kama chombo cha wananchi, chombo cha kutunga sheria cha kusimamia ile serikali. Kwa hivyo, mimi ningeshauri mikataba ile ya namna ile iletwe katika Baraza ili kamati za Baraza ziweze kupitia, hasa kwenye mikataba hii ya manunuzi na mikataba ya kuuza kwenye maeneo hayo ya majengo. Suala hili ilikuwa kidogo nataka nilisisitize ili ikiwezekana Mhe. Naibu Spika, basi nimuombe sana Mhe. Waziri ambaye anashughulika na Baraza asaidie hili ikiwezekana liletwe humu ili mikataba hii iwe inapitiwa na Baraza au kamati za Baraza kwa ajili ya kupata baraka za wananchi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele nirudi pale pale kwenye ile hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais. Wakati Mhe. Mwanasheria Mkuu alipokuwa akitoa ufafanuzi, kulikuwa kuna hoja ambayo tulikuwa tunazungumza, na wajumbe wengi walichangia hoja ya kwamba kwa nini ile ripoti ya kamati teule mpaka leo serikali haijatoa utekelezaji wa hatua ambazo ilikuwa imeagizwa na Baraza. Mhe. Waziri alitoa ufafanuzi mrefu sana, katika maelezo yake alizungumzia pia namna kamati teule ilivyofanyakazi kwa muda mrefu sana. Kwa hivyo, tusishangae kwamba wao tumewapa miezi mitatu haijatimia na hivi sasa ni miezi miwili tu kufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nataka nitowe ufafanuzi kidogo kwamba alipozungumza kuwa kamati teule ilifanyakazi miezi minane. Mimi naona sio sahihi. Ukiangalia ile ripoti ya kamati teule katika ukurasa wa nne, kwenye utaratibu wa kazi za kamati. Naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika,

“Kamati teule baada ya kuundwa na kukabidhiwa hadidu rejea, ilipangiwa kufanya kazi kwa wiki sita, sio miezi minane. Ilifanyakazi kwa wiki sita katika miezi tofauti na kwa kupata ridhaa ya Spika, wajumbe wa kamati hii walijitolea kufanyakazi hii kwa siku zisizopungua 10 bila ya malipo yoyote, lakini kwa kujali umuhimu wa kazi hii, walijitolea kuikamilisha”.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia hapa ripoti hii imeandikwa kwamba imefanyakazi kamati ile kwa wiki sita, lakini kuna siku 10 imefanyakazi kwa kujitolea ili kuonesha umuhimu wa namna gani wanavyoisimamia ile serikali. Sasa nikiendelea mbele hapo anasema,

“Kwa siku kadhaa kamati ilifanyakazi hadi saa 5:00 za usiku, kwa mnasaba huu huu wa kuikamilisha kazi hii, kama ilivyofanya hivi hata katika siku za mapumziko. Kamati pia ilimepata muda wa kuiandaa ripoti yake na kuipitia pamoja katika utaratibu ilioona inafaa na matokeo yake kufanikisha kwa pamoja ripoti hii kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 119(1) ya kanuni za Baraza”.

Hapa nilikuwa nataka kutoa ufafanuzi huu Mhe. Naibu Spika, kumsaidia Mhe. Mwanasheria Mkuu pale kidogo kwa yale maelezo ambayo aliyaeleza kwamba kamati ilifanya kazi kwa miezi minane, lakini ripoti inasema kamati ilifanyakazi kwa wiki sita. Kwa hivyo, nilikuwa nataka nitowe ufafanuzi huu ili tuweke sawa na Hansard iweke kumbukumbu vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nije kwenye suala la uwajibikaji wa serikali. Kuna Mhe. Mjumbe mmoja alipokuwa akichangia hapa asubuhi alisema, uwajibikaji hasa kwa baadhi ya watendaji wetu umekuwa ni mdogo kweli. Serikali inaonekana haiwajibiki ipasavyo kwa wananchi, hili mimi nakubaliana nalo, kuna matatizo Mhe. Naibu Spika. Ukiangalia hata hii hoja ambayo aliijenga Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba kamati imechukua miezi minane na huku ripoti inasema wiki sita, lakini ukiitizama utaiona kama ni miezi minane, maana yake imefanyakazi wiki sita ndani ya ile miezi minane, hii yote inatokana na ule urasimu uliokuwepo serikali, wa kupata hata zile fedha za posho kwa ajili ya kamati ile.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ukiangalia kwenye katiba hapa katika kifungu cha 9 cha katiba yetu ya Zanzibar kwenye serikali na watu, naomba ninukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 9(1)

"Zanzibar itakuwa ni nchi ya kidemokrasia na haki za kijamii"

Kwa hivyo, hapa inaelezwa rasmi kwamba mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa serikali kufuatana na katiba utatoka kwa wananchi wenyewe. Nikiendelea mbele kwenye 9(2) (b) kinasema,

Kifungu cha 9(2) (b)

"Usalama na hali nzuri kwa wananchi itakuwa ndio lengo kubwa la serikali".

Nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, nisogee kwenye kifungu cha 10, katika malengo ya kisiasa. Mhe. Naibu Spika, usione nakwenda sana, najaribu kunukuu hivi, halafu nitowe maelezo yangu. Kwenye kifungu cha 10 cha katiba kinasema,

Kifungu cha 10

"Kwa madhumuni ya kuendeleza umoja na maendeleo ya watu na ustawi wa jamii katika nchi, itakuwa ni wajibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar,

(a) Kutoa huduma za kutosha kwa ajili ya kuendeleza watu katika njia za mtu kuamuru kwenda atakapo na utoaji huduma kwa watu wote, na kutoa haki zote za kuishi kwa Mzanzibari sehemu zote za Zanzibar".

Nikisogea pale kwenye kifungu kidogo cha (b) kinasema,

(b) "Kuondosha kabisa vitendo vya rushwa na utumiaji mbaya wa cheo dhidi ya umma kwa wale wote walio na madaraka".

Mhe. Naibu Spika, nisogee tena mbele kidogo katika kifungu kidogo cha (f) kinasema,

(f) "kuhakikisha kwamba zipo huduma za kutosha za kiafya kwa watu wote, zipo rursa sawa na za kutosha za kielimu katika madaraja yote na kwamba utamaduni wa Zanzibar unalindwa, unaimarishwa na kuendelezwa".

Mhe. Naibu Spika, nimalizie katika ibara hii kwenye kifungu kidogo cha (h) kinasema,

(h) "vyeo vyote vya madaraka ni dhamana na vipo kwa faida na manufaa ya umma, na wale wote walio na madaraka watawajibika ama moja kwa moja kwa umma, au kupitia kwa vyombo vya uwakilishi", mwisho wa kunukuu.

Mhe. Naibu Spika, nimeyasema haya ili tuone ule uwajibikaji wa serikali kwa wananchi. Ukiangalia ripoti hii ya kamati teule ambayo iliwasilishwa, namna ambavyo tumeona serikali au watendaji ambao wako chini ya dhamana ile ya serikali wanavyofanya mambo yao, kumekuwa hakuna uwajibikaji. Kila mmoja, baadhi yao sio wote. Maana naanza kuoneshwa vidole, sio wote kuna baadhi ya watendaji wanafanya wanavyotaka Mhe. Naibu Spika, hawafuati zile sheria ambazo tumeziweka. Lakini huku ukiangalia katiba inawaambia namna gani wanavyotakiwa wawe, hata kile cheo kwamba ni dhamana. Asione mtu kapewe nafasi, basi akaone ile nafasi kama ni ya kwake, anakwenda mwananchi pale tena hana lake, mtendaji anafanya anavyotaka. Ndio maana hata kwenye hii ripoti ya kamati teule ukiitizama imeelezwa haya yanavyofanyika huku.

Lakini nilisikitika sana nilipomsikia rafiki yangu Mhe. Mwanasheria Mkuu anavyoitetea kweli kweli hoja ya kwa nini hawajatoa ripoti. Mimi nilifikiria serikali yenye kuwajibika kwa watu, ingetuambia basi hata kwa yale mawili au matatu ambayo imeshayafanyia kazi, kisha baadae ikatuletea ile ripoti kamili. Maana yake hapa wananchi ndio wanahoji, mmefanya nini katika yale ambayo yanalalamikiwa. Kwa hivyo, nafikiria ingekuwa ni vyema yakawa yameelezwa kidogo, kwamba katika haya kuna hili na hili, kama mnavyokuja kutuambia hapa. Huwa tunauliza maswali hapa. Unaambiwa serikali imeshajipanga au iko mbioni, inafanya hivi na hivi. Kama kuna ujenzi wa barabara, haa! Tumeshapata mkandarasi, sijui mkandarasi yuko hivi, lakini mkataba bado hatujafunga huwa mnatueleza.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, suala hili mimi nafikiria ingekuwa vizuri sana Mhe. Waziri ungekuja hapa ukatuambia basi hata yale ambayo mmeanzia au hakuna hata moja. Mimi suala hili linanipa shaka kidogo. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri utakapokuja hapa, hebu tueleze kidogo juu ya mambo haya, bado hatujapata majibu mazuri, au hatukuridhika na yale majibu ambayo Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo aliyatolea ufafanuzi. Sasa ningekuomba, kwa vile wizara ndio inayohusika na Baraza na lile lilikuwa ni agizo la Baraza, hebu uje utueleze kidogo.

Mhe. Naibu Spika, hata (a),(b),(c) hakuna, tusubiri tu, wananchi wana hamu ya kutaka kujua, basi tuoneshe kwamba kweli serikali imeanza kuchukua hatua hii na hii, halafu mtatuletea hiyo ripoti itakapokuwa imekamilika, mimi nafikiria hili lingekuwa zuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niendelee mbele nije kwenye kitabu cha Mhe. Waziri kwenye ukurasa wa 15, nije kwenye maafa. Mhe. Waziri ametueleza hapa juu ya masikitiko yaliyotokezea tarehe 10/09/2011 jinsi nchi yetu ilivyopata mtikisiko baada ya kutokea kuzama kwa meli ya *MV. Spice Islander*. Tukio hili ambalo liliuwa takriban watu 1,529 kwa mujibu wa maelezo ambayo Mhe. Waziri ametuandikia, ingawa hadithi nyengine zinasema ni zaidi ya hapo, kwa sababu na wao hawana takwimu vizuri kwa sababu wale watu hawakuwa wameorodheshwa wote.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niipongeze serikali kwa hatua ambazo ilichukua za kuweza kusaidia wale ambao iliweza kuwaokoa, na hatua iliyochukua baada ya kuwaokoa, kufanya mazishi kwa ile miili ambayo ilipatikana na hatua ya mwisho ya kulipa fidia. Lakini mimi bado nina masikitiko sana juu ya uwajibikaji wa kisiasa ambao hapa mimi sikuuona. Hii ni serikali ya watu na imechaguliwa na watu, hawa waliokufa hapa ni watu ambao ni zaidi ya 1,000 wamekufa. Sasa serikali ina hofu gani kuonesha uwajibikaji katika hili wa kisiasa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano yuko hapa. Mimi nilitegemea kwa tukio kama hili la kufa watu zaidi ya 1,500, basi Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano angesema mimi nawajibika kisiasa, akae pembeni aseme hii ndio siasa, nawajibika kisiasa ili kuonesha kwamba ana huzuni na masikitiko makubwa juu ya vifo vile, kwa sababu tukiangalia hata chanzo kinavyoelezwa juu ya ile ripoti, inasema chanzo ni uzembe na uzembe ule ulisababishwa na watendaji ambao wako kwenye wizara yake, na ushaidi upo maana yake hivi sasa kesi ndio iko mahakamani. Kwa nini yeye Mhe. Waziri hakuwajibika kwenye hili, akaonesha ule uwajibikaji wa kisiasa, kwamba hapana na mimi sasa nakaa pembeni kuonesha heshima kwa wananchi wa Zanzibar na masikitiko yangu kwamba hili tukio lililotokezea, sikuridhika na utendaji wa watendaji wangu nawajibika. Tumeshaona mifano mingi ya mambo kama haya.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ali Hassan Mwinyi alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani tu, wafungwa walitoroka jela, basi aliwajibika yeye waziri, siowamekufa hapana, walitoroka jela basi waziri akajiuzulu kabisa. Lakini yeye waziri hakuwepo kule sijui ndio Tabora walikotoroka huko, hapana ni watendaji wake, lakini alionesha uwajibikaji wa kisiasa. Akasema kwa kuwa kosa limefanywa na watendaji wangu, ndio nimelifanya mimi maana mimi ndio dhamana wa wizara hii. Sasa leo tunamshangaa sana Mhe. Waziri kesho na keshokutwa anakuja na bajeti yake anatuomba tumuidhinishie fedha, itakuwa ni ngumu kwa waziri kama huyu kuja kumuidhinishia fedha, maana yake juzi tu ndio tumeuwa ndugu zetu 1,500 hawa ndio walipa kodi wenyewe, sisi walipa kodi hawa waliokufa ni ndugu zetu, wajomba zetu na shangazi zetu. Kwa nini wewe Mhe. Waziri hutuoneshi uwajibikaji. Hatusemi wizara ifutwe hapana, waziri angeonesha uwajibikaji yeye, akachaguliwa waziri mwengine akaja kutuomba fedha.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nakuomba suala hili kwenye bajeti inayokuja kwa kweli tutakuwa wakali kweli, uzembe huu ambao umefanyika hatutouvumilia, wala hatutompitishia mtu bajeti yake mwenye matatizo yake. Kama kuna waziri ana matatizo, mtendaji ana matatizo kwa hivyo hapa asituletee bajeti. Bajeti ikija Mhe. Makamu wa Pili tunakuomba sana suala hili. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ni mwenzangu sana, rafiki yangu, mzee wangu na amenilea. Lakini napenda nimwambie ukweli kabisa, tutakuwa wagumu kweli kweli, hatutokubali uzembe ambao umefanyika halafu sisi tukawa tunaidhinisha matumizi, hapana. Hapa hatutoidhinisha matumizi kwenda kumkabidhi mtu ambaye tayari tuna matatizo naye. Kuna wengine wameshasemwa kwenye maripoti na kama hivyo ninavyokuambia waziri anashindwa hata kufanya uwajibikaji wa kisiasa kwenye watu 1,500, unasubiri mpaka wafe wangapi ndio useme, aah! Hawa sasa wengi ndio nakaa pembeni. Hebu tuwe tunawajibika kweli, ndio niliposema uwajibikaji wa serikali umekuwa mdogo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwenye kitabu chake ameandika kuna kifungu cha 32 kinasema:

> “uamuzi wa serikali kuwa fedha hizo zote zitolewe kwa waathirika wa maafa hayo na warithi wa abiria waliofariki wapatiwe shilingi 550,000 kwa kila aliyepoteza maisha katika ajali hiyo. Misaada mingine ya vyakula, viligaiwa katika vituo vya kulelea watoto yatima na wazee wasiojiweza kwa Unguja na Pemba”.

Hapa hoja yangu Mhe. Waziri nataka utakapokuja hebu tupe mchanganuo kidogo wa hivi vyakula ulivyovigawa. Ni wapi na ni vituo gani ulivyovigawa, nani uliyempa na idadi gani. Nafikiri Mhe. Waziri utakapokuja utatupa ufafanuzi wa suala hili.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea mbele katika ukurasa wa 21 wa hotuba hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, bado dakika 5.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Naibu Spika, nakubali nivumilie kidogo.

Sasa naomba niende kwenye Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Tumeambiwa hapa kwamba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais amefanya safari nyingi hapa ndani na nje ya nchi.

Kwa hivyo, mimi kidogo naomba nipatiwe ufafanuzi kupitia kwako Mhe. Naibu Spika wakati atakapokuja Mhe. Waziri anisasidie namna ya safari za Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alituahidi hapa kwamba atakapokuwa na baadhi ya waheshimiwa atakuwa anasafiri nao, yaani uje utupe ile idadi ya wale Waheshimiwa Wajumbe aliosafiri nao kwa ajili ya kwenda kujifunza, unipe idadi na nani walikwenda huko. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa niende kwenye ukurasa wa 12 kuhusu migogoro ya ardhi. Kwa kweli migogoro ya ardhi imekuwa ni tatizo sugu ambalo inaonekana serikali imeshindwa kulitatua, kwa sababu kila anapokuja Mhe. Makamo wa Pili wa Rais analieleza hili, yaani kwenye Hotuba zake za Kufunga Vikao hapa huwa analieleza hili, lakini utekelezaji wake umekuwa ni kikwazo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, migogoro hii imekuwa inasumbua sana jamii. Kwa mfano, kwetu Kaskazini Unguja, Pemba, yaani hakuna sehemu ambayo unakwenda hakuna migogoro ya ardhi. Kutokana na hali hiyo, nadhani serikali imeshindwa kuitatua migogoro hii, na inashindwa kwa sababu kama utakumbuka vizuri migogoro hii ambayo tumeambiwa inarejeshwa kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya ndio waishughulikie. *(Makofi)*

Lakini ukiutizama huo mfumo wenyewe, hao wanaotajwa baadhi yao ndio migogoro yenyewe, yaani Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya wengine masheha ndio chanzo cha hiyo migogoro. Sasa kama hawa ndio migogoro unawapelekea wakaitatue migogoro wataitatua vipi na wala hawawezi kuitatua. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kutokana na kilio cha wananchi kuwa kikubwa juu ya migogoro hii, mimi nina wazo Mhe. Naibu Spika kupitia Baraza lako tukufu kwamba tutumie kanuni ile ya Baraza ya 120 kuundwe Kamati Teule kwa ajili ya Migogoro ya Ardhi, ili tuweze kuwatendea haki wananchi wetu, kwa sababu kwa kuiachia serikali tu, kwa kweli serikali haiwezi kuja kutuambia kwamba jamani tumeshindwa na sasa kaitatueni. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ninachoomba kupitia Baraza lako tukufu kwamba sasa iko haja, tena ni vyema tukatumia Kanuni ya Baraza la Wawakilishi ya 120 tukaunda Kamati Teule juu ya Migogoro ya Ardhi, ili Baraza lako hili sasa liende na kuitatua migogoro ile na wananchi wetu waweze kuishi kwa amani na furaha kabisa. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, Mhe. Naibu Spika naomba kukaa kitako. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, na mimi nataka nikushukuru sana jioni hii kwa kunipatia nafasi hii angalau niseme machache katika Hotuba hii ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, nianze kwenye ukurasa wa 5.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu wengi wamezungumza habari ya Muungano, wamezungumza kwa sababu Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ina kazi kubwa ya kuratibu masuala ya Muungano, na ndani ya kitabu humu yameandikwa, kwa hivyo hatuna budi tutoe michango kidogo kuhusu Muungano.

Mhe. Naibu Spika, Muungano wetu sasa umetimiza miaka 48, kwa kweli ni jambo la kupongeza sana Muungano kwa kutimia miaka 48. Lakini kwa bahati mbaya ndani ya miaka 48 hii Muungano wetu umekuwa na dosari nyingi, wengine wanaita dosari au changamoto ama kero almuradi una matatizo. Mhe. Naibu Spika, sitaki nitaje mengi lakini matatizo yote nimeyakusanya kwenye makundi matatu au athari yake imejitokeza sehemu tatu.

Kwanza kero hizo zimetupotezea *sovereignty* yetu Wazanzibari. Vile vile kero hizo zimesababisha uchumi wa Zanzibar pamoja na hali ya Wazanzibari kudumaa sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba niende mbali zaidi au nianze mwanzo sana kusema moja katika kero kubwa hata huu uhalali wa Muungano ni wa mashaka. Kwa bahati mbaya sana juhudi nyingi zimefanywa za kujaribu kutatua hizi kero, lakini inaonekana pande zetu mbili za Muungano zimegonga mwamba.

Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu nieleze kidogo Kuhusu huu uhalali niliosema kwamba Muungano wetu uhalali wake ni wa kusuasua. Kwanza katika Mkataba wa Muungano tunahadithiwa, maana tunautafuta na wala hatuuoni mpaka leo, lakini tunahadithiwa mule kwamba baada ya Muungano ule kufanyika Mkataba wa Muungano ulizitaka kila upande katika pande zile ziende kwenye Bunge, watunge Sheria na Bunge liridhie Muungano.

Mhe. Naibu Spika, watafiti wa kisheria wanatuambia Bunge la Tanganyika hatimaye lilitunga Sheria ya Kuridhia Muungano, lakini mpaka leo imeshindikana kupata *document* inayosema kama Baraza la Mapinduzi kwa wakati ule ndio ilikuwa Bunge, yaani likitunga sheria.

Document ya kuthibitisha kama Baraza la Mapinduzi lilipitisha Sheria ya Kuridhia Muungano mpaka leo *document* hiyo haijapatikana, na inasadikiwa kwamba Baraza la Mapinduzi halikuridhia Muungano. Sasa hii ni dalili moja tosha ya kusema kama Muungano wetu uhalali wake una mashaka. *(Makofi)*

Mkataba wa Muungano pia ulidai mwaka mmoja baada ya kuunganisha Muungano liundwe Bunge la Katiba, ili kuandaa Katiba ya Muungano, Mhe. Naibu Spika mwaka ulipita na Bunge hilo halikuundwa, sasa hiyo ni dalili nyengine kwamba Muungano huu uhalali wake una matatizo. Hatimaye baada ya miaka mingi kupita Bunge la Katiba, Mhe. Mwalimu Julius Nyerere aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wakati huo, alilitangaza Bunge lile la kawaida kuwa liwe ndio Bunge la Katiba.

Lakini kasoro kubwa lililokuwemo kwenye Bunge lile hakukuwa na uwiano wa wajumbe kati ya Wazanzibari na wenzetu upande wa pili, wanasema *ratio* ilikuwa Wazanzibari walikuwemo 40 au 42 wakati wenzetu walikuwemo mia mbili na zaidi, na hapo usawa hauwezi kupatikana. Kwa hivyo, hii ni dosari ya pili ambayo inatia mashaka kuwa kuna uhalali wa Muungano.

Mhe. Naibu Spika, hatimaye hata hiyo Katiba haikutungwa na kilichofanyika hilo Bunge ambalo lina dosari nalo liliitangaza Katiba ya Tanganyika kuwa ndio Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo, dosari hizi Mhe. Naibu Spika mimi binafsi nasema Muungano huu kwanza ule uhalali wake ni wa mashaka kwa lugha nyepesi zaidi tunasema si halali. *(Makofi)*

Sasa huku si halali na halafu ukawa na kero nyingi juhudi za kutatua kero zikakwama. Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari kwa sababu wao ndio waliopata hasara kubwa sana katika Muungano, wamepaza sauti zao hawautaki tena na wala mimi siwalaumu. Mhe. Naibu Spika, kuna *quotation* ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Mwalimu Julius Nyerere alisema kwamba "Siku Wazanzibari watakapoamua kuukataa Muungano, sitawapiga mabomu". *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi huwakosa sana wenzangu wale wanaojaribu kuwalaani Wazanzibari kuwaona si watu na wamekosea sana kukataa Muungano na wala tusiwalaumu. *(Makofi)*

Vile vile nataka niseme Mhe. Naibu Spika, kwamba mimi nipo hapa kwa kuchaguliwa na Wazanzibari, nadhani kila mmoja wetu hapa asingefika kama hajachaguliwa na Wazanzibari, kwa sababu Wazanzibari ndio waajiri wetu, pia Wazanzibari ndio wenye maamuzi ya nchi hii na sisi tunakuja hapa kwa ajili ya kuwakilisha mawazo yao, sisi Wajumbe, Waheshimiwa Mawaziri ni hivyo hivyo na hata Mhe. Rais pia naye amechaguliwa na Wazanzibari. Kwa hivyo, tunapaswa sana kuheshimu mawazo ya Wazanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka nitamke wazi kwamba watu wangu walionichagua wakiamua kuwa hawataki Muungano, basi Mhe. Naibu Spika hilo nitalisimamia kwa nguvu zangu zote na wala sitorudi nyuma kabisa, kwa sababu nikifanya vyengine hivi kesho watanichagua tena wale, hawatanichagua na mimi ni waajiri wangu na nafasi hii bado ninaitaka, na wala siwezi kufanya mas-hara katika hilo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wakiniambia hawautaki basi nitasimamia maamuzi yao, na kama wataniambia wanautaka pia nitasimama na maamuzi yao, na wala sitokwenda kinyume na maamuzi ya wapiga kura wangu. *(Makofi)*

Kwa bahati nzuri sana tumepata fursa hii ya kujadili mchakato wa Katiba. Kwa kweli ni nafasi moja muhimu sana, ambayo hili dukuduku la Wazanzibari kupitia fursa hii basi linaweza kupata jawabu. Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii niwaombe sana Wazanzibari wenzangu, kwanza wajitokeze kwa wingi kwenda mbele ya Tume ya Jaji Warioba, kwa ajili ya kwenda kutoa maoni yao. Vile vile ni muhimu kutafuta elimu kidogo, yaani wawe na ufahamu wa kujua namna ya kutoa maoni. Tume ya Jaji Warioba tunasikia ina hadidu rejea, kwa hivyo ni muhimu sana watu wetu wazijue hizo hadidu rejea na wazitumie hizo, ili kuweza kutoa maoni yao.

Mhe. Naibu Spika, nadhani ile sheria ambayo imeweka mipaka kwa bahati mbaya sana sikuwepo wakati walipokuwa wakiitunga kule Bungeni. Lakini kama ningekuwepo basi ningeipinga kwa nguvu zangu zote, na kama Bunge lingeipitisha labda ningeamua maamuzi hata ya kwenda Mahakamani, kwa sababu tunajadili Katiba na Muungano huu umo ndani ya Katiba.

Sasa unapofika pahala na kusema hili jadili na lile usijadili bado umebinya demokrasia. Kwa hiyo, yule mwenye mawazo ambayo wewe umemwambia asijadili akayatoe wapi. Mhe. Naibu Spika, hapa nawaomba Wazanzibari wenzangu wawe na hadhari kubwa sana. Tumesikia Hotuba ya Mwenyekiti wa Tume ya Kukusanya Maoni ya Katiba Mpya, kwamba hata wale watakaosema hawataki Muungano maoni yao atayachukua, ndio mtu hata ukimtukana ata-*record* kwamba umemtukana, lakini je atalifanyia kazi tusi lako. *(Makofi)*

Hofu yangu Mhe. Naibu Spika, kwamba Wazanzibari wasije wakaingia kwenye mtego huu, kwa sababu kila mwenye kusimama pale mimi sitaki Muungano anaweza kuchukua Mhe. Jaji Warioba, lakini kwa sababu hili halimo kwenye hadidu rejea halitafanyiwa kazi, na hiyo ndiyo hofu yangu. Vyenginevyo watoe kauli nyengine ya kututhibitishia kwamba na haya yatafanyiwa kazi sawa na maoni mengine. Kwa msingi huo basi akubali kwamba ile sheria ina dosari. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuwaomba Wazanzibari wenzangu, kwamba amani hii na utulivu tulionao ni muhimu sana hasa wakati huu wa mchakato wa Katiba, tusipoangalia sana tunaweza tukafeli. Kwa hivyo, niungane na Mhe. Waziri kwa niaba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alisema kama nyumba za ibada hazihusiki na mchakato wa Katiba, kwa hiyo tusizishirikishe na tuziheshimu nyumba za ibada.
Mhe. Naibu Spika, kule Mahonda juzi kulitokea tukio baya na mimi naomba nitumie fursa hii kuwatanabahisha sana askari. Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa Askari Polisi, na wakati nilipokuwa nikichukua kozi kuna ule mchaka mchaka kule Moshi, lakini tulikuwa tunapiga mchaka mchaka na nikichoka kuna sehemu ya Msikiti hutoka kwenye kundi tunajitia Msikitini mule. *(Makofi)*

Sasa nyuma yetu kuna Askari wa MP, yaani MP akikuona umetoka kwenye kundi anakufukuza na ukiingia Msikitini yeye haingii, anasema huko siingii na yule ni Mkiristo na anauheshimu Msikiti kweli, na ikawa ndio mtindo wangu mimi, nikichoka kwenye mchaka mchaka basi nakimbilia Msikitini na wao wanarudi.

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana, na kwa kweli hili naomba niwausie sana askari, kwa sababu wao ni Waislamu, lakini juzi walichokifanya Mahonda hakikua sahihi, maana yake tukisema shilingi lazima tuitazame pande zote mbili, kwani tumekemea sana waliovunja makanisa, lakini na askari waliouvunjia heshima Msikiti lazima tuwakemee. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, waingia waislamu na sijui waingia kwenda kusali au kwa ajili ya kwenda kujisaidia ama kujihami, lakini kuna Msikiti pale, wangeweza kuwasubiri pale na wangetoka tu. Lakini walichokifanya waliingia mule na mabuti yao na kwenda kufanya fujo na kupiga mabomu ndani ya Msikiti, na kuvunja kata za Msikiti na kupata magongo na kupigia watu mule ndani.

Hivi jamaa raia wa nchi hii anapo pahala pa kukimbilia usimpate kweli mpaka uingie ndani ya Msikiti na kufanya fujo. Sisi Waislamu kuingia Msikitini na viatu ni haramu, yaani ni kosa kubwa. Sasa kama wameagizwa askari wafanye vile basi wajue kwamba wanavunja sheria, na kuivunjia heshima Dini ya Mwenyezi Mungu na ile ni Nyumba ya Mwenyezi Mungu.

Mhe. Naibu Spika, sidhani kama kuna mtu au kiongozi wao kama *RPC* au *IGP* sifikiri kama amewapa amri wakaingie Msikitini. Lakini kama amewapa amri basi sisi tutakufa na kufufuliwa na kule akhera tutaulizwa, sasa askari mdogo akeshakuchomwa moto atamwambia Mwenyezi Mungu mimi aliyenipa amri ni *RPC*, Mwenyezi Mungu atamwambia wewe na *RPC* nyote ni humo humo na wala halitamuombea lile.

Kwa hivyo, naomba sana ikitokea kesi kama ile mara nyengine basi askari ni afadhali wawazungumze pale Msikitini na wala hawatalala mule na hatimaye watatoka, na watawakamata kama ni haja yao ni kuwakamata. Lakini wasirudie kitendo hicho kwa sababu ni hatari sana, na wengine waliapiza na Waislamu walisali Itikafu na kusema Mwenyezi Mungu awape matende waliofanya kitendo hicho na wala mimi siwaapizi, lakini wamefanya jambo baya. Mhe. Naibu Spika, naomba hilo nilimalizie hapo.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali ukurasa wa 30. Mhe. Naibu Spika, katika Idara hii naomba nilizungumzie suala moja tu la *TASAF* imetekeleza takribani kila jimbo. Lakini kwa uzoefu nilioupata pale jimboni pangu Mhe. Naibu Spika, miradi hii ina usiri mkubwa, yaani inawezekana mradi au fedha za *TASAF* zipo, lakini taarifa wananchi hawana.

Sasa wanaoratibu kwa karibu sana ni masheha na huchagua jamaa zake, na kuwapenyezea kwamba kuna fedha kidogo hebu jikusanyeni nadhani na hata Mhe. Waziri ananiunga mkono, kwa sababu limetokea jimboni kwangu. Kwa kweli miradi imekuja na watu wakaorodheshwa na kupewa vyombo vya kuvulia na wengine ndani ya mji ule hawana habari, na tatizo hili ni la masheha na kwamba hawazitumii vizuri fursa zao.

Vile vile nilipokuwa nikisoma na kufanya *reference* kwenye kitabu cha Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kile cha mwaka jana, nimekuta kuna mradi mmoja jimboni kwangu wa fedha nyingi sana shilingi 35,995,000/=. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwanza mradi huu nao umekwenda pale ambapo tayari wameshapata mashua mbili. Lakini na hapa ndipo kwenye hoja yangu, kwamba ule mradi ni wa fedha nyingi na nimekagua ni mradi wa upandaji miti, nimejaribu kulikagua lile shamba lililopandwa na kufanya tathmini. Kwa kweli mradi wa shilingi milioni 35 Mhe. Naibu Spika haitimii hata shilingi milioni 2 ya thamani ya lile shamba. *(Makofi)*

Kwa hivyo, inaonekana hapa na kwa kupitia huu usiri wa sheha, fedha zile zinapigwa kuni, Mhe. Waziri fedha zinapigwa kuni, watu wanaibua miradi na kutiliwa fedha kinyemela wakazila na kuweka sababu kwamba tumefanya hapa. Mhe. Naibu Spika, naomba sana likakaguliwe Shamba la Mivinje Kilindi, hata thamani ya shilingi milioni mbili halifiki, na hapa ndani ya kitabu nimekuta shilingi milioni 35. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, mimi nina pendekezo kwamba Miradi ya *TASAF* ipitie kwenye Kamati ya maendeleo ya Jimbo, ili watu wote wa kona zote za jimbo wapate taarifa kama kuna Mradi wa *TASAF*, kuna fedha kiasi kadhaa na maelekezo haya na yale na watu wajikusanye bila ya kuwa na usiri mkubwa. Mhe. Naibu Spika, pia nilikuwa naomba sana Ofisi ya *CAG* iwe karibu sana na hii Miradi ya *TASAF*, kwa sababu tunataka kupata *value for money* katika fedha hizi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumzie Baraza la Wawakilishi kwa haraka tena kidogo sana kwenye ukurasa wa 50 ndipo lilipotajwa Baraza hili. Mhe. Naibu Spika, Baraza la Wawakilishi ni chombo muhimu sana katika nchi hii, kwa sababu ni chombo chenye majukumu mengi na miongoni mwa majukumu yake ni kuisimamia serikali.

Sasa kwa bahati mbaya au nzuri Baraza la Wawakilishi mara nyengine huwa kunatokezewa kazi ambazo hazikutazamiwa zinatokea. Kwa mfano, kama hizi Kamati Teule na kwa bahati nimewahi kuwa Mjumbe kwenye kamati hizi mara mbili, kama vile Kamati ya *PAC* na Kamati Teule ya Kuchunguza Baraza la Mji mote muwili ni Mjumbe.

Lakini nimegundua mapungufu makubwa ya utendaji wa hizi kamati, kwamba haziwezeshwi Baraza halina fedha, tukamuuliza Katibu mbona mambo yanakwenda hivi na hakuna kitu muhimu sana kama hizi Kamati Teule, kwa sababu zinaibua mambo na faida yake tutaiona baadae na wala mimi siko jikoni. Lakini wadadisi wanasema kwamba tokea kuzuka huu mtindo wa Kamati Teule, Mapato ya Serikali yanaonekana kuongezeka tena kwa kiwango kizuri sana na wala sitaki nitaje *figure*, lakini yanaongezeka kwa kiwango kizuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hii ni kuonesha kwamba Baraza la Wawakilishi kama litafanya wajibu wake wa kuisimamia serikali ipasavyo, basi huenda siku moja matatizo haya ya mapungufu ya bajeti kwa kiwango kikubwa yakapungua sana. *(Makofi)*

Tatizo Mhe. Naibu Spika, kwamba Baraza halina fedha za kufanyia kazi, na hii nataka niitafsiri kwamba inafanywa kwa makusudi, ili Baraza hili lisiweze kufanya kazi zake.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nikiangalia Ripoti ya Mhe. Makamo wa Pili, fungu lililoidhinishwa na Baraza mwaka uliopita lina mapungufu karibu shilingi bilioni 2,145 hazikupatikana mpaka sasa labda zimo kwenye kipindi hiki cha Aprili – Juni, lakini Baraza limepata mapungufu makubwa kazi haziendi.

Sisi kama *PAC* sasa hivi tuna vitabu vitatu vya *CAG* tulipaswa kuvifanyia kazi mwaka huu, vimetushinda kwa sababu ya pesa. Nilikuwa naomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais hili suala alione na ikiwezekana ule mfuko wetu wa Baraza sasa wakati umeshafika, taratibu zikamilike, tuwe nao wenyewe.

Jambo la mwisho niligusie kwa ufupi sana. Mhe. Naibu Spika, kuna Tume ya Mipango ya Serikali ambayo inapanga mipango mingi ya serikali. Miongoni mwa mipango inayopanga ni miradi ya maendeleo. Katika lile huwa kuna *taminoloji* wanayoitumia wanasema wanaibua vipaumbele kwa ajili ya maendeleo. Tatizo lililokuwepo vipaumbele ambavyo wanaviibua wao mara nyengine vinakuwa si vipaumbele kwa wale wanaofanyiwa, yaani wananchi wenyewe. Pengine wananchi wana kero nyengine lakini Tume ya Mipango imeona kipaumbele chengine. Manung'uniko yanakuwa hayeshi na manung'uniko yote yanatuangukia sisi Wawakilishi. Unaweza ukajua serikali imefanya hili na hili lakini ukaambiwa hili ni muhimu zaidi.

Sasa nilikuwa naomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kama Mtendaji Mkuu wa Serikali, basi aielekeze ile Tume ujaribu kugema kidogo mawazo ya wananchi. Wananchi wanahitaji nini ndio hicho kiwe kipaumbele. Vipaumbele visianze juu vikateremka chini, wananchi ikawa wanafanyiwa tu. Wangetakiwa na wao mawazo yao.

La mwisho, nimegundua mimi katika maendeleo ya kijamii, Mhe. Naibu Spika, hakuna uwiano katika jamii. Kwa mfano unaweza ukakuta watu wa Kijiji fulani wamepata labda barabara na umeme, wengine wakawa wamepata umeme na maji, lakini kuna wengine hawana umeme, hawana maji, hawana barabara hawana skuli yaani kama kwamba wao si Wazanzibari.

Nilikuwa naomba sana hebu tufanye utafiti ni wapi ambapo wenzetu hawajapata chochote angalau wafanyiwe japo mawili na wao. Mimi nina mfano mzuri na napenda kuutaja na nitautaja tena na tena ndani ya bajeti ya mwaka huu. Kuna kijiji kinaitwa Ngomeni. Ngomeni Mhe. Naibu Spika, kwanza ukizungumza karafuu kwa kule Pemba sasa hivi pahali ambapo panatoa karafuu kwa wingi ni ngomeni. Lakini Ngomeni haina barabara, haina maji, haina umeme, haina *dispensary*, haina hata ile skuli ya *nursery* hakuna. nishasema mpaka nimeshachoka. Kwa bahati mbaya sana mimi siku ya kwenda huko labda nivae nguo maalum za kwendea kule.

Namuomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ajaribu kuzungumza na hizi sekta za Serikali wawasaidie wale watu, vyenginevyo watapoteza imani na nchi yao. Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi naunga mkono bajeti.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa hii ya kuwa mchangiaji wa mwisho kwa siku ya leo kuhusiana na hii hoja iliyokuwepo mbele yetu. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia hadi leo hii kuwa hai na hatimaye kutupa uwezo na nguvu wa kuondoka katika maeneo yetu mpaka katika jengo hili tukufu, kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru Allah.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Naibu Spika, nadhani nitakuwa mchache wa shukuruni kama sikuitumia fursa hii kukushukuru wewe. Na sio kwa kunipatia nafasi ya kuchangia leo hii sio kwa hilo tu, lakini kwa jinsi ulivyo makini katika suala zima la kusimamia mijadala humu Barazani. Kwa hilo Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Laiti ingelikuwa nina uwezo wa kuwashauri wakuu wa hivi vyuo vyetu hapa Zanzibar, basi baina ya wewe na Spika, ningeshauri mtunukiwe digirii ya uzamivu katika masuala ya uendeshaji Baraza na Mabunge. Baada ya bibaji hiyo ndogo Mheshimiwa naomba sasa moja kwa moja niende katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani nianze na hali ya kisiasa, naomba niungane na Mhe. Waziri ambaye kwa kweli Zanzibar hali ya kisiasa imetengamaa, pametulia Zanzibar, tumeacha tofauti zetu za kisiasa kama alivyosema Mhe. Waziri. Sasa tunachokiangalia maendeleo ya nchi hii. Wananchi wao hawana tatizo wao wanataka maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, katika nchi kuna tabaka mbili, kuna wananchi na viongozi. Ili amani ipatikane katika nchi kila mmoja ana dhima yake. Ama sisi wananchi tumeshatulia huku, tunachokitaka ni maendeleo. Lakini inaonekana kwamba umakini wa viongozi wetu katika kutusimamia na kutuongoza inaonekana ni tatizo kidogo. Hii imani iliyopo inaonekana inaweza kupungua kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa mwana falsafa mkongwe wa nchi hii Bwana *Shaban Robert* naomba Mhe. Naibu Spika, uniruhusu kidogo nimnukuu maneno yake katika kitabu chake cha Adili na Nduguze. Kwa mujibu wa Shaban Robert, ni kwamba:

> "Mfalme ni Naibu wa Mungu Duniani, kwa hiyo ufalme ni amana kubwa. Amana hiyo ilitaka uangalifu mkubwa kwa sababu ni dhima bora iliyowekwa mikononi mwa mwanadamu. Wajibu wa kwanza wa mfalme ni kuwa muadilifu katika matendo yake. Kila tendo jema au baya ni mfano wa raia wake"

Mhe. Naibu Spika, moja katika ya tendo adhimu kwa kiongozi ni kugawa haki sawa kwa wananchi wake bila ya kujali rangi, kabila au jiografia ya mtu anapotoka. La kusikitisha na hili tumeshalipigia kelele sana tangu miaka ya 1990 katikati mpaka mwishoni mwa miaka ya 1990, ilikuwa tunaieleza serikali jinsi ya ilivyokuwa ina ubaguzi kwa raia wake. Jambo ambalo linawapotezea wananchi haki zao za msingi.

Mhe. Naibu Spika, kuna tatizo kubwa la vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, wanatubagua viongozi hawa. Hatujui kwa misingi gani. Mimi mwaka 1999 nilimueleza Mkurugenzi wa vitambulisho vya Uzanzibari, nikamwambia katika Wilaya yangu zaidi ya watu elfu tano (5,000) hawana vitambulisho na wanazo sifa. Akanambia mimi ni muongo. Mhe. Naibu Spika, akanitaka nimpe ushahidi wa watu kama kweli ninao nimuoneshe watu. Tukaagana nimpelekee watu 5,000 katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chakechake mwaka 1999 kwenye mwezi wa 10. Kama mtafungua kwenye televisheni ya ITV kama wanazo kumbukumbu vile mnaweza ukaona. Nikampelekea umati wa watu waliokuwa hawana vitambulisho, Mohammed Jumanne alikimbia akaja zake Unguja.

Mhe. Naibu Spika, sina imani nae Mohammed Jumanne sina imani nae kwa hili. Mkurugenzi wa Vitambulisho sina imani nae, na hapa ndipo patakapoanza fujo sasa. Badala ya kwamba kumeshakuwa salama, sijui tumeondosha tofauti zetu za kisiasa, Lakini sasa tunataka kuingia barabarani kudai haki zetu za vitambulisho, na mimi nitakuwa Imamu wao. Inasikitisha sana Mheshimiwa, leo Mmasai anapewa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, Mkenya, leo Mtumbatu na Mpemba hawapewi. Aibuu

Hili tunakuomba Mhe. Naibu Spika, mimi likimaliza Baraza mara hii nimeshasema serikalini sana sisikilizwi. Sasa nakwenda kuutayarisha Umma kwa kudai vitambulisho katika njia ya kwenda moja kwa moja tukalale Ikulu mpaka Rais atupe. Nitafanya hivi kupitia mikutano ya hadhara kuushajihisha umma, nitafanya hivi kupitia maandamano.

Naomba Mhe. Naibu Spika, mnisaidie bendera nisije nikapachika bendera za *CUF* nikaja nikaambiwa nafanya mikutano ya CUF, naomba bendera za Wawakilishi kama zipo, zile kubwa mnipatie na miye kwa sababu nataka kutayarisha mikutano ya hadhara kuutayarisha umma kudai haki zao. Sasa kama ikiwa mtu kudai haki yake atapigwa mabomu basi kwanza nataka nife mie hapa.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye Muungano. Kwanza mimi msimamo wangu siutaki Muungano, ni lazima nieleze wazi msimamo wangu. Miongoni mwa jambo ambalo silitaki katika nchi hii ni muungano. Nina sababu zangu nyingi, ninazo za kisheria, ninazo za kijamii. Sababu za kisheria wataalamu akina Mwanasheria Mkuu pale anajua zaidi. Lakini kwa kadri ninavyofahamu mimi muungano huu ulikosa uhalali 1964 *up to date* hauna uhalali. Kwa *Articles of Union* zilitakiwa ziwe *ratified* na Baraza la Mawaziri kule halafu na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar nalo li-*ratify* kwa mujibu wa Aboud Jumbe Mwinyi; aliyekuwa Rais wa Zanzibar katika kitabu chake cha *The Partnership*. Hakuna kikao chochote cha Baraza la Mapinduzi.
Namnukuu Bwana Aboud Jumbe akisema. "Mimi nikiwa Rais hakuna kikao chochote cha Baraza la Mapinduzi kilichofanyika ku-*ratify Articles of Union*, kwa mujibu wa Bwana Aboud Jumbe Mwinyi, Mwenyezi Mungu amjaalie awe mzima tuwe nae katika mambo haya. Hazikuwa *ratified* kwa hivyo unakosa *legitimacy*, kule tulikutana

na Baraza la Mawaziri Tanganyika. Lakini huku Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa bwana Aboud Jumbe kwenye kitabu chake cha *The Partnership* hazikuwa *ratified*. Kwa hivyo huu muungano ni haramu *since 1964 up to date*.

Jengine ambalo mimi unanifanya niukatae kata kata Muungano huu ni jinsi unavyotubagua Wazanzibari. Wazanzibari Muungano huu unatubagua, unatupiga mafungu. Nafasi nyeti kabisa katika nchi hii zikiwemo *CDF*, *IGP*, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri Mkuu hata siku moja hajawahi kutokea kutoka huku kwetu Zanzibar, wakati watu wenye uwezo wa kuhodhi nafasi hizo tunao. *CDF* tulikuwa tunao humu kina Brigedia Yussuf Himid alikuwa akitembea na bastola mbili mbili, alikuwa ana uwezo huyo u- *CDF*.

Kamishna Edington Kissasi alikuwa ana uwezo wa kuchukua IGP, hakupewa. Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa mimi naamini Kamanda Hija anaweza hii nafasi, hatupewi, halafu ning'ang'anie tu. Muungano wa sampuli hii haufai kabisa kabisa, unanuka, unatudhulumu Wazanzibari. Mheshimiwa hili ni Jinamizi la uchumi wetu limeukalia. Jinamizi hili uchumi wetu limeukalia jinamizi hili.

Waheshimiwa hivi sasa niwambie kwamba hapa Baraza lililopita tumepitisha kwamba mafuta wanayatoa kwenye Muungano. Leo mafuta kila kukicha wanaomba kilomita ngapi waongozwe wanatufanyia sisi ujanja. Halafu tukae tu hivi hivi tuseme tunataka muungano, tunataka muungano. Mie muungano siutaki kabisa kabisa muungano huu. Kuna zile 4.5% aje atueleze hizi taratibu wanavyotugaia hizi wanatugaia kinamna gani. Halafu pesa za rada tutapewa lini siye zaidi ya bilioni ngapi.

Mimi nadhani niwambie Wazanzibari wenzangu wao wakiwa hawataki muundo, mie siutaki kabisa. Sasa itakapokuja Tume hii ya kuratibu maoni kwanza nawaombeni sana Wazanzibari tuwacheni tofauti zetu. Tuungane pamoja tujiondoshe katika jinamizi hili. Kila mtu atakuwa ana mawazo yake, nyie wengine mtakuwa mnautaka na wengine hawautaki muundo, mie siutaki kabisa kabisa. Twendeni tukatoe maoni, mkishakuamua hivyo hivyo mtakavyoamua, basi tunawahakikishia sisi Wawakilishi wenu tutasimamia maamuzi yetu.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe tanbihi ya kitu kimoja. Pale Wazanzibari watakapoamua kwamba mawazo yao ni haya katika muungano, mawazo hayo ndiyo tutakayoyasimamia. Mkija mkiyachezesha mawazo ya wananchi, basi ni lazima tutaondoka na nyie mbele kwa mbele, pataruka kivumbi, kabisa kabisa. Sisi tutasimamia mawazo yenu wananchi. Serikali wakiyapindisha basi pataruka kivumbi. Hili tunawaahidi Waheshimiwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, sasa twendeni katika migogoro ya ardhi, katika ukurasa wa 12 Ibara 23. Mhe. Waziri amezungumzia migogoro ya Ardhi. Mheshimiwa kama kuna tatizo ambalo linanyemelea nchi hii ni migogoro hii ya ardhi. Hivi ninavyokwambia Mheshimiwa ndio kama unavyosikia sehemu za Kaskazini Unguja. Juzi kwa mujibu wa kwenye semina alivyotueleza yule mwakilishi wao akina mama hawana raha kule ya kuishi na waume zao. Ardhi imechukuliwa wakapewa wageni, wakaajiri watu kutoka Kenya, wanawake wanakuja zao kutoka Kenya. Basi wale kina mama wa Tumbatu na Wanungwi hawana raha. Waume zao inakuwa ni tatizo. Wanafanywa watumwa katika ardhi yao, tunafanywa manokoa katika ardhi zetu. Hapa nadhani hili suala ni zito, mie katika Jimbo langu la Wawi tatizo hili ardhi ya Makaani katika *Coastal Plane per Eastern Coast* ya Pemba, watendaji wa serikali na watendaji wa Wilaya, wameshaichukua ardhi wanakaa wanatafuta watu wawauzie.

Mimi nasema nimeshaleta hili kwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, yeye mwenyewe nilimletea tatizo hili kwamba wakulima wamenyang'anywa ardhi zao. Nashukuru Ofisi ya Mhe. Makamo wa Pili Waziri wake Mhe. Mohammed Aboud kaja mpaka kule kaliona tatizo. Naomba tu sasa serikali ifanye matendo katika kulitatua tatizo hili. Sio kwa maneno tu kwa sababu mpaka sasa hivi naona napigwa maneno tu. Umma unazuia matumizi yote ya ardhi Makaani mpaka Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais itoe suluhu pale. Kinyume na hivyo aliyekwisha kununua ardhi ile basi asije akaikaribia na mie ndiye kamanda wa kuilinda kule.

Kupitia Baraza hili Mhe. Naibu Spika, nawaomba sana wale waliozuia ardhi katika eneo la Vitongoji Makaani wasije wakaigusa ardhi ile, mpaka Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais itakapotoa suluhu ya ardhi ile waliyoing'ang'ania watendaji wa serikali, waliyoing'ang'ania wanasiasa ili wawauzie Wazungu, sisi watufanye watumwa katika ardhi yetu, hili hatukubali. Hatuwezi kuwa manokoa katika nchi yetu wenyewe. Kama wameshafanya makosa huko, basi wasije wakakosea tena Vitongoji, patazuka kivumbi. Nasema tena patazuka kivumbi.

Mimi kwa sababu mzee wangu namuheshimu sana Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, lakini nimeshampelekea mpaka wahusika walionyang'anywa ardhi hii, keshawaona yeye mwenyewe. Inaonekana kwamba kwani anagitagita nini katika kunipatia suluhu. Mimi nashauri iundwe Tume iende ikachunguze tatizo la ardhi katika maeneo ya jimbo la Wawi. Kinyume na hivyo ni kusababisha maafa. Ahsante .

Mhe. Naibu Spika: Kabla hatujaakhirisha kikao kuna tangazo kaleta Katibu wa Baraza la Wawakilishi, kwamba kuna Waheshimiwa waliombwa namba za *account* za umeme hawajaleta wale waliokuwa hawana TUKUZA. Kwa hivyo wanaombwa walete ili waweze kutengenezewa mita za TUKUZA. Baada ya tangazo hilo naakhirisha kikao hadi kesho siku ya Jumanne tarehe 26/06/2012, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 26/06/2012 saa 3:00 za asubuhi)